ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 10 Oktoba, 2012

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

WIMBO WA TAIFA

KIAPO CHA UAMINIFU

(Mhe. Spika, baada ya kutaja jina la Mheshimiwa Mwakilishi anayetaka kuapishwa, Waheshimiwa Wajumbe wa Chama cha CUF wote walitoka nje ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi)

(Waheshimiwa Wajumbe wa Chama cha CCM na wao baada ya kuona Wajumbe wa Chama cha CUF wanatoka nje ya ukumbi wa Baraza walianza kushangiria kwa kusema CCM, yakifatiwa na makofi mengi)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: *Bismillahi Rahmani Raahim*. Mimi Hussein Ibrahim Makungu, naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za Uwakilishi na nitaitumikia kwa moyo wangu wote. Na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar. Naomba Mwenyezi Mungu unisaidie. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuchukua nafasi hii kumkaribisha sana ndugu yetu, mwenzetu, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ili ashirikiane nasi katika Baraza hili, katika shughuli zake za Uwakilishi wa Jimbo la Bububu.

Waheshimiwa Wajumbe, kama mnavyofahamu nafasi hiyo ilibakia wazi baada ya kifo cha ndugu yetu, mwenzetu marehemu Mhe. Salum Amour Mtondoo. Baada ya uchaguzi uliofanyika tarehe 16/09/2012 matokeo yaliyotolewa na Tume ya Uchaguzi ni kwamba ndugu yetu Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ameshinda nafasi hiyo. (*Makofi*) (*Vicheko*).

Pili naomba nichukue nafasi hii kuwaomba radhi sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba mafundi wangu wameniarifu mapema kwamba kumetokea hitilafu ya mitambo kwamba ZBC yenyewe imekuwa ina matatizo na kwa maana hiyo na sisi tumeshindwa kuunganisha ili kuonesha moja kwa moja. (*Makofi*/*Vicheko)*.

(Waheshimiwa Wajumbe wa Chama cha CUF hapa baada ya kumaliza kuapishwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Bububu Hussein Ibrahim Makungu walirejea ndani ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huku wakipigiwa makofi na Wajumbe wa Chama cha CCM)

Mhe. Spika: Baada ya Waheshimiwa Wajumbe wenzetu kuingia sasa naomba nitoe taarifa kwamba ZBC wametuarifu kwamba wamekuwa na matatizo kwa kuweza kuturusha hewani moja kwa moja kuhusiana na matukio hayo. *(Makofi/Vicheko).*

Hapana shaka Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo atatupa taarifa baadaye juu ya nini kilichotokea kiasi cha kwamba ikawa haikuwezekana kurusha moja kwa moja matukio muhimu ikiwa ni pamoja na kuapishwa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Ambaye ameshinda katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Bububu.

Pili nataka Waheshimiwa Wajumbe nikupeni taarifa rasmi, kwamba Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ambaye tumemuapisha hivi punde tarehe 10/10/2012 ndio tarehe ambayo alizaliwa yeye. Kwa hiyo amezaliwa kwenye Baraza hili na anasherehekea tarehe yake ya kuzaliwa.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, amefuatana na hawa wafuatao:-

1) Bi Hatun Ibrahim Makungu — Mama yake Mzazi
2) Bi Warda Hussein — Mkewe
3) Bi Sada Ibrahim Makungu — Dada yake wa familia
4) Ndugu Annur Ngina — Mjomba wake
5) Ndugu Mjumbe Msuri Mjumbe
6) Ndugu Yahya Saleh Issa — Katibu Wilaya
7) Ndugu Mgeni Mussa Haji
8) Ndugu Haji Khamis Dawa — Mwenyekiti wa Jimbo la Bububu
9) Mhe. Juma Sururu Juma — Mbunge
10) Ndugu Moh'd Abdalla Khamis — Mwenyekiti wa Kampeni
11) Ndugu Mwinchumu Mikidadi Habibu
12) Ndugu Omar Ibrahim Kilupi
13) Mhe. Fatma Adam

Waheshimiwa wageni wa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, karibuni sana katika shughuli hii kwa bahati mbaya kumetokea hitilafu ya masuala ya kuonesha moja kwa moja tukio hili na pia hitilafu ya umeme ambayo bado haijakaa sawa. Lakini angalau tumekuwa tunawasiliana.

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe kama mnavyoelewa kwa mujibu wa kanuni zetu katika Mkutano wa Nane wa Baraza la Nane la Wawakilishi ulioanza tarehe 13 Juni 2012, Baraza lilpitisha Mswada mmoja wa Sheria ambao ni kama ifuatavyo.

Mswada wa Sheria wa Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi bilioni mia sita na arubaini na nane mia tisa na arubaini na tatu milioni, mia saba na tisini na nane elfu kutoka mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30, Juni 2013 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kama inavyotakiwa na sheria chini ya kifungu 90(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012. naomba kutoa taarifa kwamba Mswada huo sasa umekuwa ni Sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nawashukuru sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 11Agosti, 2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Mswada wa Sheria Kuhusiana na Hifadhi na Usimamizi wa Vihatarishi vya Afya ya Jamii na Afya ya Mazingira na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla sijawasilisha Hati Mezani naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana, sana Mwakilishi mpya Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, hongera sana.
Baada ya hayo sasa naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria Kuhusiana na Hifadhi na Usimamizi wa Vihatarishi vya Afya na Jamii na Afya ya Mazingira na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 28

Tatizo La Wizi Wa Ng'ombe Katika Jimbo La Wawi

Mhe. Saleh Nassor Juma: Aliuliza**:-**

Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Wawi katika Vijiji vya Umangani, Kibokoni, Vunjamembe, Matungu, Uwandani, Vikunguni, Furaha, Ditia na kadhalika wameekeza nguvu zao katika mifugo na mbuzi. Kwa kuwa hivi sasa katika maeneo hayo kumekuwa na wimbi kubwa la wizi wa ng'ombe na kwa kuwa ng'ombe hawa wa wizi huchinjwa na hatimae kuuzwa nyama kwenye mabucha badala ya kuuzwa ng'ombe mzima jambo linalozidi kuchochea wizi huo. Na kwa kuwa vijana wetu katika ulinzi shirikishi hutoa taarifa za wizi huo kwa Masheha pamoja na Kituo cha Polisi.

(a) Je, ni kesi ngapi za wizi wa ng'ombe zilizopo katika kituo cha Polisi Chake Chake na ni ngapi zilizopelekwa Mahakamani na kuhukumiwa.

(b) Je, kuna bucha zozote zilizotuhumiwa kwa wizi huo na wanaozilimili kuhojiwa na Jeshi la Polisi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu
Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kwanza nichukue fursa hii na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa kuapishwa rasmi leo hii na vile vile kwa kushinda katika jimbo la Bububu, namtakia mafanikio na kumuhakikishia mashirikiano yetu kwake kwa maendeleo ya wananchi wa Bububu na Zanzibar kwa jumla.
Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kwanza nieleze yafuatayo:-

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Wawi hususan katika vijiji vya Umangani, Kibokoni, Matungu, Uwandani, Mikunguni, Furaha, Ditia na kadhalika kutokana na juhudi zao za kuwekeza katika mifugo ya ng'ombe na mbuzi. Aidha niwapongeze kwa dhati kabisa vijana wetu wanaoshiriki katika Ulinzi Shirikishi (Polisi Jamii) nawaomba waendelee kutoa taarifa za uhalifu au wizi unaotokea katika maeneo yao ili kukomesha vitendo viovu vinavyodhoofisha juhudi za wananchi katika kujikwamua kiuchumi na kujenga maisha bora.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 28 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuanzia mwezi wa Januari hadi Septembar 2012 kituo cha Polisi Chake Chake Pemba kimepokea malalamiko manne ya wizi wa mifugo na yote yameshapelekwa Mahakamani ambapo malalamiko matatu tayari yameshatolewa hukumu na lalamiko moja bado linaendelea kusikilizwa Mahakamani.

(b) Mhe. Spika, jeshi la Polisi linaendelea kufanya upelelezi kutokana na taarifa zinazotolewa na wananchi kuhusu wizi wa mifugo pamoja na mabucha yanayouza nyama za wizi. Hatua za kisheria zitachukuliwa

kwa yoyote atakayethibitika na wizi huo. Aidha elimu kwa umma itaendelea kutolewa ili wananchi waelewe umuhimu wa kutii sheria na kuacha vitendo viovu vinavyoathiri maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu masuri sana ya ndugu yangu Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba kesi zilizopokelewa na kufikishwa Mahakani ni nne tu miongoni kwa kesi nyingi ambazo ziliwasilishwa katika jeshi la polisi katika kituo cha Chake Chake. Kwa kuwa kuna vijana wengi ambao hupelekwa polisi na hatimaye kupelekwa Mahakamani na baadaye kesi zikafifia na kuonekana vijana hawa wanadunda mitaani huku wakijisifu pamoja na kuendeleza wimbi la wizi wa ng'ombe zetu. Je, isingekuwa vyema kwa serikali ikaturuhusu hawa vijana inaonekana kwamba Mahakama zetu zimeshindwa kuwashughulikia, basi ikaturuhusu kuwahukumu wenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, bado jeshi la polisi lina uwezo mkubwa wa kushughulikia matatizo yanayojitokeza. Pale ambapo imetokea kasoro ya aina yoyote ya utekelezaji wa kazi zao. Serikali haitosita kuwasiliana na jeshi la Polisi ili kuhakikisha kwamba tunakomesha vitendo hivi vya uhalifu wa wizi hasa wa mifugo ambavyo vimekuwa vikiendelea huko kisiwani Pemba, ili wananchi wetu waweze kuendelea na shughuli zao za ufugaji katika mazingira yaliyo mazuri zaidi. Nataka nimuhakikishie Mhe. Saleh Nassor, kwamba kesho tu nitaenda Pemba walifatilie jambo hili ili tuone undani ulivyo.

Mhe. Spika, katika kesi ambazo zimekwenda Mahakamani kesi tatu ambazo zilipata ufumbuzi, wahusika wenyewe ndio waliokwenda kuomba kesi hizo ziachiwe, sisamehewe.

1) Kesi ya Kwanza ya Wizi wa mbuzi mmoja aliyeibiwa huko Pujini Chake Chake. Muhusika aliiomba Mahakama isiendelee na kesi hiyo.

2) Vile vile kesi moja ya ng'ombe iliyotokea Uwandani Vitongoji, mlalamikaji aliiomba Mahakama kwamba kesi imalizike.

3) Kesi ya tatu ambayo ni ya wizi wa ng'ombe mmoja iliyotokea Gombani, hii aliomba Mahakama isiendelee kwa sababu aliyeiba ni mtoto wake.

4) Kesi moja bado inaendelea ya wizi uliotokea huko ziwani.

Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba vitendo hivi vya wizi wa mifugo vinapigwa vita sana na serikali yetu na hatutovumilia kuona kwamba vinaendelea katika nchi yetu.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sheria inaonekana kuwa na mapungufu ya kutoa adhabu, je ni lini serikali itaifanyia mapitio sheria hiyo ili kuipa nguvu sheria hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sheria kwa sasa inavyoonekana haina mapungufu isipokuwa tatizo linalojitokeza ni ile ile imani ya wananchi wa Pemba katika kuhurumiana. Kesi ishakuwa mahakamani kosa limeshaonekana, Polisi imeshapeleka kesi mahakamani mlalamikaji mwenyewe anaomba kuondosha kesi hiyo. Hilo ni tatizo ambalo tunalo inabidi sasa tutoe elimu kwa umma ili wananchi waelewe utaratibu wa sheria uchukue mkono wake na wale wakosaji wapate adhabu inayostahili.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa ruhusa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala hili limeenea sana kisiwani Pemba, lakini na hata Unguja lakini cha kusikitisha wananchi hawa wanapomkamata mwizi huchukua hatua mikononi mwao bila ya kufika katika vyombo vya sheria. Je, Mhe. Waziri huoni kama hili ni kosa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuchukua hatua mikononi ni kosa kwa mujibu wa sheria wananchi waendelee kuviamini vyombo vyetu vya sheria na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili hatua za sheria zichukue mkondo wake na wanaohusika kufanya makosa wahukumiwe kwa mujibu wa sheria, kufanya vyenginevyo ni kwenda kinyume na sheria.

Nam. 19

Kuanzishwa Mfumo wa Recycle

Mhe. Saleh Nassor Juma– Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imejenga msingi unaokusanya maji machafu na ya mvua kuanzia Msingini hadi Kichungwani katika mji wa ChakeChake. Na kwa kuwa maji hayo hatimae hukusanywa kwenye Mabwawa maalum na hatimae kuchunjwa na kuachiwa yaingie baharini yakiwa salama. Na kwa kuwa Kisiwani Pemba bado kuna tatizo kubwa la maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, mifugo na mashambani.

Je, ni lini Serikali itatutayarishia miundombinu ya kuyarejesha (Recycle) maji yale kwa ajili ya matumizi ya binaadamu, mifugo na kilimo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa swali lake namba 19 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Miundombinu ya kusafisha maji machafu ipo ya aina nyingi na ujenzi wake hutegemea uwezo wa nchi. Ipo miundombinu ambayo husafisha maji machafu kutoka vyooni na sehemu nyengine mbali mbali hadi kufikia viwango vya kuweza kurejesha maji yaliyosafishwa kwa ajili ya kunywa, kupikia, kukoga, kilimo, mifugo na kadhalika bila ya kuathiri afya za watumiaji.

Hivi sasa miundombinu mingi ya aina hiyo inapatikana zaidi katika nchi zilizoendelea. Hii inatokana na ukweli kwamba miondombinu ya kusafisha maji machafu hadi kufikia viwango vinavyokubalika vya kuweza kurejesha maji yaliyosafishwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu ni ghali sana na ni vigumu kwa nchi masikini na zile zinazoendelea kumudu gharama za mitambo na miundombinu ya aina hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 19 kama ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi inapenda na ingefarajika sana kupata uwezo wa kutayarisha na kuendesha miundombinu na mitambo ya kusafisha maji machafu hadi kufikia viwango vya maji yaliyosafishwa kutumika tena kwa ajili ya matumizi ya binadamu (kunywa, kupikia, kukoga na kufulia mifugo na pia kwa ajili ya shughuli za kilimo). Hata hivyo hali ya uchumi iliopo hivi sasa inaviza nia njema hiyo ya Serikali ya kufikia faraja hiyo.

Ni matumaini yangu kuwa Serikali haitosita kutayarisha miundombinu na mitambo hiyo pale hali ya uchumi wa nchi itakaporuhusu jambo hilo kufanyika hapa Visiwani mwetu. Tumuombe Allah aturuzuku uchumi mkubwa wenye kheri na sisi ili tufikie azma hiyo ya kuwa na miundombinu ya kusafisha maji machafu itakayosafisha maji hayo na kufikia viwango vya maji yatakayosafishwa kuweza kutumika tena kwa matumizi mbali mbali ya binaadamu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa maji yanayosafishwa kutoka katika mtaro ule wa msingini Chake Chake na hatimae kumwagwa baharini huwa hayakeri katika suala zima la umwagiliaji maji katika shughuli za kilimo za mboga mboga. Na kwa kuwa amekiri kwamba miundo mbinu ya kuyafanya maji yale kuwa safi ya kunywa serikali haina uwezo. Je serikali haina uwezo hata wa kuchimba malambo kama wanavyofanya wenzetu Bara vile wakachimba malambo na kuyahifadhi maji yale kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mboga mboga pamoja na ufugaji. Hilo moja.

La pili Mhe. Spika, kwa sababu Waziri kakiri mwenyewe kwamba serikali haina uwezo, na kwa kuwa tatizo la maji bado lipo je haoni kwamba serikali badala ya kuwashawishi wawekezaji kuja kujenga mahoteli tu humu na kusababisha kupotea maadili ya kizanzibari, isingekuwa vyema wakawashawishi kuwaleta wale wawekezaji katika kuyachuja maji machafu na kufikia kiwango cha ku-*recycle* kwa ajili ya matumizi mazuri zaidi ya kunywa na mambo mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante Mhe. Spika, suala alilozungumzia kwamba ni kweli maji yale yangeweza kutumika katika shughuli za kilimo lakini vile vile utaratibu wa kuweza kuyaondoa pale na kuyajengea malambo na kuweza kuyafikisha katika shughuli za kilimo nao ni utaratibu ambao una gharama. Na serikali itaangalia njia bora ya kuweza kushirikiana na wizara husika ambayo ni Wizara ya Kilimo, lakini pia Wizara ya Miundombinu kuweza kuona kwamba matumizi bora ya maji ambayo yanatoka pale kama yatawezekana basi yaweze kutumiwa, ushauri wake tunauchukua kwa ajili ya kuufanyia kazi.

Mhe. Spika, ni mara nyingi nchi ambazo bado hazina uchumi ulio bora unawategemea wawekezaji katika shughuli zake mbali mbali. Ni kweli kwamba sasa takataka za maji maji na takataka ngumu ni mali kwa maana kwamba zinaweza kuwa *recycle* zikarudishwa kwa ajili ya matumizi mengine. Ushauri wake tunauchukua na kama basi yeye pia anayo *idea* ya wawekezaji ambao anawafahamu si vibaya akatueleza ili tukaweza kufanya majadiliano nae kuhusu uwekezaji huu. Kwa sababu suala la wawekezaji pamoja na kwamba serikali inatafuta zaidi *interest* hujengwa na wawekezaji wenyewe jinsi gani ya uwekezaji wanaotaka kuja kuwekeza katika sehemu hizi ukilinganisha pia jinsi gani wataweza kurejesha fedha ambazo wataziwekeza katika miradi ambayo wao wenyewe wanapenda kuiwekeza.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, ninashukuru kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Waziri swali moja lenye sehemu (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa lengo kubwa la mradi ule ulikuwa ni kukusanya maji machafu yanayotoka majumbani na hatimaye kuyakusanya katika bwawa maalum katika eneo la Mkokota ngozi.

Na kwa kuwa ndani ya kipindi kifupi imebainika kwamba mtaro ule umekuwa ukiziba mara kwa mara na kufora hali iliyopelekea kwa kweli mtaro wa zamani ambao ulikusudiwa kutumiwa maji ya mvua tu ndio huo ambapo sasa hivi utumike katika maji yanayotoka katika majumba ya maji machafu. Je Mhe. Waziri utakubaliana nami kwamba utaalamu mdogo ulitumika katika kujenga mtaro ule.

Pili, je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kwamba malengo yaliyokusudiwa kwa mradi ule hayakufikiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, suala analozungumzia la wananchi kutupa taka katika mtaro huo na kusababisha shughuli ile ya maji kutiririka vizuri kwenda katika mabwawa kuweza kusitasita ni kweli. Mimi binafsi na watendaji wangu tumefanya ziara na tumeligundua hilo. Ni wito wangu kwake kama akiwa Mwakilishi wa wananchi wa eneo hili ambalo mtaro huu upo kuweza kuwashajihisha wananchi kuachana na tabia mbovu ya kutupa takataka katika maeneo ambayo serikali na wao wenyewe wakiwa wananchi wamegharamika katika kuweka suala hili, ili mradi huu na uwekezaji huu ambao upo hapa uweze kuleta faida ambayo imetegemewa.

Vile vile ofisi yangu imeiandikia Baraza la Manispaa kuomba mashirikiano ya dhati kuangalia kwamba kila wakati mtaro huu unapitiwa na kuweza kusafishwa ili nia njema iliyokusudiwa pale iweze kupatikana.

Mhe. Spika, naomba nisikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba mradi huu tumeutembelea na kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa mradi huu umefikia malengo, umekamilika, na hivi sasa uchafu ambao ilikuwa ukisambaa wa maji machafu na takataka kutoka katika majumba yote yamekusanywa na yanapelekwa katika mabwawa maalum hatimae yanachujwa na kwenda baharini. Kilichopo ni kwamba wananchi waone uchungu na fedha zile ambao wao wenyewe wameshiriki katika kuchangia miradi ya TASAF, UNEP na wahisani wengine ili maendeleo ya mradi huu yaweze kuwa kama yalivyofikiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, asubuhi ya leo na mimi kupata fursa kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza Mheshimiwa ninamsifu sana mshindi wetu wa Bububu ninampa pongezi kubwa, lakini Mhe. Waziri pamoja na majibu yako mazuri je, serikali iko tayari kuipokea kampuni ambayo itafuata sheria zote za Zanzibar na kuweza kuondosha takataka maji na kila uchafu wa Zanzibar serikali iko tayari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni vyema sana Mhe. Mshimba aweze kuonana na taasisi inayohusika na masuala haya ya utupaji wa takataka kwa kuwa ofisi zetu ziko wazi, mawaziri milango yao ipo wazi, watendaji milango yao iko wazi, aliwasilishe vizuri na awalete hawa wawekezaji ambao wanataka kufanya uwekezaji katika shughuli hiyo ili tuelewane nao. Na kama watakidhi matakwa na haja ya serikali naamini kwamba serikali itafuata ushauri wake.

Nam. 41

Uwekaji wa taa za barabarani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub– Aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yoyote duniani huonekana uzuri wake kutokana na majengo yake, barabara zake pamoja na taa za barabarani zinazong'arisha mji wake wakati wa usiku.

Je, Serikali ina mipango gani ya kudumu ya kuhakikisha mji wetu wa Zanzibar unawekwa taa hizo katika barabara zake ambazo zitakuwa zikiwaka kwa siku zote.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba na mimi kumpongeza sana ndugu yangu Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, ninamkaribisha sana Barazani kwa kuuliza maswali ya Tawala za Mikoa.

Mhe. Spika, sasa naomba kuchukua fursa hii kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni swali lake nambari 41 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali katika kuimarisha huduma za taa za barabarani katika maeneo ya mji wetu wa Zanzibar ina mpango wa kudumu na madhubuti wa kuweka mfumo mpya na wa kisasa wa taa hizo ambao unatumia mifumo miwili kwa pamoja ambao ni kutumia nguvu za jua (*Solar energy Source*) na mfumo wa gridi ya taifa ili kuhakikisha Mji wetu wa Zanzibar unaweka taa ambazo zitakuwa zikiwaka kila siku.

Mpango huu wa kudumu unategemewa kuanza kutekelezwa mapema mwakani (2013) kwa awamu mbili tafauti. Maeneo yatakayonufaika na awamu ya kwanza ni Shangani, Mkunazini na Kiponda ambayo yapo katika Mji Mkongwe. Aidha, awamu ya pili mpango huu unalenga kuweka taa katika barabara za Amani hadi Kwabiziredi, Amani hadi Mwanakwerekwe, Mwanakwerekwe hadi Kariakoo, Mnazi mmoja hadi Kikwajuni.

Mpango huu utatekelezwa kupitia Mradi mkubwa wa uimarishaji wa huduma za Mjini (*ZUSP*) ambapo jumla ya USD 2,600,000, tayari zimeshatengwa kwa utekelezaji wa mpango huo. Mhe. Spika, mpango wenyewe unaonekana kidogo umechelewa na hivi sasa uko katika hatua ya kumtafuta mshauri elekezi akishapatikana yeye na tayari *objection* tumeshapeleka World Bank na tunatarajia wakati wowote watatujibu ili *consultant* wapatikane tena atafutwe mkandarasi. Kwa hivyo ni hatua nzuri sana.

Mhe. Spika, mpango wa kudumu wa kuweka Taa za barabarani za Michenzani pamoja na barabara ya Malindi hadi Mnazimmoja unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu kupitia ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambapo jumla ya YUAN 5,000,000 sawa na dola za kimarekani 791,850 au shilingi za Kitanzania zipatazo 1.2 bilioni zimetengwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kusaidia mradi huu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na ya kutia moyo, Zanzibar imekuwa ya mwanzo katika shughuli za kimaendeleo na baadae kushindwa. Tumeshuhudia TVZ televisheni ya mwanzo kuanza je, umejitayarisha vipi na *system* hii.

Pili, nataka kujua taa za barabarani zina umuhimu sana na wananchi wamekuwa wakipata shida sana kutumia taa za muangaza wa magari. Nani mwenye dhamana ni Baraza la Manispaa au Shirika la Umeme.

Tatu, kwa kuwa Mji Mkongwe ni jicho kubwa la watalii kuna mpango gani wa dharura wa kupeleka huduma za taa ikiwa Mji Mkongwe inang'ang'ania mambo mengi ukitaka kukata mti Mji Mkongwe unaambiwa eneo laMji Mkongwe, ukitaka barabara unaambiwa Mamlaka ya Mji Mkongwe. Je, na hii inahusiana na Mji Mkongwe Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ninashukuru kwamba Mwakilishi Jaku ingawa yuko Muyuni lakini anaishi Mji Mkongwe *alhamdulillahi* anataka Mji Mkongwe uwake na utawaka na tutaung'arisha hayo ndio madhumuni yetu.

Ninafikiri Mhe. Spika, suala la msingi ni kuung'arisha mji wetu na ndio kioo cha mji tunakubali. Sasa sisi tumejitayarisha na matayarisho mengine leo hivi Mhe. Rais wa Zanzibar anakwenda kuzindua uwekaji wa umeme huo mpya wa Kimarekani unatolewa na wamarekani. Kwa hivyo hiyo ni kuhakikishia kwamba umeme utakuwepo muda wote. Sasa na sisi ule mtandao ndio tunauweka kabisa, nakubali kwamba kulikuwa kiza kulikuwa kuna matatizo. Ninakumbuka tokea tulipokuwa wadogo pale wale wawashaji taa za barabarani walikuwa wanawasha na baskeli na kingoe kile kwaa huyo anapita. Lakini sasa zitawaka wenyewe na zitazima wenyewe Mhe. Jaku, kwa hivyo tumejitayarisha kwa mipango mizuri kwa mradi huu.

Anasema nani dhamana, ni kweli kwamba Shirika la Umeme wanataka watuuzie ule umeme, sasa hapo tutafanya mazungumzo na Baraza la Manispaa tuone kwamba tunafanikisha vipi hili suala lakini mji wetu uwe safi.

Amesema je kwa nini Mji Mkongwe tu, tunaanzia Mji Mkongwe na Miji mengine ikipata hadhi ya kuwa miji basi mambo haya yatafuata, mambo kidogo kidogo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali mawili yafuatayo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba Wizara yake ina mpango kabambe wa kuweka taa za barabarani ili kuung'arisha mji wetu. Lakini atakubali kwamba Ofisi yake chini ya Baraza la Manispaa imeshindwa hata kuendesha *stop light* ya Mkunazini na Malindi je, atawezaje kuendesha taa zote za barabarani katika Mji Mkongwe.

Pili, hivi sasa kabla ya huo mfumo mpya wa nishati wanaotegemea, taa za barabarani zinatumia umeme wa *ZECO* na kumekuwa na malalamiko kwamba Baraza la Manispaa hawalipi bill yao kwa *ZECO*, lini watalipa bill yao hii ili iingie kwenye mfumo mpya *ZECO* wawe tayari wamejipatia fedha zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba *stop light* za Malindi pamoja na Mkunazini zimekuwa zinatupa tabu kidogo na muda mrefu zimesita kuwaka. Nataka kusema tumejitahidi sana kutafuta uwezekano wa kuzitengeneza zile taa, lakini matatizo yaliyotokezea makubwa kwamba ile mitandao yake, unajua kuna baadhi ya vitu ukipewa msaada, msaada huukatai lakini uchukue *package* nzima, sasa tumepata matatizo pale unaambiwa *manual* yake anayo huyo mwenyewe *supplier* tumefuatilia.

Ninafikiri kama unavyokumbuka taa zile tumepatiwa na bwana Ali Youssuf, sasa tumemfuatilia sana lakini tumekwama mpaka tukaona tutafute njia nyengine ya kupata mtandao mpya kabisa. Kwa hivyo sasa dawa ya kudumu inakuja ya moja kwa moja ya kuziondoa zile na kuweka mtandao mwengine kabisa. Kwa hivyo ninakubali Mhe. Hija *observation* yake lakini sasa tumesema tusichukue *piece milk* tufanye kazi ya pamoja tulimalize lote lile suala. Hilo ndio tatizo lililotokezea.

Bill za *ZECO* kama alivyosema ni kweli kuna deni, hilo tutakaa pamoja na *ZECO* watafute njia ya kulimaliza deni la zamani na watafute njia za kuelewana, lakini mradi wetu upate kutengenea na mji wetu ung'are. Hayo yanazungumzika na yanafanyiwa kazi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Katika mpango wake wa kueneza taa katika miji ya Zanzibar kama vile Amani, Darajani, na Mkunazini je, serikali ina mpango gani wa kueneza katika miji ya Pemba kama vile Chake, Mkoani, Mtambile na Kangani. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwanajuma Mdachi wa viti maalum wanawake swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwanajuma kwamba mradi huu wa *ZUSP* kwa awamu hii kuna mambo maalum yaliyotengwa kwa miji ya Pemba. Kwa hivyo kuna mambo ambayo tutaanza nayo halafu haya yatafuata baadae mpaka Kangani kule nako kutawaka, madhali barabara imeshafika na taa zitafika tu tustahamili.

Nam. 21

Kupandishwa Daraja Hospitali ya Vitongoji

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Vitongoji Cottage Hospital ni moja kati ya hospitali itakayopandishwa daraja kutoka ya kijiji hadi ya Wilaya. Na kwa kuwa hakuna dalili zozote zinazoonesha kuchukuliwa na Serikali ili kutekeleza azma yake hiyo.

Je, Serikali inaweza kueleza zoezi hilo la kuipandisha hospitali hiyo daraja limeanza mwaka gani na linatarajiwa kumalizika mwaka gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mwakilishi wetu mpya wa Jimbo la Bububu na baada ya hayo uniruhusu nimjibu Mwakilishi Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi swali lake nambari 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hospitali za vijiji (*Cottage Hospital*) zinatakiwa zipandishwe daraja kuwa hospitali za Wilaya.

Hatua ya kuzipandisha daraja hospitali hizo zimeanza kuchukuliwa na kwa mujibu wa mipango hiyo upandishwaji wa daraja unaanza kwa zile wilaya ambazo hazina hospitali za wilaya. Na wilaya zenyewe ni Kusini na Kaskazini Unguja. Na kwa Pemba Micheweni, na zoezi limeanza 2011.

Hospitali ya Vitongoji zoezi hilo halijaanza kwa sababu ile ile kwamba Chake Chake pana hospitali ya Wilaya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa msingi wa kujengwa hizi *cottages* hospital ilikuwa ni kuwapunguzia matatizo wananchi wa vijijini pamoja na uwepo wa hospitali za Wilaya. Lakini kwa kuwa madhumuni na malengo ya milenia ni kuboresha afya ya mama na mtoto, na kwa kuwa hospitali ya Vitongoji *Cottage* pale haina hata ile *maternity ward* kwa maana ya ile *pre natal, labour na post natal*.

Kuna chumba kidogo sana ambacho kina mama akiingia mmoja tu mwengine asubiri mwenzake kujifungua. Je kwa kuendelea kukaa tu kwa kusema ipo hospitali ya Chake Chake pale haiendelei kuboreshwa si kwenda kinyume na malengo ya milenia pamoja na dhamira nzuri ya serikali ya GNU kuboresha hali ya afya ya mama na mtoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nijibu swali lake la nyongeza Mhe. Saleh Nassor Juma wa Wawi kama hivi ifuatavyo:

Ni sadakta na ni kweli kwamba lengo la Milenia ni kufanya hicho.

Wizara ya Afya imejiandaa kwa hilo lakini ukizungumzia suala la Vitongoji sehemu ya kuzalia ipo na shughuli zinafanyika, tunachohitaji hapa ni kuhakikisha kwamba na sehemu nyengine zinafikiwa ili watu waweze kuzalisha. Lakini kama tunazungumzia suala la kupandisha daraja hapa tutakwenda kwa awamu kwa sababu ndivyo uwezo wetu ulivyo, tutakwenda kwa zile hospitali ambazo hazina hospitali za wilaya na zile ambazo zina hospitali za wilaya zitafuata baadae, lakini kutakuwa na vituo vingi tu ambavyo wazazi watafika kwenda kuzaa. Katika vituo vidogo vidogo vya *PSU* na *PSU+*, kwa hivyo itabidi tufuate huo utaratibu kwa sababu kupanga ni kuchagua na uwezo unategemea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa Hospitali za *Cottage* zipo lakini zinakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa wataalamu na vifaa, mfano katika Hospitali ya Chake Chake tatizo ni ukosefu wa taa za *theatre* imeungua moja baada ya moja na huduma hivi sasa hazipatikani. Je, haoni kufukuzia kuzipeleka hospitali za madaraja ni kuwadanganya wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, taa za *theatre* anazozizungumza tayari zimeshawekwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi katika hospitali hii hakuna daktari mwenye uwezo wake?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Sijafahamu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru Mhe. Spika, kuweza kunirejesha tena kumuuliza Mhe. Naibu Waziri katika swali hili la nyongeza. Nauliza atakubaliana na mimi katika hii *Cottage* ya Vitongoji hakuna daktari ambaye ana ujuzi wake?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, changamoto ya wafanyakazi nafikiri kila siku tunazungumza kwamba hilo ndio tatizo la Wizara ya Afya, lakini kwa masuala ya uzazi wazalishaji wapo.

Nam. 32

Ujenzi Wa Barabara Jimbo La Mtambwe

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Kwa kupitia mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa Changamoto ya Millenium (*MCA*) kutoka Serikali ya Umarekani, Jimbo la Mtambwe limebahatika kujengewa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa km. 13.6. Barabara hiyo imeanzia Bahanasa – Daya, Daya – Makongeni na Daya – Mtambwe Kaskazini. Kutokana na kuwa kijiografia, wananchi wa Jimbo la Mtambwe wametawanyika katika vijiji mbali mbali.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuona kuwa barabara hiyo inatumika ipasavyo na kuleta tija iliyokusudiwa ya kuwaunganisha wananchi wa jimbo hilo.

(b) Kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla katika sekta hii ya uchumi Jimbo la Mtambwe ni moja kati ya majimbo yanayozalisha karafuu na mazao mengine ya chakula kwa wingi. Je, Wizara ina mpango gani wa kuendelea kuziimarisha barabara za jimbo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote na mimi naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mwakilishi halali wa wananchi wa Jimbo la Bububu, Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 32 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itazifanyia matengenezo pindi tu hali ya fedha itakapokuwa nzuri barabara zote ambazo vijiji vyake vinaunganishwa na barabara iliyoanzia Bahanasa – Daya, Daya – Makongeni na Daya – Mtambwe Kaskazini, ikifanikisha lengo la kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itazifanyia matengenezo barabara hizo pamoja na barabara za ndani pale hali ya fedha itakaporuhusu lakini pia tunaomba viongozi wa majimbo kwa kushirikiana na halmashauri husika tuendelee kufanya kazi kwa pamoja kwa kutambua kwamba barabara hizo za ndani ni jukumu la moja kwa moja lililo katika mikono ya halmashauri husika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata jibu zuri la swali langu, lakini Mhe. Spika, tukumbuke kuwa serikali kwa kutumia mradi huu unaofadhiliwa na *Millenium Challenge Corporation* imetumia mamilioni ya fedha kwa kutengeneza barabara hizo za Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwemo na barabara hii ya Mtambwe inayoanza Bahanasa – Daya, Daya – Makongeni na Daya Uondwe kwa madhumuni ya kuwaondolea shida wananchi na kuwapunguzia umasikini.

Lakini Mhe. Spika, barabara hii hata ikimaliza ni lazima ihudumikie watu waliomo katika vijiji mbali mbali ikiwa ndio jiografia ya Mtambwe ilivyo. Kuna barabara inayotoka Kinazini kupitia Mitambuuni ambayo mpaka ifike Makongeni ndio itaweza kupata huduma ya barabara hii, kuna kijiji cha Kivumoni barabara yake mpaka iungane na barabara hii kubwa ndio faida zitapatikana. Hivyo hivyo na kijiji cha Chanjaani, Kiapaka, Kidundo, Chekea, Jambaji, Nyali na barabara inayotoka Uondwe kupitia Kele mpaka Matuli.

Mhe. Spika: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Swali ni kuwa, kwa sababu barabara hizi hazijaumbwa leo ziko miaka yote, na mimi Mwakilishi wao muda mrefu hapa huwa nazipigia makelele lakini sijaona lolote lililofanywa. Je, si sawa kusema kuwa Mhe. Naibu Waziri ananijibu tu aonekane kuwa swali limejibiwa lakini hakuna azma ya matengenezo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa ni kweli, lakini msingi wa majibu ni kwamba kama serikali inashughulika zaidi na zile barabara kuu mimi ningeendelea kumuamini Mhe. Mwakilishi kwamba ataendelea kutupongeza kama serikali kwa kupitia wafadhili wa *MCC* kujenga barabara ile Kubwa. Na kwa upande wa barabara za ndani namuomba Mwakilishi tuendeleze ushirikiano wetu yeye mwenyewe ni shahidi maeneo ya Kele tumemjengea daraja kwa kushirikiana na wenzetu wa *TASAF*, barabara za ndani nyingi tumefanya mazungumzo mazuri tunaanza utaratibu wa kutia kifusi. Kwa hivyo, nikuombe tu Mhe. Mwakilishi barabara hizi za ndani tuendelee kushirikiana na wizara yetu, halmashauri na viongozi wenzako wa jimbo ili kuwapunguzia wananchi wetu changamoto zinazowakabili likiwemo suala la usafiri.

Lakini pia Mhe. Mwakilishi utakumbuka maeneo ya chini kule kulikokuwa kukisafirishwa karafuu kwa wingi, kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tuliweza kutia kifusi ili kuwapunguzia wananchi changamoto hizo za usafiri. Nikuombe sana Mhe. Mwakilishi tuendeleze mashirikiano yetu katika kuwapunguzia wananchi wetu kwa kutambua kwamba jukumu la barabara ndogo za ndani ni jukumu linaloangukia katika halmashauri, lakini wizara yetu iko tayari kutoa msaada wa vifaa, ufundi na watendaji kazi pale kila hali itakaporuhusu.

Nam. 1

Kukauka kwa Vianzio vya Maji

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo sugu la maji katika kila upande wa Zanzibar, na kwa kuwa serikali imekuwa ikitegemea zaidi vyanzo vya maji asilia ambavyo kwa sasa vimeanza kukauka kutokana na mabadiliko ya Tabia nchi.

Je, ni lini serikali itafikiria kuyachuja maji ya bahari na kuweza kutumika kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kama zinavyofanya baadhi ya nchi zilizoendelea pamoja na zile zinazoendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 1 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa serikali imekuwa ikitegemea zaidi vyanzo vya maji asilia ambayo kwa sasa vimeanza kukauka kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na hali hii si kwa Zanzibar peke yake.

Mhe. Spika, kuhusu kuwepo kwa tatizo la maji katika kila upande wa Zanzibar naomba kwa heshima na taadhima nisikubaliane na Mhe. Mwakilishi, hii ni kwa sababu kwa mujibu wa takwimu tulizonazo kwa sasa wastani wa wananchi asilimia 81 ya wananchi wa Zanzibar wanapata huduma ya maji safi na salama, ingawa kwa baadhi ya maeneo mengine maji hayo yanapatikana kwa mgao.
Aidha, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inafanya juhudi mbali mbali na kuhakikisha kuliondoa tatizo hilo kwa muda mfupi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa uwezo wa serikali katika kusambaza maji safi kwa wananchi wote ni mdogo mno hii ni kutokana na kwamba *ZAWA* hivi sasa ina madeni ya Shirika la Umeme (*ZECO)* ambayo wanashindwa kuyalipa.

Je, isingekuwa vyema kwa serikali kufikiria suala hili hii *ZAWA* kuibinafsisha na kupewa wawekezaji ili ikafanya kazi *efficiently* kwa wananchi hilo moja.

Pili, kwa kuwa Zanzibar tumezungukwa na maji ya chumvi ambapo wenzetu huyatumia maji haya kupitia *freshener distillation* kupata maji safi ya kunywa sambamba na chumvi ya mezani (*table salt*) pamoja na gesi ya *chlorine* ambayo inatumika viwandani. Je, ni lini serikali itafikiria suala hili la kufanya *freshener distillation* ya maji ya chumvi kusudi tukapata maji safi ya kunywa, gesi ya *chlorine* ya kuuza nje pamoja na mambo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kuhusu Mamlaka ya Maji kubinafsishwa hili ni suala ambalo sisi wizara tutakaa pamoja na tutalifikiria jinsi gani ya kufanya.

Lakini vile vile kuhusiana na suala la kufanya utafiti katika maji ya bahari, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tayari suala hilo imeanza kufanya. Kuthibitisha hilo, wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Wajerumani imeanza kufanya shughuli hizo kwenye Chuo cha Fedha Chwaka ambako tayari mradi huo kwa sasa hivi umeanza kutumika kwa kubadilisha maji ya chumvi kugeuza kuwa maji baridi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba siku hizi maji yanapatikana kwa gharama kutokana na uchache wake, lakini hivi karibuni tumeshuhudia magari ya maji safi ya serikali yakimwagia maji katika bustani za Michenzani. Je, wizara haioni kuwa ipo haja ya kuwasogezea wananchi maji haya badala ya kuyapoteza katika bustani za Michenzani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, serikali lengo kuu ni kuhakikisha kwamba huduma hii ya maji safi na salama inapatikana na katika kuwasogezea kwa yale maeneo ambayo yana matatizo mazito ya suala hili la maji, basi nathibitisha kwamba katika kipindi cha Mwezi wa Ramadhani nyinyi wenyewe mlikuwa mashahidi ambapo magari yetu tuliyasambaza katika sehemu zote ambazo zilikuwa zinakosa maji katika kipindi hicho. Kwa hivyo na sasa hivi tutajipanga katika kulishughulikia tatizo hilo na kuhakikisha kuwa tunaliondoa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kabla ya hayo nimpongeze Mwakilishi mpya aliyeapishwa leo lakini pamoja na Mhe. Jaku Hashim kutaja mambo matatu, lakini na la nne tumeongeza idadi yetu ya Chama cha Mapinduzi Wawakilishi wote. Baada ya hayo machache naomba kuulisa swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa umekiri katika majibu yako ya msingi kuwa kuna matatizo ya maji pamoja na miradi mikubwa ya *ADB, JICA* kukosekana maji katika mji wetu wa Zanzibar na vitongoji vyake. Serikali haioni haja sasa kutoa tamko kuwa Mamlaka ya Maji imeshindwa kabisa kuweza kuleta huduma hii bora na salama kwa wananchi.

(b) Kwa kuwa viongozi wa Majimbo, Wawakilishi na Wabunge wameleta huduma hii karibu zaidi na kwa ufanisi mkubwa. Je, atakubaliana na mimi sasa kuwa atoe tamko jengine hapa kuwa Mamlaka sasa ihamie kwenye majimbo wananchi waweze kukusanya pesa zao kwenye majimbo na kuleta huduma hii bora yenye ufanisi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri aliyokuwa akiendelea kuyajibu naomba kuchukua nafasi hii kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mhe. Spika, *ZAWA* haijashindwa kutoa huduma ya maji kwa wananchi na ndio maana asilimia yake ya wanaopata maji inaongezeka kila mwaka kutokana na jitihada mbali mbali wanazozifanya. Pia misaada tunayoipata kutoka wahisani mbali mbali nayo inatusaidia sana vile vile kuweza kueneza maji katika maeneo mengi. Tatizo lilikuwemo

katika suala la msingi ambalo Mheshimiwa wa mwanzo aliliuliza ni kwamba kuna mabadiliko ya tabia nchi na ni suala zuri sana ambalo mimi nimelipenda na ni vizuri Waheshimiwa hawa wajue kwamba sasa hivi kuna matatizo ya mabadiliko ya tabia ya nchi na maji katika ardhi yamepungua na uwezo wa visima vyetu kutoa maji umeshuka. Juzi tulikuwa na ziara na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kutembelea vianzio vya maji na tumeona kwa macho yetu namna gani maji yamepungua.

Suala la msingi alilouliza Mheshimiwa la kutengeneza maji ya chumvi ni suala ambalo tayari kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri *Pilot Project* imeanza kwa Chwaka na Kokota na kuna Wajerumani wametusaidia kuleta mashine ambazo zinasaidia kutengeneza hayo maji. Sasa hili ni tatizo sio kwamba *ZAWA* imeshindwa, *ZAWA* inajitahidi sana kutoboa visima vingi tu, lakini kwa bahati vinakuwa na matatizo.

Tatizo pengine linalokuwa linatokea ni kwamba wakati mengine unaweza ukakitoboa kisima mahala ambapo maji yake si salama kwa kunjwa kwa hivyo *ZAWA* wanakuwa wagumu kuendeleza kisima kile ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi huwa wanafanya. Kwa sababu katika maeneo yetu kuna sehemu ukichimba kisima utaweza kutumia mara ya mwanzo lakini baada ya muda mfupi tayari yanakuwa *contaminated* kutokana na vyoo vilivyozunguka katika maeneo yale.

Suala la kusema kuwa tamko litolewe ihamie kwenye majimbo Mheshimiwa bado sisi tunasema Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Wabunge jitihada yao wanayoifanya katika kuhakikisha kuwa watu wanapata maji tunaithamini sana, tunakwama wakati mwengine kutokana na uwezo wetu wa kifedha. Kwa hivyo, naomba waendelee kuisaidia *ZAWA* kama wanavyoisaidia hivi sasa. Ahsante sana Mhe. Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri wa Afya kuwasilisha Mswada ili kusomwa kwa mara ya pili yeye mwenyewe Mhe. Waziri ameniomba nitoe taarifa kwenu pamoja na kuwaonesha picha ambazo zinatisha sana za madhara yanayotokea kutokana na matumizi ya sigara. Zipo picha hapa ambazo zinaonesha ndugu mmoja ambaye eneo moja la shavu hapa limekufa kabisa na kuna donda kubwa mno na pengine pameharibika kabisa kabisa na nyengine mapafu yamekufa kabisa.

Nawaomba watendaji wetu wachukue hizi ili kuwapitishia Waheshimiwa Wajumbe waone na hiyo ndio hatari na madhara ya matumizi ya sigara. Kama kuna maelezo zaidi nafikiri Waziri mwenyewe anaweza akayatoa baadae. Lakini picha zinatisha mno. Baada ya hapo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunisaidia kufikisha ujumbe juu ya madhara ya sigara ambapo moja katika sehemu ya sheria hii tunazungumza jinsi ya kujikinga tusiyapate hayo Mungu akitujaalia.

Mhe. Spika, naomba nikushukuru na niishukuru ofisi yako kwa kupata nafasi ya kwanza katika kikao hiki mimi kufungua dimba ya kuwasilisha miswada itakayojadiliwa na sheria mbali mbali zitakazopitishwa katika kikao hiki.

Mhe. Spika, sheria iliyo mbele ya Wajumbe ambayo inaonekana ni kubwa kidogo ni sheria muhimu sana ambayo tunahitaji kuijadili kwa kina na kutoa michango ili itusaidie katika kutayarisha na kurekebisha masuala yanayohatarisha afya yetu. Kwa muda mrefu tumekuwa tukilalamika au tukilaumiana kwamba Baraza la Mji halitimizi wajibu wake kwamba maeneo ya mitaa taka hazizolewi, michirizi ina maji machafu na mambo mengi ambayo yanadhalilisha ustaarabu wetu wa Zanzibar. Sasa madhumuni ya sheria hii au mswada huu ni kuweka sheria itakayosimamia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii na wakati huo huo kunyanyua kiwango cha afya cha watu ndani ya Zanzibar.

Sheria ya Afya ya Jamii ambayo ilikuwepo zamani sura ya 73 imefutwa tokea mwaka 2006 kwa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya 2006 hata hivyo, masharti ya Sheria ya Afya ya Jamii hayakuwekwa vizuri katika sheria nyengine yoyote inayotumika, kwa kutoweka huko kumetoa pengo la msingi katika kushughulikia kwa

ufanisi masuala ya afya ya jamii. Pengo hilo linawezwa tu kuzibwa kwa kutunga sheria mpya inayohusiana na afya ya jamii na mazingira.

Mhe. Spika, hivyo mswada huu umetungwa kuweka njia bora za kulinda jamii dhidi ya vihatarishi vya afya ya jamii na mazingira na mambo yanayohusiana nayo. Sheria ina vifungu visivyopungua kumi na moja.

Kifungu cha kwanza kinaeleza tafsiri na masharti ya awali, kifungu cha pili kinaelezea usimamizi wa sheria, inatoa jukumu kwa Mkurugenzi Mkuu wa Afya kusimamia sheria, uteuzi na mamlaka ya afisa wa maeneo na kanda mbali mbali, wilaya na mkaguzi.

Kifungu cha tatu kinahusu usafi na makaazi ambapo waziri amepewa uwezo wa kuweka viwango vya usimamizi wa taka vitakavyoendana na kanuni za kimataifa za afya. Usimamizi wa taka za aina tofauti kama vile taka za gesi, maji na taka ngumu zinawekewa utaratibu. Vile vile inaelezea usimamizi wa taka za maambukizi hatari kitabibu, mifugo na kemikali za kilimo. Inatoa wajibu wa kutosababisha madhara kwa jamii kwa uangamizi wa taka ngumu na maji. Mwisho kinatoa uwezo na wajibu kwa mamlaka ya upangaji kuendana na viwango vya afya ya jamii kabla na baada ya ujenzi na kubomoa kusafisha mtaa wa ovyo.

Kifungu cha nne kinahusu usumbufu, kinaelezea kinga na marufuku ya kusababisha usumbufu au hatari kwa afya ya jamii na mazingira. Afisa mwenye mamlaka na Mkurugenzi Mkuu wa Afya wamepewa uwezo wa kutoa amri ya usumbufu kwa mhusika wa usumbufu, wakaguzi wamepewa uwezo wa kuingia katika jengo na kufanya ukaguzi vile vile mtu binafsi ana haki ya kufungua kesi mahakamani kuhusiana na usumbufu.

Mhe. Spika, kinga na kuzuia maradhi ya kuambukiza imeelezwa katika kifungu cha tano, kimempa uwezo waziri kutangaza maradhi ya kuambukiza na kuweka viwango na mbinu za kuangamiza taka za maambukizi. Pia kinaelezea ushughulikiaji wa mtu aliyeko katika chombo cha usafiri ambaye amekumbana na maradhi ya kuambukiza, vile vile inatoa masharti ya kuzima na kuchoma maiti na inatoa masharti ya lazima kwa uchunguzi wa kiafya kwa waajiriwa.

Kifungu cha sita kinatoa masharti kuhusiana na maradhi ya kutolewa taarifa kimataita na chanjo, ukaguzi na uchunguzi wa vyombo na wasafiri, chanjo kwa watu wanaoingia Zanzibar, chanjo ya dharura na uwezo wa wakaguzi kutembelea skuli wakati wa miripuko ya maradhi. Chanjo dhidi ya maradhi ya watoto imeelezwa kuwa inatolewa bila ya malipo, waziri anapewa uwezo wa kutangaza orodha ya maradhi ya kutolewa taarifa kimataifa.

Kifungu cha saba kinaeleza masharti ya kukinga na kudhibiti wadudu na panya, kupiga dawa na kupuliza kwa ajili ya kukinga maradhi. Pamoja na masharti hayo kuna masharti maalum yanayohusu katazo la uchafu katika makaazi.

Kifungu cha nane kinahusu maeneo ya kuzika, kinaelezea kuwekwa na kufungwa kwa maeneo ya kuzikia, maeneo ya kuzika ya familia, kukataza kuzika na kufukua mwili wa marehemu bila ya kibali na udhibiti wa uchomaji maiti. Waziri amepewa uwezo wa kutunga kanuni za usimamizi wa maeneo ya kuzika.

Sehemu ya tisa inatoa masharti ya udhibiti, bidhaa za tumbatu na ulevi ambazo vitayarishi vyake ndio kama vilivyosambazwa na Mhe. Spika. Inaweka udhibiti wa uingizaji, uuzaji, usafirishaji, utangazaji na usazambazaji wa bidhaa za tumbaku bila ya kuweka onyo la kiafya kwamba uvutaji wa sigara hatari kwa afya yako kwa lugha ya Kiswahili na kiingereza.

Inakatazwa kuvuta sigara katika maeneo ya umma na inaweka masharti ya lazima ya kuweka alama ya maeneo yasiyotakiwa kuvutwa sigara. Watoto kisheria ni wenye umri chini ya miaka 18 wamekatazwa kujishughulisha na uuzaji, usambazaji, uingizaji na utangazaji wa bidhaa za tumbaku.

Sehemu ya kumi inahusu huduma za afya za bandari. Inaanzisha Afisi ya Afya ya Bandari na kuelezea kazi za Maafisa wa Afya Bandari. Waziri amepewa uwezo wa kutunga kanuni za utekelezaji mzuri wa Afisi ya Afya ya Bandari.

Mhe. Spika, mwisho sehemu ya kumi na moja inaelezea masharti mengine yanayohusiana na adhabu ya jumla, kutoa *notice* na adhabu bila ya kushitakiwa ambapo mtenda kosa amekiri kosa atalipa faini kwa Mkurugenzi bila ya kushitakiwa Mahakamani.

Imeanzisha Baraza la Ushauri ya Jamii na Mazingira ambalo pamoja na mambo mengine limepewa jukumu la kumshauri Waziri kuhusiana na masuala ya afya ya jamii na mazingira.

Mwisho umeelezwa uwezo wa jumla wa Waziri wa kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, nachukua tena fursa hii kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele yetu ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya kamati juu ya Mswada wa Sheria ya Kuhusiana na Hifadhi na Usimamizi wa Vihatarishi vya Afya ya Jamii na Afya ya Mazingira na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, aidha ninapenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya kwa kuandaa na hatimaye kuweza kuwasilisha mswada huu katika kamati yetu ili kamati kutoa mapendekezo yake kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza letu tukufu.

Shukurani zangu za dhati pia kwa Wizara ya Afya kwa namna ambavyo wameisaidia kamati katika kuufahamu mswada huu pamoja na wadau mbali mbali waliowasilisha maoni yao kwenye kamati yetu. Jitihada zao hizo za kuiletea maoni kamati imeufanya mswada huu kufahamika kwa kiasi.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo napenda sasa kuwataja wajumbe wa kamati ambao tumeshirikiana katika kujadili mswada huu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu Haji	-	Mjumbe
4. Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Mjumbe
5. Mhe. Nassor Salum Ali	-	Mjumbe
6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
7. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
8. Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Mjumbe
9. Ndg. Asha Said Mohamed	-	Katibu
10. Ndg. Talib Enzi Talib	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya kuwataja Wajumbe wa Kamati natoa pongezi zangu za dhati kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuziwezesha Kamati zake za kudumu kukutana na wadau mbali mbali kuhusiana na Mswada husika ili kupata maoni yao. Kwa kweli maoni yao yamesaidia sana kamati zetu.

Mhe. Spika, sasa napenda niende moja kwa moja kwenye mswada. Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu ni kuweka sheria itakayosimamia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii na wakati huo huo kunyanyua kiwango cha afya ya watu wa Zanzibar na pia kuleta ufanisi katika kushughulikia masuala ya afya ya jamii na afya ya mazingira.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kwa muda mrefu kumekosekana sheria maalum ambayo inasimamia masuala ya afya na mazingira. Kutokana na kukosekana kwa sheria kumepelekea kuwepo kwa udhaifu katika kutekeleza shughuli mbali mbali za afya ya jamii na mazingira kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kuwepo kwa sheria hii kunaleta matuimaini makubwa katika utekelezaji wa kazi zinazohusiana na masuala ya afya ya mazingira na jamii kwa ufanisi. Mhe. Spika, katika kuupitia mswada huu kamati yetu imependekeza marekebisho mbali mbali yakiwemo yale yanayotokana na kiuchapaji, uandishi, kurekebishwa kwa vifungu kama kifungu 15 (1), kifungu 48 (7) na kifungu 50 (1).

Pia ilipendekezwa kuongezwa kwa baadhi ya maneno na vifungu. Vifungu vilivyoongezwa ni kama kifungu cha 7 (3), kifungu cha 15 (2), kifungu cha 58 (4) na kifungu cha 96 (2).

Vile vile kumejitokeza baadhi ya vifungu kufutwa kama kifungu 50 (2), kifungu 50 (3) na kifungu cha 72 (1).

Mhe. Spika, kamati katika kuupitia mswada huu imebaini pia kuna ugumu mkubwa katika kufahamika kwa mswada huu na jamii. Hasa ukizingatia kuwa umekusanya mambo mengi ambayo yanaigusa jamii moja kwa moja. Kama vile masuala yanayohusiana na usafi na makaazi, usumbufu, kukinga na kuzuia maradhi ya kuambukiza, kukinga na kuzuia wadudu na panya wanaoeneza maradhi katika makaazi ya jamii. Utaratibu wa maeneo ya kuzikiwa, udhibiti wa bidhaa za tumbaku na ulevi ikiwemo uvutaji wa sigara hadharani na kadhalika.

Hivyo basi kamati imeona pia ipo haja kwa wizara kuendelea kuelimisha jamii juu ya madhumuni ya mswada huu ili yale yaliomo yaweze kufahamika na kuleta ufanisi katika suala zima la utunzaji mazingira katika maeneo yaliyotuzunguka na afya kwa ujumla.

Pia kamati imeona ni jambo la busara kutoa maoni yake ya jumla jumla juu ya mswada ili kuuwekea mazingira mazuri ya kutekelezeka.

Mhe. Spika, kuhusu utaratibu wa kuweka na kuyashughulikia maeneo ya kutupa taka. Kamati inashauri serikali kuyazingatia maeneo ambayo kwa muda mrefu yamekosa sehemu maalum ya kutupa taka, kama vile maeneo mapya ya makaazi na kupelekea wakaazi wa maeneo hayo kutupa ovyo katika maeneo yasiyo rasmi.

Mhe. Spika, kamati imeona kuwa kuna haja ya kuwepo kwa juhudi za makusudi katika kuhakikisha kuwa kunatengwa maeneo ya kutupa taka na wananchi wakayafahamu maeneo hayo. Hii itasaidia katika kupunguza ama kuondosha kabisa kuenea kwa taka katika kila sehemu ya mji wetu. Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri zake zishirikiane katika kuhakikisha maeneo hayo maalum yanapatikana.

Mhe. Spika, katika kifungu kipya cha 15 (2) ambacho kamati imependekeza kiingizwe, kinahusiana na adhubu kwa atakayechanganya taka hatari na taka zisizo za hatari. Kamati imependekeza adhabu iwe kubwa kwa taasisi au kampuni kwa ajili ya kuweka kinga kwa taasisi au kampuni juu ya kutupa taka ovyo ambazo zinaweza kuleta athari kwa jamii na mazingira yetu.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa maeneo yaliyotuzunguka yanakuwa katika hali ya usafi, suala la kuwekwa vyoo katika jengo lolote la umma au sehemu yoyote ile ikiwemo hoteli, marikiti, kumbi za starehe, kumbi za mikutano, skuli, vyuo vikuu, ofisi na kadhalika ni muhimu sana.

Mhe. Spika, hivyo kamati inasisitiza uwepo wa vyoo hivyo pia izingatie watu wenye mahitaji maalum, hii itasaidia katika kuwapa upesi watu hao pamoja na kuweza kujumuika nao katika shughuli zetu mbali mbali za kijamii.

Mhe. Spika, aidha kamati imeona kuwa kuna adhabu iliyoekwa chini ya kifungu cha 27 (3) cha mswada huu inayohusiana na katazo la kutupa kitu chochote au kemikali katika mitaro ya umma ya maji machafu. Kabla ya kuanza kutumika kwake kuna haja ya kuelimisha jamii, kwani kutupa taka ovyo katika mitaro imekuwa ni tabia inayofanywa na watu wengi. Hivyo kuwaelimisha kwanza kutasaidia katika kupunguza au kuondosha kabisa tabia hii.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa kunisikiliza kwa umakini wakati nilipokuwa ninawasilisha maoni ya kamati yetu. Pia napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwamba naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Afya kwa asilimia 100 na nawaomba Wajumbe wenzangu wote wa Baraza wauchangie na hatimaye waupitishe mswada huu muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwa kuchangia mswada wa Sheria ya Hifadhi na Usimamizi wa Vihatarishi vya Afya vya Jamii na Afya ya Mazingira.

Mhe. Spika, kwanza kabisa kabla ya yote nimshukuru *Mwenyezi Mungu Subhana Wataallah* aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema na leo tunazungumzia afya, Mwenyezi Mungu atujaalie sote kwa pamoja tuwe na afya njema.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri anayehusika na mambo ya afya ambayo ni muhimu sana. Sasa tuna matumaini makubwa ya kuelekea na Zanzibar katika mambo ya afya. Mhe. Waziri ninakupongeza sana pamoja na watendaji wako wote waliokusaidia kwenye mambo haya.

Mhe. Spika, kwanza kabisa niseme sheria hii kuhusiana na hifadhi ya usimamizi wa vihatarishi vya afya ya jamii na afya ya mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo, sheria hii ni nzuri na tumuombe Mwenyezi Mungu tuisimamie vizuri.

Zanzibar tuna sheria nzuri sana tunazozitunga na wataalamu wazuri wanaotunga sheria hizi lakini tunakuwa tunafeli ambapo tu usimamizi unakuwa ni mdogo na tunaanza tu hatufiki kumalizia. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunatoa indhari sheria tunazozitunga zisimamiwe vizuri ili mambo yetu yafanikiwe, lakini kwa sheria nzuri Zanzibar hatushindwi ambapo tutasimamia vizuri basi afya hii tutaipata na tutakuwa katika mstari wa mbele.
Mhe. Spika, afya ya jamii ni muhimu kusimamiwa na vyombo husika na hata watu wengine, kwani afya ni uhai na uhai ni afya. Mhe. Spika, ukosefu wa afya na kinga mwilini utakuta wananchi wetu tumekosa afya na kinga ndani ya mwili, ndio maana hata tunashindwa kuoa mke zaidi ya mmoja kwa kuwa hatuna nguvu na kinga ndani ya mwili. (*Kicheko*).

Lakini wazazi wetu huko tunakotoka walikuwa na nguvu za kutosha kwa sababu walikuwa wanakula vyakula vya kutosha ambavyo vinajenga mwili, lakini hivi sasa vyakula vyote tunavyokula ni kemikali tupu, mtu anakosa hata kinga ya mwili. Unaweza kuletewa keki imeshakaa sijui siku ngani hata haina virutubisho ndani ya mwili tunakula tu. Lakini kama tutarejea kutoa elimu ya kutosha kuwafahamisha wananchi wetu namna ya vyakula vinavyojenga mwili basi afya itakuwa nzuri.

Mhe. Spika, katika hii ya kinga ya mwili hata watoto wetu wanakosa afya nzuri kutokana na lishe bora pamoja na kukosa maziwa ya mama. Mtoto tumekuwa na mtindo akishazaliwa baada ya siku tatu anapewa chupa ya kunyonya wakati maziwa ya mama ni muhimu sana na hii tunakosa afya njema na kinga ndani ya mwili. Tunaomba elimu itumike na kuelimisha akinamama.

Lakini vile vile akinamama wajawazito wamekuwa wanafanyakazi nzito sana wakati wanapokuwa waja wazito. Mhe. Spika, ni lazima wawe na muda wa mapummziko kujiepusha na kazi nzito wakati wanapokuwa wajawazito, halafu kujiepusha na mambo ya moto na kufanya kazi ngumu, hii tunakosa *support* na inakuwa hatari.

Vile vile Mhe. Spika, kuna mambo ya vihatarishi kama vilivyozungumzwa katika mswada huu, ni vyema sheria hii ikapewa umuhimu mkubwa ni kuangaliwa na maeneo hatarishi kwa maisha ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, kuna maeneo mengi tu, ukiangalia masoko yetu ya matunda basi ninathubutu kusema kama ni maeneo hatarishi kutokana na kutokuwa na usafi wa kuuza bidhaa zetu. tuangalie katika soko letu liliopo hapo Darajani na masoko mengineyo, hayapo katika hali nzuri hata kidogo.

Vile vile katika sehemu wanazouza vyakula kwa mama ntilie, zile sehemu ukenda ukiona katika zile meza ukiangalia chini huku basi ni maeneo hatarishi ya kutosha kwa afya ya mwanadamu lakini tunajilia tu ovyo. Ni lazima Mhe. Spika, na Waziri husika alenge sana kuangalia huko kama tumekusudia kwenda kwenye afya na kuujenga mwili uliokuwa safi.

Halafu tuangalie katika masoko yetu ya kuuza samaki na kununua samaki, hasa leo nazungumzia kwenye soko la Malindi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri apate siku atembelee ajionee kwa sababu kule samaki wanauzwa chini, sehemu hizo wakati wowote wanakojoa ovyo, halafu kuna vimelea ambavyo bahati mbaya hatuvioni na vile ni vyakula. Sasa hiyo afya tutaipata wapi.

Naomba tuwaige wenzetu wa soko la samaki *Ferry* pale, wana meza nzuri za kuuzia samaki na sehemu za matayarisho ya kuwasafirisha samaki mpaka kufika kwa mlaji, lakini sisi tunamuomba Mhe. Waziri siku moja afanye ziara aende na akisha atizame afanye marekebisho makubwa tujue haya tunayo zungumzia hapa yana

umuhimu wa kutosha, isiwe tunabwata tu hapa lakini tukifika kule hatuoni lolote linalofanyika. Sheria ni nzuri lakini utekelezaji wake ndio unakuwa ni taabu kabisa, ni matatizo.

Mhe. Spika, ni lazima tutizame. Halafu tutizame soko letu la Mwanakwerekwe kunakochinjwa kuku kule. Hebu tutizame tutembelee sana utaona hali halisi jinsi ilivyo. Mhe. Spika, pamoja na Waziri husika tutizame hayo maeneo.

Mhe. Spika, na maeneo yetu yote ya machinjoni tuyatizame kwa sababu hata ukimuona mtu kabeba nyama pale soko la Darajani kaibeba kwenye mgongo mwili wote upo wazi. Halafu vile vile kukojoa ovyo sehemu za mitaa yetu kuna athari kubwa sana, utakuta kwenye mitaa yetu tunayoishi basi kuna sehemu hazipitiki kwa uchafu, tena mikojo ya binadamu. Sasa mvua ikinyesha ile ni athari na maambukizi makubwa sana, lazima tutizame kama tunaelekea huko, kama hatukuangalia suala kama hili basi tutakuwa tumefeli kabisa.

Mhe. Spika, majaa yetu, ukiangalia jaa la Darajani hili mimi siku zote huwa ninalizungumzia, ikinyonyota tu mvua ni mashaka makubwa. Jana nilipita pale harufu kubwa sana inatoka na ndio mjini pale.

Sasa katika mji tunakosa usafi kama huo tuelekee wapi. Pale pana hoteli moja inaitwa Marikiti Café na hawa watalii ni sehemu yao wanayokwenda mara kwa mara. Lakini ukiangalia hali halisi ya pale Darajani ni mbaya katika jaa.

Mimi ningeshauri jaa lile liondolewe na liekwe sehemu nyengine kwa sababu tuna vyombo vya kutumia gari zinachukua taka zipelekwe. Jambo moja ambalo nipongeze watu wa Manispaa kuhusiana siku hizi tukiamka tunakuta sehemu ya Darajani ni safi, ninafikiri wanafanya usafi usiku, kama ni hivyo hili tunakubaliana nalo na mji ni lazima ufanyiwe usafi usiku, sio kwamba asubuhi watu wameshafika makazini ndio wanafanya usafi, usafi haufanyiki.

Mhe. Spika, upungufu wa vyoo vya jamii. Kuna upungufu wa vyoo vya jamii, mtu anaweza kutembea na akashikwa na haja ndogo au kubwa akakimbilia Msikitini, wakati mwengine Msikiti uko wazi na wakati mwengine umefungwa; wakati wa sala haujafika. Hata ndugu zetu wanaokuja kutembea wanakimbilia Msikitini kutokana na haja na hili ni tatizo.

Kama tunataka kuboresha mambo ya usafi na mazingira basi na vyoo viekwe vya jamii vinavyoweza kuwasaidia mjini na vijijini, kwa sababu mtu popote hushikwa na haja. Haitoshi Mhe. Spika, elimu tunaamini kama inatolewa lakini elimu yenyewe haijatosha. Elimu ni kitu muhimu kwa jamii kwa anayetaka kufanya jambo lolote lile itangulie elimu ili watu waelewe kuna kitu gani kinakuja. Tukilijua hilo tutafanikiwa na kama hakuna elimu hakuna lolote tutakalofanikiwa.

Vile vile kuna na huduma zinazotolewa za kubahatisha na madaktari na wakunga; wakunga wetu hawa wa kienyeji *sometimes* wanazalisha mtu hata *gloves* hawavai ni tatizo. Tunawaona ndani ya magari yetu tunapowapowapeleka hospitali, mtu anaweza kuzaa ndani ya gari lakini mkunga wenyewe hana chombo chochote cha kumsaidia. Hili ni tatizo kubwa sana na ndio maana nikasema elimu itumike kuwafahamisha jamii ili tupate kufikia huko tunakokusudia.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika watoto wachanga kuna tetesi kuna watu wakishazaliwa wanawahudumia ni tetesi tu hizi na sina uhakika na hili, lakini kuna watu wanahudumia wanawatia dawa kwenye sehemu za vitovu hivi, halafu ndio wanatoa hivyo vyandarua, sijui Mhe. Waziri atakapokuja hapa atatufahamisha analijua au halijui, lakini kuna tetesi tunazipata kama watu wanapita wanawatia dawa katika vitovu ndani ya majumba. Kwa hivyo tuelezee dawa hizi ni za uhakika au jambo lipo au ni tetesi tu.

Mhe. Spika, kwa kweli mengi yapo ya kuchangia katika mambo haya lakini mwisho ninasema kutochunguzwa kwa afya ya uokozi ni jambo hatarishi. Kama ajali zote zilizotokea hapa, kuna waokozi wanaotoka serikalini na katika vikukndi vyengine vya kijamii, na tuliokoa maiti waliokuwa katika hali nzuri na maiti waliokuwa katika hali mbaya, lakini wakati wale waliahidiwa kuchunguzwa afya zao na mpaka leo hawajachunguzwa afya zao na wakati maiti nyengine wakati mwengine zilikuwa hata kuzitazama kwa macho ni tatizo na watu wakibeba.

Kama tumekusudia kwenda huko ni lazima na hili liangaliwe. Halafu watu hawa pia waliahidiwa kupewa vitambulisho rasmi ili wajulikane lakini mpaka leo hakuna chochote kinachofanyika, ni kuwakatisha tamaa kabisa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, pamoja na Waziri husika muliangalie waokozi wa baharini na nchi kavu halikadhalika mufanye hivyo. Baada ya kusema hayo mwisho nasema naunga mkono mswada huu wa sheria asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, nikushukuru wewe asubuhi hii kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mswada huu ambao ni muhimu sana kwa jamii na hasa watu wa Zanzibar kutokana na hali ya mazingira yetu tunayotoka nayo.

Pili nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kuliona hili na kuweza kutuletea.

Mhe. Spika, mara nyingi sana mimi hupenda kueleza vitu ambavyo tayari vipo na vinaeleweka lakini hatimaye vinakuwa vinasikitisha sana kwa jamii. Mhe. Spika, wataalamu wanakaa katika meza zao na kutumia akili zao zote kabisa kwa nguvu zao zote walizopewa na Mwenyezi Mungu na kuweza kutoa kitu baada ya uchunguzi wao wakatoa kitu ambacho kitaweza kuokoa binadamu katika kuwaweka katika afya zao zenye mazingira mazuri.

Mhe. Spika, mswada huu wasi wasi wangu ni mmoja. Kwanza kutokana na mswada huu hitilafu haitotokezea kati ya *Municipality* na afya yenyewe, hapa tayari nakuwa na *tension* kwa sababu tayari tuna *department* ambayo inayohusiana na masuala hayo na sasa hivi tunataka kuchukua ama kuchukua madaraka yao watu wa *Municipality* kuipeleka afya

Mhe. Spika, kwanza Mhe. Waziri aje anieleze vizuri pamoja na wataalamu wake kuwa hakutokuwa na hitilafu au mgongano huo. Kama ni hivyo *fiyamanillah* nakubaliana nao, lakini kama kutakuwa kuna hitilafu basi itakuwa huu mswada mzima hautoweza kufanya kazi zake, kwa sababu ni yale yale ambayo yalitutokezea nyuma yatatokezea sasa hivi.

Mhe. Spika, kusema jambo sio dhambi, kwa sababu binadamu anasema jambo ambalo lile alililoliona katika ulimwengu, kwa sababu tuna ulimwengu wa kisasa sasa hivi, tuna ulimwengu wa kwenda mwenyewe kuona na tuna ulimwengu tunatumia teknolojia kuangalia katika mitandao. Mhe. Spika, nchi za wenzetu wamepiga hatua kwa masuala haya ya mazingira kama takataka ngumu na takataka majimaji, sio vibaya sisi kuanza kujikokota na ndio maana tukaanza kuletewa sheria hii, lakini tuwe waangalifu sana Mhe. Spika, na sheria hii. Sheria hii tunaileta basi twende na mazingira ya wakati na wenzetu wa huko nje.

Mhe. Spika, mimi nilikwenda Marekani juzi tu nimerudi. Lengo la kwenda Marekani Mhe. Spika, sio kwenda kumuangalia Obama au kuangalia lile jiji la Washington DC, hapana. Nilichoendea Mhe. Spika, kuangalia ni mambo ya mazingira, mambo ya ukusanyaji wa taka na kuleta umeme kwa njia ya taka, ndio maana nikagundua kuwa taka ni nzuri zinaleta neema na ni hatari vile vile taka tukiziachia.

Mhe. Spika, sitaki niende huko, lakini kidogo tu niende katika suala la shimo la kumwagilia maji, katika ukurasa wa 233. Hapa ndipo ninapoanzia mimi. Mhe. Spika, kifungu hiki mwaka ambao mlitupeleka kule China, tuliona ni jinsi gani wenzetu wanavyohifadhi maji machafu na tuliona ni jinsi gani maji yale ikawa tunayatumia sisi tena kwa kuogea na masuala mengine. Mhe. Spika, wenzetu wamepiga hatua.

Kwa hivyo, mimi ningeomba nitoe mfano wa pale Mwanakwerekwe. Sehemu ile tungeitengeneza na tukaitia saruji vizuri, basi naamini maji yale yale tungeweza kuyatumia kwa shughuli nyengine na ndio utaalamu wa sasa hivi unavyotakiwa. Lakini tunayaacha mazingira yanazidi kuchafuka pale, lipo tu lile bwawa.Unafikiri Mheshimiwa kusitokezee matatizo ya miripuko. Leo tutafanya maarifa gani ya kulifukia shimo lile, hatuna uwezo huo kwa sababu kuna njia maalum ambayo inaleta maji kutoka juu na kufikisha pale.

Kwa hivyo, mimi ningeomba sana kwamba pamoja na mswada wetu huu basi tuende na vitendea kazi sasa hivi vya kileo. Ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili alione kuwa hatari yake ipo.

Nikienda katika ukurasa wa 234 takataka hatari. Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapa takataka ni hatari kweli na hiyo ni kweli sio uongo, lakini vile vile takataka ni nzuri kama tuko *serious*. Mhe. Fatma leo nilimuuliza swali na hakujua kama leo nitalileta hapa suala hilo na akakiri kabisa akasema vyombo vyote vya habari vimechukua sauti

yake. Mhe. Spika, serikali yetu ina kitu tuseme uzito wa kuweza kuzikubali hizi kampuni zikaja kututengenezea neema, kwa sababu mule ndani tunapata faida nyingi.

Kwa mfano, hiyo Kampuni ya Secrona iliyonipeleka mimi huko Marekani. Mhe. Spika, hiyo ikija hapa kwanza. Leo mfano mdogo tu ni mara ngapi umekatika umeme ndani ya ofisi yako hapa leo hii. Hawa jamaa wa kampuni hii inapeleka umeme ndani ya Pentagon, inapeleka umeme kwenye Kambi za Majeshi na umeme wenyewe usifikirie ni maji, ni hizi takataka zako hizi tunazozisema hapa ni takataka tu. Halafu haya mambo ya kule hospitali Babu Juma ukiileta hii kampuni huna haja ya kuchoma sindano, yeye anazichukua bado kwake ni mali. Tusihangaike tena serikali kuweza kutumia *incinarator* kuweza kununua kwa pesa chungu nzima kwa kupata tatizo. Lakini la kushangaza zaidi kampuni hii ina *mobile toilet* imewekwa kwa makusudi, vile vinyesi nyinyi mnavidharau wao kwao ni mali, hatimaye tunatengenezewa haya matofali ya kujengea yakawa imara kabisa, ndio maana majengo ya wenzetu yanakuwa imara kwa sababu gani, kumbe vitu hivi tu ambavyo sisi tunavidharau, kumbe ndio vinajenga yale matofali yao yakawa imara kabisa Mhe Spika.

Kwa hivyo, mimi naomba kwamba kama kweli tunataka mswada huu uhalalike basi Kampuni hii tuikubali na tayari imeshaleta ombi lake kwa kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Lakini Mhe. Spika, mimi kuna jambo moja linanisikitisha sana na hili mimi nitalisema.

Mhe. Spika, hawa watu wa Kampuni walitoa ofa pamoja na mawaziri wetu, mimi nikawa mkali sana nikasema Waziri anakwenda kufanya nini Marekani. Kwa nini tusimpeleke huyo *engineer* mwenyewe ndiye atakayetoa maelezo yake mazuri hapa yakaeleweka. Hatimaye mawaziri hawakwenda *engineer* tumewakosa, kenda *engineer* kwa kuzaliwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk peke yake kwenda Marekani. Ni aibu Mhe. Spika, wale wametumia mapesa zaidi. Mhe. Spika, niseme ukweli *five star* na *four star*, sijakaa hoteli za chini hata siku moja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninaomba sana serikali sasa hivi tubadilike kwa kuzichukua hizi Kampuni. Leo hapa Mheshimiwa kasema kwamba Chwaka kuna mtu anayatengeneza maji ya chumvi kuyageuza na kuyafanya maji ambayo tayari yananufaisha katika hoteli, ndivyo tunavyotakiwa tuwe hivyo. Sasa na mswada huu hiyo Kampuni ya Secrona ni lazima Mheshimiwa Babu Juma utaondoa dhiki, vijana wetu watapata ajira serikalini. Lakini la kufurahisha ukiona kile kiwanda chake basi *Wallahi* hakiharibu mazingira, utasema ndio Ikulu yenyewe, utapotea njia, kiwanda chao ni kizuri kabisa.

Mhe. Spika, ukiingia kwenye kiwanda *Wallahi* huzibi pua, jinsi ambavyo *model* yake ilivyotengenezwa kiwanda kile, wanatumia takataka za mipira ya gari, wanatumia takataka za betri, wanatumia takataka za oil chafu, wanatumia karatasi, wanatumia chupa za plastiki na wanatumia kila aina unayoijua isipokuwa hizi chupa za *glass* tu. Mhe. Spika, tukiileta hiyo hapa sidhani kama kutakuwa na uchafu tena hapa.

Mhe. Spika, kampuni hii inaleta gari zake wenyewe hapa, serikali haitaki kuchukua kampuni hata moja, haitaki hata kufanya msaada na wewe. Serikali ikubali kuchukua ule umeme tu, wana uwezo wa kuweka *megawatt* 20, 30 mpaka 40 kwa hizi takataka zetu, tunangoja nini Mhe. Spika. *Wallahi* tungepewa mapema basi mswada huu usingekuja, kama tungeruhusu Kampuni hiyo, tusingempa tabu Mhe. Babu Juma pamoja na wataalamu wake, lakini bado uko kwenye *cable* tu kila siku unarandaranda wananchi wetu huku wanakufa na njaa, tunakosa kodi za mapato.

Mhe. Spika, lazima niwe mkali kutokana na haya mambo, kwa sababu wenzetu wa nchi za nje usifikiri wana uwezo wao wenyewe, makampuni yanatoka nchi nyengine za wenzao wanakwenda kufanya kazi kule ndipo wananufaika, wanapata *tax* pamoja na mambo chungu nzima. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sana hili suala tulifikirie na tuweze kuileta kampuni hiyo itusaidie ili twende na wakati kwa suala hili.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 240, katika kifungu cha 12, kinasema; mtu au taasisi itayoshughulikia uangamizaji taka bila ya uangalizi wa mtaalamu wa afya. Mhe. Spika, sijui kama tunao wataalamu hao na kama tunao basi niseme *minalfaidhina*, kwa sababu wataalamu sasa hivi hapa Zanzibar wameshatukimbia kwa sababu ya pato dogo. Nina wasi wasi tutachukua wataalamu waliokuwa sio wenye elimu ya taaluma hizi, tutabandikiza tu hiyo ndio hatari yake, tunarudi kule kule Mhe. Spika, wataalamu ni lazima tuwasaidie na tuwaweke katika mishahara ya juu, tusione tabu Mhe. Spika, ndio kukua kwa uchumi. Kwa sababu tunasema siku zote kwamba unakua uchumi, lakini unakua uchumi katika *level* za juu tu, lakini *level* za chini huku hakuna kukua kwa uchumi Mhe. Spika.

Kwa hivyo, mimi nimefikiria kwamba na hao wataalamu tunawatia katika sheria hizi lakini bado hatujawatendea haki kabisa. Mtaalamu anayeitwa mtaalamu basi anapata mshahara wa shilingi laki 300,000/=. Hiyo siisemi kwamba ndio hakika, nasema *yaumulshaka*, sitokwenda moja kwa moja, nasema *yaumulshaka*. Lakini *yaumulshaka* Mhe. Spika, unajua ni kitu kiko kinaeleaelea.

Kwa hivyo, mimi ningeomba sana Mhe. Spika, kwanza tuanzie katika mswada huu tujirekebishe na hao wataalamu ambao tuliowaweka humu kwenye mswada huu, tuwaweke kwenye *standard* ya kiwango cha mishahara yao ya uhakika, kwa sababu hiki kitu Mhe. Spika, ni kitu hatarishi, jina lake kinaitwa hatarishi.

Mhe. Spika, mimi humu sijaona zile *community* za mazingira, ambazo zimo kwenye shehia sasa hivi, ndio ambazo zinahusiana na masuala hayo, mimi sijaona humu. Vile vile sijaona katika mswada huu jinsi gani mswada huu unaelekeza kuwa hiyo kamati yenyewe itakayoundwa ita-*manage* vipi ili taka zisiweze kusambaa, sijaona mimi. Wenzetu kule Mhe. Spika, wanaweka ma-*dust bin* lakini ni ma-*dust bin* tofauti na ya Zanzibar tunayoweka, kwa sababu kule ya wenzetu ni mazuri na ni *quality*.

Mhe. Spika, kuna mambo ya mahoteli, sasa hivi uchafu umekuwa ni mkubwa sana kwenye mahoteli, tukitaka tusitake tukubaliane hivyo. Vile vile niseme elimu kwenye mahoteli bado haijafika jinsi gani ya kuweza kukusanya zile taka zao, kwa sababu ukija Kiwengwa Mhe. Spika, msitu wote umejaa takataka. Kama wale wangekuwa na taaluma nzuri basi nafikiria kuwa wangeweza kuweka pahala jaa la taka wakalijenga ambalo linakwenda na wakati, ili gari husika ikaenda kule kuchukua kwa wakati na kwenda kutupa sehemu nyengine ambayo inatakiwa zihifadhiwe.

Mhe. Spika, mimi leo kama nilivyokuambia kwamba sitotaka kuuchangia sana, lakini lengo nalirudia kusema kwamba serikali iwe wazi kabisa kuruhusu kampuni ambayo itaweza kuondosha tatizo hili sugu la takataka zilizokuwa ovyo. Mhe. Spika, pamoja na hizo takataka za ovyo, lakini pamoja na wanyama wetu tunawaruhusu sasa hivi wanakuja mjini, wanakunya na kuweka uchafu zaidi. Hili nalo tuliangalie Mhe. Spika, la wanyama wetu, kama ni lazima waje basi tuwavike nepi ili wasiweze kuziharibu barabara zetu kwa kinyesi, nalo hili tuliangalie.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba sana kwa kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili, *asaakheri* hili jambo walione kwa jicho la huruma kabisa. Zanzibar itakuwa sasa hivi takataka zote zitaondoka, Zanzibar matairi yale tuliyokuwa tunachoma barabarani sasa yatakwisha, Zanzibar sasa hivi vijana watapata ajira na serikali itapata kodi. Isitoshe tutapata umeme sio wa kubipu na bei rahisi, tofauti na wenzetu wa Bara, kuna tofauti kubwa sana Mhe. Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, wakati wowote sasa hivi semina italetwa ya kuhusu hizi takataka kama alivyosema Mhe. Babu Juma Duni, yeye kaleta mswada, lakini hiyo kampuni italeta na wao semina yao ya kuelimisha wananchi jinsi gani takataka zitaweza kukusanywa na kufikishwa katika sehemu inayohusika.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniruhusu kuchangia mswada huu ambao umenihusu na mimi ni mmoja kati ya wadau. Mswada huu Mhe. Spika, kwa kweli ni mgumu na utekelezaji wake sifikirii kama utawezekana. Kuna mambo ambayo tumeyapigia kelele kama ni Mjumbe wa Kamati hii na yamepungua kwa kiasi fulani na mengine ikabidi yateremshwe huku shimoni ili tuje tuyajadili, lakini kwa kweli mswada huu mmoja ni mzito, tusifiche, tuangalie kipengele baada ya kipengele, tuanze na kifungu nambari 2, katika ukurasa wa 232 utekelezaji wake kama utawezekana kweli.

Katika kifungu hiki Mhe. Spika, usimamizi wa afya ya jamii, nani msimamizi kwa mujibu wa sheria zetu, ukitizama sheria za Baraza la Miji Halmashauri za Manispaa. Mfano, sheria ya manispaa nambari 3/1995 kifungu cha 34 masuala ya *public art* yanasimamiwa na manispaa kadhalika na mabaraza mengine ya miji na halmashauri katika maeneo hayo. Hapa Mhe. Spika, sijui tunafanya nini, maana kuna taasisi ya Wizara ya Afya, kuna taasisi ya Dk. Mwinyihaji, tayari mwananchi anabanwa huku na akienda huku anabanwa huku atatoka wapi. Imekuwa tunajiongezea mizigo mizito huku na sheria utekelezaji wake haupo yanabaki maandishi. Huu mswada kwa kweli haufai. Baraza la Mji linataka chake na Wizara ya Afya inataka chake, hivyo utawaumiza wananchi wanyonge wa nchi hii.

Mhe. Spika, tuangalie mswada huko mbele ilikuwa mwananchi kama hana choo apigwe faini laki 500,000/=, tukalia huku na huku zikafika laki 200,000/=. Vifungu hivi huku ndani kama tunavyoviona huko mbele inaonesha kuwa havitekelezeki, kuna wasi wasi mswada huu utabaki kama ni sheria tu inasimamia na mambo mengine yaliyo humu, tuje kwenye kifungu cha 189 tukiangalie.

Mhe. Spika, sehemu hii ya tatu ya mswada huu ina mambo ambayo yameshaelezwa katika sheria kama nilivyotangulia awali. Kifungu cha 9 cha mswada huu kinaanzisha kazi zinazofanana na zile nilizosema mwanzo katika Mabaraza ya Miji ya Manispaa. Mfano Sheria ya Manispaa ya mwaka 1995 nambari 3(1) kifungu cha 37 kinaeleza mambo hayo. Kadhalika na kifungu nambari 10, kwa nini tusitekeleze mambo hayo katika sheria hizo zilizopo badala yake tunatunga sheria nyengine.

Utekelezaji wa Sheria hapa Mhe. Spika, umekuwa mgumu hautekelezaji, tunafukuzia mambo utekelezaji wake haupo. Mhe. Hamza Hassan Juma keshazungumza mara nyingi, sheria zimekuwa nyingi nyengine tuzipunguze, utekelezaji umekuwa haupo.

Mhe. Spika, kama hapo hapatoshi tuendelee katika kifungu cha 240 alichokizungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, katika kifungu cha 13; kuweka na kushughulikia maeneo ya kutupa taka. Hapo ndio huo ubovu kabisa uliokuwepo, sidhani kama utekelezaji wake utatekelezeka wa kushughulikia maeneo ya kutupa taka na kuzisafisha kunahitaji nyenzo na zana ambazo zinahitaji gharama kubwa, sijui serikali imeshajipanga vipi tukishapitisha mswada huu wa sheria tunategemea utekelezaji uanze bila kusita, tusije tukaambiwa kuna ufinyu wa bajeti huku hatuwezi kusafisha taka.

Leo kuna kifungu kinataka pesa zinunuliwe meli, ili mradi sijui kafanya nini. Hizo taka zilizokuwepo hapa katika majaa yetu zinafika siku tano au wiki hayajasafishwa, si wanawadanganya wananchi, hatujawa tayari na mswada huu bado wakati wake. Tuyaangalie hayo majaa yetu yaliopo, huu mswada wakati wake bado haujafika, hayo majaa yanafika siku tano au sita hayo magari hayajapita kuzoa taka, halafu tunataka kuja kutengeneza mswada huu.

Kama hapo hapatoshi Mhe. Spika, tuangalie tena na jirani yake katika ukurasa wa 241, kifungu cha 16 kuhusu usimamizi wa maji machafu. Hapa ndipo panaposikitisha zaidi Mhe. Spika. Nataka kujua vipi mswada huu umezingatia maji machafu yanayotoka mitaani na mahotelini yakaingia baharini bila ya kusafishwa, je tumeshakuwa na miundombinu ya kusafisha maji haya. Hatujawa tayari hiyo miundombinu iko wapi na ukizingatia kule kuna samaki, binadamu sisi tunawahitaji wale samaki kuwatumia kwa kitoweo. Kwa kifungu hiki mswada huu bado ni mzito.

Bila ya kupoteza muda tuangalie katika ukurasa wa 243 kwenye kifungu cha 20 kuhusu uhifadhi na utunzaji wa majaa. Ndio ule utekelezaji wake sijui uko wapi, baada ya kuwa na sheria hii tuifanyie kuwa ni majaa ya mitaani yaliyozagaa kama yataondolewa yatawekwa mengine, yatawekwa wapi na hiyo nafasi iko wapi ya kuweka majaa huko mjini, hivyo viwanja vyenyewe vimekuwa havitoshi sasa hivi bado tunatafuta mengine, hili ni la kuja kuwadanganya wananchi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tuje kwenye ukurasa wa 247 katika kifungu cha 31 kuhusu sababu za kutoidhinishwa ramani, kifungu cha 34 ukiukwaji wa kanuni za ujenzi. Hapa kuna sekta tatu. Baraza la Mji, Wizara ya Afya na Mipango Miji. Tayari sekta tatu zimeshagongana hapa na ukitizama sekta ya Mipango Miji ndio yenye dhamana ya kuongoza miji. Leo mwananchi keshajenga nyumba yake, kisha anaambiwa ikabomolewe je, serikali ilikuwa wapi alipokuwa akijenga, kwa kuwa ni mnyonge yule, hii ni dhamana. Hapa alikuwa atujie tusubiri, angalau ije sheria ya mipango na miji tujadili sio hapa, huu mswada bado ni mgumu tutawaonea wananchi wetu. Kila mmoja anavyoona katika kutoa maoni yake, huu ni mchango wangu mimi, na mimi nilikuwemo katika hii Kamati na mengi niliyapigia kelele ndio yakaanza kupungua, lakini ulikuwa ni mswada uliokuwa haufai hasa kuletwa Barazani.

Mhe. Spika, leo Mzanzibari anatafuta chakula chake cha mchana hajakipata atakipata cha jioni. Hatuwezi kufika Mhe. Spika, hii ni kuwadanganya wananchi wetu tu. Hapa ilikuwa ije Mipango Miji na Vijiji, hii sheria ipo sura ya 85 iangaliwe. Mimi sijalewa wala sijavuta bangi, ninavyozungumzwa yakaangaliwe haya, Sheria 85 ya Mipango Miji ipo. Sasa tunakuja tukadanganyana sheria nyingi utekelezaji wake uko wapi. Sekta tatu tumezungumza tena Mipango Miji, Wizara ya Afya na Baraza la Manispaa huyo mtu atatoka wapi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 249 kwenye kifungu cha 38 naomba tukiangalie. Kifungu hiki ni cha ajabu sana; kinasema iwapo mamlaka itaona majengo hayafai kwa makaazi ya binadamu, itaandaa mpango wa usafishaji. Yakhe, si kudanganyana kweli huko. Hayo majaa hayasafishwi zitakwenda kusafishwa huko. Tuangalie mji wake baada ya Mkurugenzi wa Manispaa kufanyakazi kwa muda mfupi angalau ndio matunda yake tunauona huu mji. Mji wenyewe unanuka, huko kunako kituo cha utalii hasa Mji Mkongwe makaro yote yanafuka maji juu, huku ni kuja kudanganyana, huu mswada bado haujafika wakati wake, mataa hayawaki huko mjini, watalii wanapigwa visu, badala ya kuleta maendeleo tunarudi nyuma, hatuwezi kufika namna hii. Hiki kifungu cha ajabu kabisa, huu mswada haujafika, mamlaka hazioni kuwa majengo mengine hayafai kuishi watu kutokana na kujengwa ovyo ovyo.

Mhe. Spika, kwa hivyo mswada huu ukipita tutegemee kuiona Zanzibar mpya maana yake, itakuwa na majengo kama Singapore au wapi kama mswada huu tutaupitisha, itakuwa hakuna nyumba za chini. Mswada huu watakuja kuonewa wanyonge waliojenga vibanda vyao waliojenga huko Tomondo, kama wale waliovunjiwa miaka ya Salmini iliyopita mpaka leo kuna watu hawajalipwa nyumba zao. Maana yake sheria hii tutegemee mji utakuwa mzuri na wa kupendeza na hatujawa tayari kwa hili kujenga majumba ya ghorofa. Leo unajenga ghorofa tatu ya nne unavunjiwa, hayo ndio maendeleo, bado mswada huu wakati wake umeshakuwa mgumu. Mtu mnyonge keshajenga kibanda chake leo unaambiwa inakuja sheria hii, itamuhusu nini sheria hii kwa wakati huu tuliokuwanao, tunawadhalilisha wananchi.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije ukurasa wa 259 kwenye kifungu cha 58(2), ametajwa Afisa wa Bandari ambaye atafanya kazi za ukaguzi hata kwenye vyombo vya baharini. Hebu tukaangalie Afisi ya Bandari kule ya Afya, tumekwenda sisi Kamati kuna kidirisha tu. Kidirisha hicho kinauzwa kadi za siku pengine mule ndani Mwenyezi Mungu atusamehe, pengine mule tiketi za meli zinauzwa pale pale. Tunataka kutengeneza haya mambo hatujawa tayari, ofisi iko wapi bandarini, tuyatengeneze haya tuliyokuwa nayo kwanza halafu tufukuzie mbele.

Hapa palikuwa na sheria Mhe. Spika, naomba kuinukuu, nataka kujua zile kazi ambazo walizopewa *port state control* kwa mujibu wa sheria za usafiri wa baharini nambari 5 ya mwaka 2006, kifungu cha 327(3) (b) zitasita kwa vile kazi hizo sasa zitafanywa na Afisa wa Afya Bandarini. Sheria tayari ipo hii, ya nini kuweka sheria nyengine.

Mhe. Spika, katika ukurasa 264 kifungu cha 80 kuingiza maradhi Zanzibar, hayo ndio hatari kabisa. Hebu tuelezwe vizuri kifungu hiki kitatekelezwa vipi, kwa sababu ipi. Suala la uingizwaji Zanzibar, kwa sababu mtu anaweza kuingia wakati wowote na akatoka wakati wowote, tofauti na vile zamani. Je, haya maradhi tutayazuia vipi. Hiki kifungu ni cha ajabu, Zanzibar haina udhibiti maalum kwa sasa, wazee wetu waasisi wa Mapinduzi waliuwekea udhibiti huo hapo zamani, yakiwemo maradhi na vipimo. Hapa atakuja kubanwa mtu bure, sijui tunafanya nini na tunaelekea wapi.

Nije ukurasa wa 267 Mhe. Spika, sehemu ya Saba, kinga na kuzuia wadudu wa maradhi. Hapa atakuja kufungwa mtu bure. Sehemu hii ni ngumu kutekelezeka kwa sababu haikuzingatia makaazi duni ya wananchi wetu hasa vijijini na maeneo mengine ya mijini, ambako nyumba zimejengwa katika mazingira hatari kiafya kama ilivyoelezwa humu. Nadhani mkazo ungeanzia kwenye sheria ya upimaji mipango ya miji na vijiji, sura ya 85 kutawekwa utaratibu mpya wa ujenzi, hayo yaliomo hapo kutekelezeka ukija sheria mpya ya adhabu chungu nzima, hii sheria ipo watakuja kubanwa watu tuondolewe.

Kifungu kinachokuja sasa hivi Mhe. Spika, ninakaribia kulia, kifungu hiki cha 112. Mhe. Juma Duni umeshafanya mengi ya kheri na umeshafanya mengi makubwa, mimi shahidi kwa hilo, ulikuwa ukilia habari ya wajawazito Mhe. Juma Duni na Mwenyezi Mungu atakujaalia kwa nia yako. Unajua ukiwa na jambo baya una nia ya kulifanya basi huandikiwi baya mpaka ufanye baya lenyewe, na ukiwa na nia ya kufanya jambo zuri basi utaandikiwa thawabu. Mimi siwezi kuwa na nia ya kutaka kumpiga Mhe. Ismail Jussa basi siandikiwi mpaka nifanye kitendo chenyewe. Hizi kazi ni nyepesi kwa Mwenyezi Mungu za kutafuta kheri, nia ya mtu unaweza kupata thawabu kwa nia nzuri tu, lakini kwa nia mbaya ni mpaka ufanye jambo baya ndio upate kuandikiwa hilo baya lenyewe au dhambi zenyewe.

Kwa hivyo, nia yako Mhe. Babu Juma ilikuwa ni nzuri. Mimi ulikuja kunisikitikia nyuma pale mkahawani, ukaniambia hakuna kitu kinacho kera Zanzibar kuliko wajawazito kuchangishwa. Mwenyezi Mungu kasikia kilio chako, leo tumshukuru *Alhamdulillah*. Leo unakuja kutuambia tutangaze ulevi humu, hii mimi siikubali hata kidogo. Leo unatangaza tangazo madhali halidhuru watu tangazo tu niwe naonywa, hili halikubaliki hata kidogo. Tena sio kwa Wajumbe tu, kila mmoja atakwenda kuulizwa, sheria hii ifutwe mara moja haikubaliki kabisa. Mhe. Spika, leo

wavuta unga wako wapi, mahoteli yaliyokuwepo Mji Mkongwe, itabaki Zanzibar itakuja kuzama hii. Kifungu hiki kinaruhusu matangazo ya ulevi hadharani mradi matangazo hayo yatakuwa na onyo.

Mhe. Spika, kifungu 112(2) kwenye ukurasa wa 272 hebu tuangalieni Waheshimiwa Wajumbe, naomba kwa heshima na taadhima tukiangalieni hiki kifungu. Naomba Waheshimiwa sijawahi kupata kuomba, lakini hili leo naomba. Kifungu hiki hakikubaliki kifutwe mara moja. Waheshimiwa Wajumbe tutakwenda kuulizwa sote humu ndani karibu asilimia 99 humu ni Waislamu, tuje tupitishe kitu na tunakijua ni kibaya, mwishowe tutakuja kujenga kiwanda cha ulevi hapa Mhe. Waziri.

Suala hili Mhe. Babu Juma mimi sina ujanja nalo. Nafikiri atakayekuja kuchangia hili atachukua jukumu kwa Mwenyezi Mungu. Likisharuhusiwa hili tutakuja kujaza mabaa humu pamoja na viwanda vya ulevi, hili lifute Mhe. Babu Juma halikubaliki hata kidogo. Sisi tuje tuwaruhusu wavuta unga na uje uruhusu ulevi huu mtu atangaze kwa kuwa una hatari, kwani ukimwi hatujui kuwa una hatari. Hesabu inaanzia moja Mhe. Babu Juma, huu mswada haufai kabisa.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri taarifa.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe *speed* anayozungumza nashindwa kukamata hoja zake, amekuwa kama vile anazungumza na mimi moja kwa moja uso kwa uso. Kwa hivyo, sijui nitakuja kuwezaje kumjibu, kwa sababu *speed* yake ni kubwa mno. Wenzangu wako wananisaidia, lakini na mimi kama Waziri nahitaji kusikia vile vile. Hatuko kwenye ugomvi, tuko kwenye kujadili.

Mhe. Spika: Taarifa imefika Mhe. Jaku Hashim Ayoub nenda taratibu, ili Mhe. Waziri akusikie vizuri, kwa ajili ya kufanya majumuisho na kufahamisha Baraza. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, karibu endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante kwa masikitiko na uchungu, huruma pamoja na imani aliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu kifungu cha 112 ukurasa wa 272 naomba Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima na taadhima tukiangalie vizuri kifungu hichi.

Kwa kweli kifungu hichi kitakuja kututesa kutoka hapa duniani mpaka akhera twendako, kwani haya maisha ya dunia ni uchafu mtupu, yaani ni maisha ya kuazima tu haya, na maisha ya kudumu yako akhera, kwa sababu dunia ni mzoga tu Mhe. Spika.

Kifungu hichi tukikipitisha sisi Wajumbe sote na kila mmoja atakwenda kuhukumiwa, na mimi wajibu wangu kutumia mdomo na mkono wangu pamoja na kulikimbia, lakini kifungu hicho naomba kifutwe Mhe. Spika, kwa sababu tumeshapiga kelele mara nyingi kutangaza timu za mipira ulevi, ndio sawa na kunywa mchuzi na nguruwe ukamuacha ndio yale kwa yale.

Kwa hivyo, kifungu hichi naomba kifutwe na atakayekuja kuchangia yeye na Mungu wake na mimi simo, "*Kullukum rai wakullukum mas-uul an raiati*" kila mmoja ni mchunga na mchunga ataulizwa juu ya alichokichunga, hichi hakifai. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hii ni hatari kwa sababu ukishaanza kuruhusu hichi kitakuja kidogo kidogo, kwani mtoto anapozaliwa haendi moja kwa moja tu Mhe. Spika, huanza na kukaa, kutambaa na baadaye kupata mguu mmoja na kuanguka na kupata mguu wa pili na hatimaye akachanganya. Sasa leo tunakuja kuruhusu kifungu hichi na mimi wala sina dhamana nacho kabisa na wala hichi hakifai tena kwa uchungu Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nadhani kilio changu kimesikiwa Mhe. Spika.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 273 sehemu ya 10 kuhusu Huduma ya Afya Bandarini. Mhe. Spika, nilirudia hichi na nilisema pale bandarini Kituo cha Afya hakipo, sasa tutapelekaje hizo huduma za afya pale na lipo dirisha tu pale.

Kwa hivyo, kwa kuwa hatujawa tayari basi itakuwa tunapoteza muda wetu kwa kufikiri na kuchanganya, lakini twende huko bandarini nikaoneshwe hicho kituo cha afya ndio hichi na kuna nini, kwa kweli sheria zimekuwa nyingi Mhe. Spika, lakini utekelezaji wake haupo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani mswada huu ni vyema ukarejeshwa kwanza bado hatujawa tayari na sheria hizi, taasisi tatu zinagongana hapa Mhe. Spika kwa serikali hii moja huyo mwananchi atatoka kwa njia gani, kwa sababu wananchi wetu wanchi hii ni wanyonge tena wanaumia. Kwa kweli hakuna mtu asiyetaka kuwa na choo lakini inambidi, kwa sababu mtu anataka kuishi katika maisha haya na leo mtu hana choo anataka kupigwa faini ya shilingi 500,000/= kwani amekusudia asiwe na choo Mhe. Spika.

Kwa mfano, leo anakwenda kutafuta *panadol* katika Hospitali ya Mnazimmoja. Sasa katika hali kama hii hatuwezi kwenda na tutawanyanyasa wananchi wetu na sisi tumechukua jukumu na tumekula kiapo baadaye tusijekuoneana haya kwa kutokuja kusema ukweli huu, kwa sababu huu ndio ukweli ulivyo usiofichika, na wala hautaki hata tochi kumurika huu. Kwa hivyo, hii ndio hali tunayokwenda nayo tuukubali muongozo wa nchi yetu.

Vile vile kazi zilizoelezwa hapa ni nyingi na tatizo zaidi utekelezaji wake unahitaji nyenzo na zana za kisasa, sijui kama serikali imeshajipanga kwa hili katika kifungu cha 113(2), tunapitisha vifaa vyenyewe bado hatujawa tayari kuwa na vifaa kama hivi.

Mhe. Spika, tumepitisha sheria ya *ZBS* utendaji wake mpaka sasa tunasubiri muda gani, ukitaka kupima maji upeleke Bara, ukapime na huku kuna vifaa mbali mbali vya umeme vinavyokuja vinaripuka kutokana na *fake*, yaani vifaa vibovu na wala havina viwango. *(Makofi)*

Kwa kweli sheria zimekuwa nyingi nadhani tuingilie kati na tuseme basi kwanza tulichokuwa nacho tukitekeleze hichi na leo nyumba zinaripuka tu kwa vifaa vya Kichina. Kwa maana hiyo, sheria zimeshakuwa nyingi na utekelezaji wake haupo na zinabaki kama maandishi tu. *(Makofi)*

Maudhui ya mswada huu Mhe. Spika ni mabaya na tuangalie kwa makini mambo yafuatayo. Kwa mfano, kuna vifungu ambavyo nimevitaja na vinaendelea kubaki katika sheria nyengine badala ya kuweka humu. Vile vile kuna vifungu nimevitaja uwezekano wa kutekelezwa ni mgumu na vinahitaji gharama, nyenzo, mabadiliko ya sera ya uhamiaji wa Zanzibar.

Vifungu vinavyoruhusu matangazo ya ulevi kwa hali yoyote, kwa heshima zote, kwa huruma zote pamoja na imani zetu zote basi kifungu hichi kifutwe na Waheshimiwa Wajumbe nadhani wataniunga mkono kwa hilo.

Kwa hayo, machache Mhe. Spika, sitaunga hoja hii mkono mpaka nipate maelezo ya kuridhisha kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mtukufu *Azza Wajalla*, kwa kutujaalia kukutana tena kwa mara nyengine katika Mkutano huu wa Baraza la Wawakilishi, tukiwa bado tukiwa hai na wazima wa afya.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira 2012.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji kwa kuja na mswada huu kwa sababu moja tu Mhe. Spika, kwa sababu naamini dhamira yake ni njema. Kwa kweli dhamira ya kutuelekeza katika *Public Health* bila ya shaka hiyo ni dhamira njema. *(Makofi)*

Lakini wakati napongeza dhamira nikubaliane kabisa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba mswada huu bado hatujawa tayari Mhe. Spika. Kwa kweli nikisema hivyo nasema kwa masikitiko makubwa sana kwamba leo nchi ambayo ilipiga hatua za maendeleo katika nyanja nyingi nchi ya Zanzibar.

Ndio maana ukienda katika vile vitabu vya sheria vya asili, mambo mengi haya leo dunia inaona ni mambo makubwa ya maendeleo Zanzibar tayari ilishakuwa nayo na ilikuwa na sheria zake kamili, lakini kwa bahati mbaya mambo kama haya sisi badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma.

Kwa hivyo, tatizo langu lipo hapa katika mswada huu kwenye madhumuni na sababu amesema Mhe. Waziri katika maelezo yake, kwamba ilikuwepo Sheria ya Afya ya Jamii, yaani *Public Health Decree cap* 73, ambayo ilifutwa mwaka 1976, ndio kuonesha kwamba mambo hayo yalikuwepo, lakini yapo na mengi mengine katika sheria zetu au yalikuwepo. Lakini tujiulize kwa viwango tunavyokwenda navyo sasa ambavyo vinarudi nyuma badala ya kusonga mbele tunaweza kweli kutekeleza haya yaliyomo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi binafsi nina wasi wasi kwa maana hiyo utaniona katika mchango wangu leo ile kawaida ya kwenda kifungu kwa kifungu nitaiacha, isipokuwa kuna vifungu vichache ndivyo nitakavyovitolea maoni, lakini nataka nieleze kwa ujumla suala hili.

Mhe. Spika, wenzangu waliochangia mwanzo wameeleza hali ya nchi yetu ilivyo, kwa kweli kiasi kikubwa cha hali ya kukosekana kwa viwango vya afya ya jamii ni matokeo ya kufeli kuwajibika kwa serikali yetu na taasisi zake. Kwa hivyo, hata haya tunayowapelekea wananchi kwamba leo wananchi wa Zanzibar ambao wakisifika kwa ustaarabu na viwango hivyo vya afya ya jamii, leo wamerudi nyuma kwa sababu serikali yenyewe haikuwa makini siku zote katika kusimamia haya Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pameelezwa hapa tunahimizana huku kwamba tukusanye taka zetu halafu tukazitupe jaani, hebu tutizame hayo majaa katika mitaa yetu. Mhe. Spika mimi naishi katika Nyumba za Michenzani, unakuta na nimeshasema si mara moja wala mbili tangi la kuhifadhia taka limeshajaa na linafurika na kutapika, yaani uchafu kila pahala Mhe. Spika tena ni aibu na wala wahusika hatuwaoni kuja kuzoa taka, isipokuwa ni hodari wa kukusanya mapato tu hawa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wamezungumza watu hapa na leo tumeruhusu biashara za vyakula ovyo holela kila pahala na ukienda kutizama hakuna chochote kinachosimamiwa na wahusika na sheria nyengine pamoja na kanuni zake zipo, isipokuwa kinachowagusa wao ni kutembeza risiti na kukusanya mapato basi ndio *interest* yao. *(Makofi)*

Kwa mfano, tuangalie michirizi pamoja na mitaro ya maji machafu, yaani kila pahala pametumbuka na nchi inanuka ni aibu na hii ni kazi ya taasisi ya serikali Mhe. Spika. Sasa leo Mhe. Spika tuangalie hata usafi wa hayo majengo tunayoambiwa ya *public* haya yetu sisi, nimewahi kusema mara nyingi na nitaendelea kusema hapa. *(Makofi)*
Mhe. Spika, unakwenda pahala kama hospitali ambapo pangetegemewa kwamba pangekuwa ndio kioo katika usafi wa mazingira, basi kile kibao kilichoandikwa weka mazingira katika hali ya usafi chenyewe kinanuka kwa uchafu, mavumbi na mabuibui, yaani kinawasuta wale waliohusika pale na halafu unawaletea wananchi sheria kama hii Mhe. Spika. *(Makofi)*

Vile vile vyoo katika mitaa yetu, yaani *public toilets* Mhe. Spika vyengine vimegeuzwa biashara za watu kuingiza mapato mifukoni, maeneo mengine mengi miji yetu imetanuka, leo vyoo vimebakia vya asili alivyoacha mkoloni. Lakini tumejenga vyoo vingapi kwa ajili ya kusaidia jamii katika miji yote ambayo tumeitanua hivi sasa, kwa sababu kila pahala kuna mji katika Zanzibar leo na matokeo yake watu wanajisaidia ovyo mitaani.

Barabara zetu Mhe. Spika kufyagiliwa hazifyagiliwi tumekuwa wakati fulani sisi na wala sizungumzi enzi zenu nyinyi Mhe. Spika, isipokuwa enzi zetu sisi wakati tulipokuwa wadogo nakumbuka unakwenda skuli asubuhi unakumbana na watu wanamaliza kusafisha barabara, yaani wameshafyagia na wanakusanya taka. Lakini leo imekuwa *fashion show* mimi naita *fashion show* Mhe. Spika, pale Darajani usiku ukipita watu wameshughulika na wakeshakuondoka hao wasafishaji pita uone hizo taka zilizozolewa ni taka zipi na mji uko mchafu vile vile.

Kwa kweli tunakusanya katika maduka na nyumba shilingi 6,000/=, 9,000/= mpaka 16,000/= yaani kila siku zinaongezwa tu na *interest* yetu ni kukusanya mapato wakubwa wajaze mifukoni mwao na wala sio kwa maslahi ya nchi yetu na hata kwa wananchi wake tusidanganyane.

Mhe. Spika, mabwawa ya maji yaliyozagaa humu kama vile ukipita pale Mwanakwerekwe pamoja na maeneo mengine mengi yanatapika na kutoa harufu hasa kipindi cha mvua, matope yakeshakujazana mpaka yanavunda wamezungumza wenzangu.

Vile vile wanyama ni aibu kwa nchi hii kwamba kiongozi mkuu wa nchi ametoa na kila siku *ZBC* wanamkejeli Rais, mimi nasema wanamkejeli Mhe. Spika, maana yake lile tangazo kumtoa Mhe. Rais anahimiza kununuliwa ng'ombe na leo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Baraza la Manispaa wote wakashindwa kutekeleza agizo dogo tu la kuzuia

wanyama kuingia mjini Mhe. Spika, hivi tunatekeleza lipi jengine hata tuje kusimamia sheria hii Mhe. Spika, isipokuwa tunadanganya hapa.

Mhe. Spika, leo mizoga ya wanyama wanaokufa imezagaa kila pahala, serikali imekuja na utaratibu kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza kuangamiza kunguru, yaani kila unapopita mizoga ya kunguru, kwa sababu wameshategа lakini mwenye dhamana ya kusafisha baada ya pale nani katika miji yetu na wala hakuna kitu Mhe. Spika.

Sasa leo hiyo Ofisi ya Manispaa ambayo mpaka hivi sasa kabla ya kuja sheria hii ndio wenye dhamana ya *public health* katika maeneo yetu, basi pale kwenye ofisi yao Darajani mbele ya uso wao pananuka kwa kila aina ya uchafu Mhe. Spika. Maana yake si kazi yetu masuala ya usafi ni mambo ya madiwani na wala sio ya Mwakilishi, lakini tunabeba jukumu hili kwa sababu wengine tunaona hawawajibiki. Kwa mfano, unakwenda kupanda ngazi na kushuka kwa suala dogo tu Mhe. Spika mpaka unachoka halitekelezwi.

Masoko yetu Mhe. Spika, mara ngapi tumesema ndani ya chombo hichi, hivi tunataka kudanganyana kwamba yalikuwa hayatekelezwi kwa sababu hakuna Sheria ya *Public Health* na wala tusidanganyane Mhe. Spika, isipokuwa hakuna dhamira.

Masoko yananuka hakuna mpangilio, vyakula vinatupwa ovyo vinavyouzwa na amesema Mhe. Hassan Hamad Omar, maana mimi sijui mara ngapi nimeshasema hapa kwamba leo kitoweo namna samaki anavyoburuzwa katika sehemu ambazo watu wanatema makohoo na kila kitu kwenye marikiti zetu.

Vile vile nyama ile mtu anajitwika hujui mwili wake uko katika hali gani na wala hana chochote katika kuweka *public hygiene*, yote hayo kwa sababu tulikuwa hatuna sheria hii Mhe. Spika na wala tusidanganyane.

Mhe. Spika, hata vyombo vyetu hivi na leo tunataka kuleta sheria ya kuhakikisha kwamba tuna viwango katika vyombo vya usafiri, zinatushinda sheria za kusimamia udereva wa daladala ambao ndio *public transport*. Kwa Kweli zinaendeshwa na ahakikishwe mtu atakayekuwa anaweza kujua ana dhima ya abiria aliowapakia, kwa sababu ndio dhima ya *public transport* duniani tumeshindwa na tumeshapiga kelele mpaka tumeshachoka katika Baraza hili Mhe. Spika na wala sio Baraza lilipita ni hili lililoanza Oktoba, 2010.

Mhe. Spika nimetoa mifano hii kuonesha kwamba bado hatujawa tayari. Kwa hivyo, naipongeza dhamira njema ya Mhe. Waziri wa Afya, lakini namuonea huruma kwa sababu sheria hii haitekelezeki Mhe. Spika, kama anavyoendelea kusema Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba sisi ni hodari mno wa kurudufisha masheria, na siku moja nilisema hapa kwamba mbali na suala la mfumko wa bei karibu tutakuwa na mfumko wa sheria. Lakini kiasi gani hizo sheria, hebu kwanza tutekeleze zilizopo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub ametaja hapa na ninamsifu amefanya *research* nzuri pamoja na *references* ametaja sheria ambazo zipo na wala hatuzitekelezi, hivi kwa kuwa na sheria moja ndio tutatekeleza mambo hayo. *(Makofi)*
Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi nina wasi wasi mkubwa kwamba tunataka kudanganyana na kufurahisha watu tu hapa kwamba tunajali vitu hivi basi. Mhe. Spika, mbali ya mengine yaliyozungumzwa hapa kama vile kuna mahitaji ya vifaa, wataalamu katika masuala haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine kwamba sheria hii haitatekelezeka kwa sababu nchi yetu imetopea na inanuka rushwa. Kwa kweli moja ya tatizo letu kubwa sheria hazitekelezwi Mhe. Spika, kwa sababu tume-*institutionalize corruption* katika nchi yetu. Kwa mfano, tumepitisha Sheria hapa ya Kupambanana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, kwani tatizo letu Mhe. Spika ni sheria, isipokuwa tunarudi pale pale utekelezaji.

Mhe. Spika, rushwa na sisi mara nyingi tukizungumza rushwa huwa wanaangaliwa labda viongozi wa juu pamoja na wanasiasa, lakini rushwa imekuwa *institutionalized* katika nchi yetu kiasi ambacho hata *traffic* hasimamishi sheria barabarani kwa sababu ya rushwa, hata huyo *Inspector* ambaye unayetaka aende kusimamia *Public Health* hatasimamia kwa sababu ya rushwa akeshapewa chake mfukoni basi ataachia na hayo ndiyo yaliyokuweko hivi sasa Mhe. Spika.

Kuna sheria ngapi na hiyo mipango miji inayozungumzwa katika sheria hii ambazo tayari kuna sheria zake hazitekelezwi kwa sababu anayesimamia sheria ameshapewa chake anaruhusu uendelee kujenga unavyotaka

mwenyewe. Mhe. Spika, nitatoa mifano mpaka nitachoka, lakini kwa kifupi bado hatujawa tayari na wala tusidanganyane Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nchi yetu imekuwa kama vile ni nchi yetu *law of the jungle* ambayo ndani yake kuna *survival of the fittest*, yaani mwenye nguvu mpishe basi.

Sasa mimi nakubaliana na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba sheria hii tunakwenda kuwaonea watu bure, kwa sababu utekelezaji wake utakuwa pamoja tu Mhe. Spika, kule kwenye faini na wala hazitaingia serikalini faini hizi, itatekelezwa kwa ajili ya watu kwenda kuwatunishia mifuko yao basi, lakini sifikiri kama tutaona *improvement*.

Kutokana na hali hii mimi Mhe. Spika na-*challenge*, kama ingekuwa unaniruhusu ningechukua mas-hafu na kuweka mkono wangu juu na kusema *Wallahi* baada ya miaka mitatu tuje kutizama hakuna mabadiliko yoyote katika sheria hii ambayo itakayopitishwa kwa kutungwa sheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na wamesema wenzangu hapa kwamba sheria hii pia itatuletea *confusion*, kwa sababu baadhi ya mambo ambayo yametajwa hapa tayari yamo katika sheria nyengine na wamepewa wengine wenye dhamana hiyo.

Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi mkubwa sana na sheria hii. Kwa mfano, leo amesema Mhe. Jaku Hashim Ayoub tunazungumza humu kuwaongezea dhamana Afisa wa Afya wa Bandari, kusimamia meli kuhakikisha abiria wanaopakiwa ni sawa kwa mujibu wa viwango tukaepusha ajali imetushinda hapa na tunapoteza roho za watu kila siku kama kuku, watu wanakufa katika nchi hii tutakuja kusimamia *public health* Mhe. Spika hapa. *(Makofi)*

Tumetoa ripoti hapa baada ya ripoti ya mwanzo ya ajali hapa tukatoa ripoti ambayo imejaa mapendekezo tangu Mv. *Fatih* imekuja *Mv. Spice Islander* imekuja nyengine na zitakuja na nyengine Mhe. Spika, kwa sababu tuna tatizo kubwa la kutotekeleza sheria zetu kwa kuwa tume-*institutionalize corruption* katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo siku tulipopitisha Mswada wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hapa niliukataa kwa *principles*, na baadaye nikauchangia kwa sababu najua kwamba kwa mambo yetu yalivyo utapita, pamoja na kwamba mimi nasema hatujawa tayari.

Lakini najua kwa maumbile yetu hapa utapitishwa kuna baadhi ya vifungu nataka kuvizungumzia *specifically* kama kweli tuko *serious* Mhe. Spika, yaani ile dhamira aliyokuwa nayo Mhe. Waziri wa Afya kama kweli inataka kutekelezwa.

Kwanza Mhe. Spika, katika tafsiri nimepata wasi wasi na nitaunganisha kabisa yale aliyozungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba Mhe. Spika tuna tatizo katika nchi yetu ambalo ninaloliona mimi na wataalamu wetu wanaotunga sheria zetu au wanaoandaa miswada kwenda kutizama sheria za nchi nyengine waka-*copy* and *paste*, labda na kubandika na vitu vyengine ambavyo vinalingana na mazingira yetu.

Matokeo yake tunaweka vitu ambavyo tayari kimaadili na *conversion* tu sheria na kanuni zetu katika maumbile kwenye nchi yetu hazikubaliki. Mhe. Spika, kwa maadili ya nchi hii kwa kiasi kikubwa yanayoendana na maadili ya Kiislamu; dini ya watu ambao ndio wengi Zanzibar.

Mimi nimepata *shock* kwamba katika tafsiri ya sheria ya vifungu au maneno mbali mbali yaliyotumika kifungu cha tatu cha mswada huu Mhe. Spika, tafsiri ya neno biashara inayoudhi kwenye ukurasa wa 235 Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 235 unaeleza hivi:-

> “biashara inayoudhi inajumuisha biashara za kuchoma na wameandika mkaa na mimi sijui mkaa ninavyojua ni makaa ndio Kiswahili, kuchoma makaa, kuchoma chokaa, ukamuaji mafuta, upikaji sabuni na uvunjaji mbata, shughuli za usafishaji sullage na huko mbele umerekebishwa na tumeambiwa ni usafishaji vyoo na makaro, viungo vya wanadamu, ukahaba na umalaya kwa watoto na biashara yoyote, kazi au utengenezaji ambao umetangazwa na Waziri kuwa amri ya kisheria kuwa ni biashara inayoudhi”.

Mhe. Spika, nchi hii tumeshafika kuhalalisha kwamba ukahaba na umalaya ni biashara ambayo mpaka tuitambue katika sheria zetu. Kwa kweli napata wasi wasi Mhe. Spika, kwa sababu kwa kuingiza katika tafsiri hapa maana yake tunatambua kumbe umalaya na ukahaba inaudhi tu lakini ni biashara, sijui Mhe. Spika. Kwa hivyo, nasema tuna tatizo na mara nyengine kuchukua vitu ambavyo sio vyetu.

Lakini Mhe. Spika, kuna moja ambalo napenda kuligusia katika tafsiri hii kwamba tumeingiza ukahaba na umalaya, lakini kuna biashara nyengine ambayo mimi naiona inaudhi na wala hatujaiingiza hapa, hii biashara ya siku hizi ya watu kupiga miziki katika kumbi za wazi. *(Makofi)*

Public health Mhe. Spika, *noise pollution* uharibifu wa mazingira kutokana na ghasia pamoja na makelele yanayokera Mhe. Spika, haya yanaleta athari hata kwa afya zetu, kwa sababu ukimsikia mtu siku saba mfululizo anasikia midundo tu katika masikio yake Mhe. Spika hapati utulivu wa usingizi na hiyo ni *problem* katika *public health* na wala hatukuitaja hapa, sijui kwa sababu kuna wakubwa wana manufaa nayo au vipi.

Lakini hii Mhe. Spika inaudhi kuna watu tumesema mara nyingi hapa mwaka huu tulipokuwa tukipitisha bajeti nilimwambia Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwamba kwa Mji Mkongwe watu wamekuwa taabani, yaani kuanzia Bwawani mpaka Ngome Kongwe kumekuwa na shughuli za kupiga miziki katika sehemu za wazi. Kwa hivyo, dunia nzima inajulikana kama unataka kufanya starehe basi piga muziki, lakini kunakuwa na *sound proof* katika sehemu ambazo zinapigwa muziki ule na wala hausumbui watu na sikuliona hapa kilitajwa hilo Mhe. Spika.

Vile vile katika tafsiri ya neno mahala naomba kutoa indhari tu ambayo iko katika ukurasa wa 236 katika kutambua mahala imejumuisha ardhi, maakazi na *point* yangu ni mwisho kabisa kule mstari wa mbili kabla ya mwisho wa kifungu hichi na imesema "… au chombo chenginecho kilichomo ndani ya maji katika Zanzibar au katika fukwe zake".

Mimi nadhani kwa tafsiri nzuri ingesemwa kilichomo ndani ya eneo la bahari ya Zanzibar kuliko ndani ya maji katika Zanzibar na hiyo ndiyo lugha ambayo pia imo Kikatiba.

Nikiendelea na mchango wangu katika tafsiri ambapo tafsiri ya mwisho kabisa ni bidhaa ya tumbaku na bidhaa hii imeishia kutambua hii tumbaku yenyewe tu.

Kwa hivyo, naomba serikali kwa jumla ikiwa Waziri mwenyewe mwenye mswada au wengine watusaidie, hivi hatukuona kama maeneo mengine. Kwa mfano, bangi, mirungi, siku hizi kuna vitu vinaitwa kubari hizi haziingii katika athari? Kwa sababu sikuziona kutajwa popote katika sheria hii, hivi haziathiri afya ya jamii Mhe. Spika naomba maelezo katika hili.

Nikimalizia sehemu ya kwanza ambayo ilikuwa ni kubwa yenye kuzungumzia tafsiri, basi kwa uchache nije katika sehemu ya pili. Mhe. Spika, sehemu ya pili ni utawala na aliyepewa dhamana ya sheria hii ni Mkurugenzi na ukienda kwenye tafsiri ndio utajua hapa ni Mkurugenzi Mkuu wa Afya.

Mhe. Spika, Mkurugenzi Mkuu wa Afya hizi kazi zake ambazo anazo hivi sasa kila siku tunagipa kelele kwamba hazifanyiki, sasa leo unakwenda kumuongezea dhima na sheria kama nilivyosema hapa kwamba mazonge yake huko nje ni makubwa kweli.

Kwa hivyo, mimi nasema kama kweli serikali tunataka tuiamini iko *serious* katika hili, basi ningetegemea labda ingeanzishwa hasa nafasi ya idara na ikawa na Mkurugenzi Mkuu wake wa *Public Health* akawa anasimamia hizi.

Lakini hiyo maana yake nini, na vile vifungu vyengine vyote vilivyoko katika sheria mbali mbali nyengine vilivyokuwa vimetoa mamlaka kwa watu wengine viondoshwe na vihamie kwa idara moja ambayo itakuwa na madhumuni. Kwa kweli sheria hii kama itatekelezwa basi itabadilisha kabisa kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba nchi yetu itakuwa kuliko Singapore kama itatekelezwa.
Sasa kama kweli kuna dhamira, basi angalau tuone kwamba kunawekwa idara maalum ambayo itakuwa inashughulikia badala ya kwenda kumtwisha majumu haya Mkurugenzi Mkuu wa Afya, na ninajua tutakuja kuambiwa hapa kwamba awe na wasaidizi wake ataekewa wakaguzi, lakini yule msimamizi mwenyewe Mhe. Spika.

Sambamba na hilo naomba kuiuliza serikali kwamba ukitizama katika sheria kwenye vifungu mbali mbali wananchi kwa maana ya walengwa wa sheria hii kila pahala wameekewa adhabu kwa kutotekeleza sheria hasa katika kifungu cha 123.

Huyu Mkurugenzi yeye pamoja na wasaidizi na maafisa wake, ikiwa wao hawatekelezi hawa hawaadhibiwi, maana sheria hii itakuwa haina maana kama inataka kwenda kumkomoa mwananchi tu, ili kuwapa uhalali watu wakawakomoe matozo pamoja na faini mbali mbali. Lakini yule muhusika katika serikali na kama nilivyosema kwamba tatizo la nchi yetu ni utekelezaji wa sheria, sasa huyu mwenye dhima ya utekelezaji wa sheria hii, yaani msimamizi yeye hatumpigi faini huyu. Mhe. Spika, naomba maelezo katika hili.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu na nimesema leo ninachangia kwa jumla. Sehemu hii inazungumzia kuhusu usafi na makaazi. Lakini hapa Mhe. Spika, kuna kitu nimekiona kwamba sheria hii imetaja kuna mamlaka hapa lazima zipatikane na kwenye vifungu mbali mbali vinazungumzia kufanyakazi kwa pamoja.

Kwa hivyo, katika sheria hii hata ukija kusoma kwenye sababu na maelezo imeelezwa kwamba sehemu hii ya tatu inahusu uratibu, kwa sababu inasema hii katika vifungu kuanzia vifungu vya 30 Mhe. Spika kuna Mamlaka ya Upangaji imeeleza maelezo yake, na halafu kifungu cha 39 kinazungumzia *coordination* Waziri kwa kushauriana na mawaziri wengine wanaohusu na mifugo, uvuvi, kilimo, viwanda, mazingira, ardhi, makaazi, maji, nishati na serikali za mitaa atatunga kanuni, *point* yangu nini Mhe. Spika.

Kwa kweli moja katika udhaifu mkubwa kufeli kwa serikali hii ni tatizo kubwa la uratibu wa shughuli za serikali. Mimi hili nalibebesha lawama Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa sababu kikatiba ndio yenye jukumu la kuratibu shughuli zote za serikali. Mambo mengi tumeyapitisha sheria hapa, yanakwama kwa sababu ya tatizo hili la kukosekana uratibu. Nina wasi wasi kwamba sehemu hii nzima iliyowekewa ili ifanye kazi, roho yake ni uratibu wa shughuli za wizara mbali mbali, lakini pia na hii mamlaka inayoitwa na upangaji. Mimi naamini hapa ndio tutakapopata *total fail,* kwa sababu sioni huo uratib katika Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais. Naeleza uhalisia wa mambo ninavyouona.
Mhe. Spika, nimeeleza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nashukuru kaligusa. Ukenda Sehemu ya Sita hii imezungumzia suala zima la kuzuia maradhi kutoka nje, “Maradhi ya Kutolewa Taarifa Kimataifa na Chanjo”. Hili Mhe. Spika, linanipa mashaka kwa sababu moja. Nchi yetu ina mambo ambayo inayasimamia yenyewe. Lakini hatuna udhibiti wa watu wanaoingia hapa Zanzibar. Najiuliza mtu akishakuingia katika mipaka ya Jamuhuri ya Muungano kwa tafsiri zetu zilivyo, tayari keshaingia Zanzibar huyo. Sasa tunadhibiti vipi kimataifa kwa wanaotoka huko Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi hili nitalielewa na nitaliona mantiki yake, ikiwa tu serikali itanambia inarejesha utaratibu wa watu kuingia Zanzibar kwa kutambulika kupitia vitambulisho maalum. Bahati nzuri Zanzibar hivi sasa inayo vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Ningetegemea kungewekwa utaratibu wa kuwatambua watu wanaoingia. Lakini sasa hivi Zanzibar watu wanaingia kiholela tu.

Leo katika miji yetu wale watu ambao kwao kule wamefukuzwa omba omba, wakapigiwa marufuku warudi katika Mikoa yao, leo wote wamehamia Zanzibar na kama Mawaziri wa serikali hawajui wapite Darajani pale wakawaone. Kuna wimbi kubwa la wale wenzetu tunaowaita wagogo kule, waombaji ambao wanaathiri mpaka maadili yetu, kwa sababu hatujazoea kuomba kwa staili ile, basi wanaathiri hapa leo. Sasa uingiaji wa watu Zanzibar ni holela, tutawezaje kutekeleza Sehemu ya Sita hii tunayoizungumzia kudhibiti maradhi na kutolewa taarifa kimataifa na chanjo. Mimi siamini Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nataka kulizungumzia hili alilolizungumzia Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kifungu cha 112 kule mwanzo katika tafsiri nilizungumzia kwamba kwa mlango wa nyuma kwamba sheria hii sasa inahalalisha biashara ya ukahaba. Kifungu cha 112 kinakwenda kinyume na sera ya serikali yetu. Sera ya serikali yetu sote tumekataa matangazo ya pombe na ndio maana hata ligi zetu timeathirika, kwa sababu tumesema haturuhusu kudhaminiwa na wanaotangaza biashara ya pombe. Hata alivyokuja Malta hapa kambiwa atangaze kile kinywaji ambacho hakina kilevi ndani yake basi.

Lakini Mhe. Spika, ndio nikasema patizo la ku – *copy and paste* sheria za watu.

Kifungu cha 112 "(1) Hakuna mtu atakayeajiri mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 katika matangazo ya biashara ya ulevi".

Maana aliyezidi miaka 18 maana yake ni ruhusa kutangaza ulevi, ndio maana yake.

"(2) Matangazo yote ya biashara ya ulevi yatabeba maonyo juu ya athari za pombe kwa afya, familia na uendeshaji wa vyombo vya usafiri"

Maana yake Mhe. Spika, kumbe tunaruhusu lakini uweke onyo tu kama vile sigara. Hebu serikali itwambie inasimamia nini? Hairuhusu matangazo ya pombe au inaruhusu lakini badala yake ibebe na onyo? Mbona serikali yetu haifahamiki inasimamia nini Mhe. Spika. Nilikuwa naomba hili tupatiwe ufafanuzi. Mimi nasema naungana na Mhe. Jaku, kifungu hiki hata nibakie peke yangu katika kupitisha vifungu, nitakikwamisha, siwezi kukubali kabisa.

Mhe. Spika, zaidi na lile linalohusu matangazo ya sigara. Imewekwa faini yake tena imewekwa kwamba isipindukie au isizidi hapana, imewekwa *fixed* hasa kwamba atalipa faini ya shilingi laki mbili, atalipa faini ya shilingi laki tatu. Mhe. Spika, mtu mpaka akifika kufanya biashara ya ulevi mpaka akaweka matangazo, faida yake ni kubwa, hizi shilingi laki mbili ni pesa ndogo sana Mhe. Spika.

Kwa hivyo najiuliza tumeamua sasa kuacha ile misingi ya maadili ya watu wa nchi hii. Naungana na wale wote ambao wamesema kwamba sheria hii ina matatizo yake na kifungu hiki sikikubali. Lakini kama nilivyosema kwa jumla namalizia kwa kusema, narejea pale pale, naipongeza dhamira lakini siamini kama tupo tayari kutekeleza sheria hii wala siamini kama itatekelezwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, sitounga mkono hoja hii angalau kwa hatua ya mwanzo vile vifungu ambavyo vimekuja kuhalalisha biashara ya ukahaba na ulevi vitakapo ondolewa katika sheria hii.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kurudi tena katika kipindi hichi katika kutekeleza majukumu yetu katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, na mimi nimeinuka kwa kuchangia Mswada huu kwa maneno kidogo tu kwea sababu maalum ambayo katika sheria hii kuna mambo ambayo mimi binafsi yamenigusa.

Mhe. Spika, Mswada huu nadhani watanguliaji waliochangia wameeleza kwa upana kuhusu juu ya dhamira ya Mswada huu, lakini bado tuna wasi wasi na kutekelezeka kwake Mswada huu. Sitaki kurejea waliyoyasema wenzangu hali inaonekana ya mazingira na uchafu. Kwa kweli Mswada huu unaonekana kwa njia moja au nyengine labda tunaweza kusema sheria hii itawagusa wanyonge tu. Hali inayoonekana sasa hivi katika hizo taka za majumbani, ukushanyaji wa taka za majumbani ukichukulia hasa katika sehemu yetu ya Mwanakwerekwe, mataka yaliyokuwepo majumbani yananuka.

Ambapo kuna Halmashauri zinazokuja kuchukua taka majumbani, mimi mwenyewe nina risiti chungumzima, lakini wanakaa mwezi mzima hawaji kuchukua taka, uchafu huu unatupwa wapi. Mpaka mimi mwenyewe nikawambia basi msije kuchukua kwa sababu ukifika mwisho wa mwezi wanyonge wanatoleshwa pesa mataka yale inabidi yatupwe tu. kwa hivyo kila pahala kweli umeenea uchafu na unanuka.

Kwa hivyo hizi sheria tunavyozitunga mimi nadhani tutunge kwa mujibu wa kutekelezeka. Lakini hali inaonesha kweli bado mazingira ni machafu, hali ni mbaya na hali ngumu ya uchafu iliyokuwepo.

Mhe. Spika, mimi nije katika Sehemu ya Saba katika kifungu cha 92(4) mstari wa pili, watatu, ningeomba hapo tufanye marekebisho kidogo kwa sababu huku hakuna. Katika sehemu ya wadudu, majengo, hapo kidogo kuna mchanganyo wa maneno. Katika sehemu hii ukija kifungu cha 93 (1) kuna suala zima kama nilivyosema mwanzo kwamba sheria hii itawakamata wanyonge na hasa tuseme wazee wetu wa Vijijini.

Mhe. Spika, nadhani hakuna mtu hata mmoja, wewe hupikii makumbi, wala makaa, wala kuni, hupikii Mhe. Spika. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri hapa aje aniwekee wazi na anifahamishe juu ya kipengele hiki. Kipengele hiki kinasema kwamba suala zima la kuweka makumbi. Ukitizama makumbi ni kuni na matumizi ya wazee wetu.

Sisi tunaokaa Vijijini tunajua mazingira ya Vijijini, mzee anangoja anahesabu keshokutwa masika tayari, anahesabu Machi kwamba masika yanaingia, anaanza kukushanya kuni zake kama leo, anaziweka vizuri. Wazee wanatokea hali hii na si wazee tu, kuna watu ambao ni vijana ambao wanachukua hatua kama hizi, wanakushanya kuni zao wenyewe wanaziweka, leo hili ni kosa. Watu wanasema ukuni wa masika hatumwi mtoto maana hakutokeki nje, kumbi, kifuu ndio kuni zake mzee huyu.

Sijui Mhe. Waziri sheria hii katika kuitunga na katika kutekelezeka kwake tunawasaidia nini wazee hawa ambao wanakushanya mititiriko hii ya makumbi, makozi, kuweka majumbani kwao. Mimi nadhani hii sheria tuitizameni vizuri. Ndio liposema kwamba sheria tunapozitunga inaonesha kwamba tunawatungia wale wanyonge. Ni kweli kwamba kututurika makumbi haya au vifuu kunasababisha kuingia panya. Mtu nyumba yake hiyo hiyo anavuna mpunga wake gunia 6, 7, 8, 9, 10 anazituturika ndani pia wataingia panya. Panya wale wataanza kula, wataanza kutoa makapi, baada ya mpunga unakuwa makapi sasa. Yele makapi yaliyokuwepo ndani sasa wanahamia panya.

Kwa hivyo hii hali kweli tunaitunga sheria lakini mimi naona sheria hii nayo ina matatizo kwa upande fulani. Mimi nadhani Mhe. Waziri aje atueleze pia watu hawa tutawapa msaada gani au sheria itawakwama tu, kwa sababu Sehemu ya Pili inasema kwamba

Kifungu cha 93(2) "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi laki moja na hamsini elfu na kifungou cha siku kumi na nne au vyote".

Mhe. Spika, mimi kwa mtazamo wangu naona hii sheria inawagusa hawa wazee wetu ambao wameshazowea kututurika vitu hivi. Kwa hivyo mimi naomba taaluma wapewe na wasaidiwe kwa hali yoyote.

Mhe. Spika, jengine ukurasa wa 270 Sehemu ya Tisa, hapa mimi nadhani bado hatujawatayari kulinda afya za watu wetu hata siku moja. Jambo lolote lenye madhara na lenye matatizo, lenye kuleta athari kwa afya ya binaadamu, Sheria ya Mwenyezi Mungu alipokataza kila kitu anajua kitu hiki kina matatizo basi alikataza moja kwa moja na mwisho Mwenyezi Mungu anatilia mkazo. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu msiikurubie.

Kwa hivyo na sisi hapa wakati tunajua kwamba sigara ina matatizo, halafu tutoe tangazo kwamba hatari kwa afya yako. Sijui tunakusudia nini Mhe. Waziri. Hapa hatujawa tayari kuwaonea huruma wananchi wetu kutokana na kulinda afya zao, bado. Leo daktari atakwambia sigara ina hatari kwa afya yako.

Mimi Mhe. Spika, kwa hili naona gumu sana, kwasababu hata katika familia yangu nimeshapoteza watu wengi kwa sigara. Nilikuwa nina marehemu bibi yangu aliugua, daktari akamwambia usivute sigara. Lakini mtu kama huyu keshajua kwamba miye hichi kweli nimeshaambiwa kina hatari anamtafuta mtoto mdogo anamwambia kaninunulie sigara na kibiriti. Anakuja nayo yule mtoto na yeye anachukua anavuta. Lakini je, ingelikuwa haimo madukani angenunua wapi, asingeipata.

Kwa hivyo tunavyopiga vita kwamba kitu fulani kina athari kwa afya ya binaadamu, mimi nadhani moja kwa moja iwe ni marufuku kuingizwa katika nchi. Siku zote tunasema kwamba tunapiga marufuku ukimwi usiingie lakini tunatangaza na tunaweka kinga kondom. Hizi ndio athari tulizonazo, tunatunga sheria kwamba ukimwi usiingie lakini tunaweka kondom na ukimwi ukija unaripuka. Leo tunapiga marufuku tunasema sigara ni hatari kwa afya yako lakini kimewekwa kidhibiti zitakapo ingizwa sigara ziwe na tangazo hili. Mimi nadhani bado hatujawatendea haki wananchi kutokana na sheria hii hasa kwa hapa.

Ukija huku hii sheria inasema kwamba hakuna mtu yeyote chini ya umri wa miaka 18 atakayeruhusiwa kununua pombe, kunywa ulevi, kwenda katika mabaa na club wakati wa usiku. Lakini hakuna sehemu yoyote iliyooneshwa hapa angalau mtoto miaka 18 kuvuta sigara pia. Hivi sasa watoto wetu kuanzia miaka 6 wanaanza kuvuta sigara, wapo skuli ndio zinapoanza kuvutwa sigara 6, 7, 8 pale ndio wanapoanzia. Leo kavuta sigara, kesho na keshokutwa anabadilisha sigara anaonja chengine. Hatimaye huyu mwisho anakuja kuwa mla unga mkubwa lakini wameanzia kwenye sigara hawa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nadhani haya tusiyaruhusu katika sheria, tuondoe kabisa suala la kuingizwa sigara au vyenginevyo babu Duni Waziri wa Afya atuekee tiba nyingi, dawa za kutosha ya kuwatibu watu wanaovuta sigara.

Mhe. Spika, Makka ukiingia katika lango utakuta kuna picha ya moyo halafu na ile sigara imegandishwa pale. Mimi si mvutaji wa sigara lakini nilipoona nikaona kumbe hii ndio athari ya sigara ilivyo. Tayari nikaanza kutoa taaluma niliporudi huko, nawambia watu jamani athari yake ndio ile. Kwa hivyo bado leo hii hali tukaweza kuruhusu hali hii Mheshimiwa, mimi nasema tutafuteni dawa za kutosha za kuwatibu watu wanaovuta sigara. Leo tunaona hali ilivyo, hata mtu anajua hichi kitu kina hatari lakini atakwenda kukitafuta tu.

Mhe. Spika, mimi kwa Mswada huu kwa kusema ukweli nimesimama kwa suala hili ni suala ambalo linaniumiza katika nafsi yangu. Leo tunaruhusu mambo haya yatolewe matangazo, matangazo ya ulevi. Mheshimiwa sote ni wenye kwenda kuulizwa. Mimi nasema Mswada huu siuungi mkono na katika vipengele hivi nilivyovitaja basi utakapopitishwa mimi ningeliomba niruhusu nitoke nje.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa hii ya kuchangia mawili matatu juu ya Mswada huu muhimu ambao unahusu mazingira yetu.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Bububu kwa kuapishwa leo rasmi hapa kuweza kuchukua jukumu la kuwatumikia wananchi wa jimbo la Bububu, Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheria na afanye kazi zake kwa ufanisi mzuri sana kama ambavyo watu wa jimbo la Bububu wamekuwa wakitarajia kupata mchango huo kutoka kwake.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sasa nije katika suala zima la Mswada wetu huu.

Mhe. Spika, nimejitahidi sana kuingia ndani katika Mswada huu na kuweza baadhi ya vipengele vingi ambavyo vimekuwa vimeainishwa katika Mswada huu. Kimsingi ndugu yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub amezungumza mambo ambayo baadhi yake yana matatizo katika Mswada huu. Kuna mambo Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwa kina kabisa juu ya zile hoja ambazo Mwenzetu Mhe. Jaku Hashim Ayoub amezizungumza. Zipo hoja ambazo zina mantiki ndani yake na zipo hoja ambazo zinataka maelezo na ufafanuzi zaidi ili tuweze kuelewa zaidi katika hayo.

Mhe. Spika, pamoja na yote hayo vile vile ningependa kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na kazi nzito na kubwa ambayo amekuwa akiendelea nayo na ambayo aliianzia Pemba juu ya kutoa semina elekezi kwa watendaji wakuu wa serikali. Semina ile Mhe. Spika, inaweza ikawa kichocheo na jawabu muwafaka kwa baadhi ya hoja ambazo waheshimiwa wajumbe walikuwa wakizielezea katika namna ya kuchangia katika Mswada huu.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kueleza hayo, sasa napenda kuchukua fursa hii kuelezea namna ambavyo ninaelewa na hali ninavyoiona katika mandhari yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, suala la usafi katika Mji wa Zanzibar ndio suala kuu ambalo linaendana na mustakbali mzima wa madhumuni ya Mswada huu kama ambavyo ilivyokuwa imewasilishwa hapa na Mhe. Waziri husika katika Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kusema kweli afya ni usafi na usafi ndio afya. Lakini kwa kuangalia mandhari yetu ya Zanzibar kwa kweli hali ya usafi hairidhishi kabisa kabisa. Sheria hii ambayo tunaitunga sasa hivi ili baadhi ya sheria ziweze kuchukuliwa hatua na faini ziwe zinatolewa kwa wahusika. Hii inaweza kuleta matatizo kwa wananchi wetu na tukafika pahala tukaona wananchi wao wanakuwa ni watu wanaoteseka kutokana na zile adhabu za faini ambazo kuwa zitakuwa zinalipwa kutokana na uhalisia wa hali zetu.

Lakini pamoja na yote hayo, wananchi na wao wanajukumu vile vile katika Mswada huu. Kwa kutolea mfano Mhe. Spika, nyumba za Maendeleo za Michenzani, Kilimani na Kikwajuni. Maeneo haya yamefikia pahala sasa zile taka baada ya kuwekwa chini sasa zinawekwa juu ya majumba. Hili ni jukumu la wananchi wenyewe, si jukumu la serikali wala si jukumu la kusema labda la watu wa Manispaa. Watu wa Manispaa sio watu ambao wanakaa juu, kama ambavyo baadhi ya wajumbe wamekuwa wakichangia kwamba hili ni suala ambalo linasababishwa na

Serikali Kuu. Serikali Kuu haimshawishi mtu kwenda kuchukua taka atoke kwenye ghorofa yake ya 3 ya 4 au ya 5 akapeleke juu katika majumba ya maendeleo. Hili ni tatizo ambalo linasababishwa na wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, kwa kupitia fursa hii mimi ningependa kutoa wito maalum kwa wananchi wote na wakaazi wa Zanzibar hususan katika nyumba za maendeleo. Huu utaratibu wa kuchukua taka taka na kuziweka juu katika majumba haya, si utaratibu mzuri na uwachwe mara moja ili kujiwekea afya zetu ziwe nzuri na salama katika maisha yetu tunayokwenda nayo siku hadi siku.

Mhe. Spika, kwa siku ya leo nilikuwa nataka kuchangia hoja zangu kwa ujumla tu, sitaki nende katika vifungu.

Mhe. Spika, tuna matatizo katika miji mbali mbali ya Zanzibar, ikiwemo matatizo ya misingi ya kuhifadhia maji machafu. Katika maeneo mengi ambayo tunakaa tuna mitaro mingi sana ambayo imetengenezwa ipo kwa sababu ya kusaidia kuondosha maji machafu katika maeneo ambayo wananchi wanaishi kikawaida. Misingi hii naona imekuwa kama mapambo. Serikali timetumia fedha nyingi sana kuweka misingi ili iweze kusaidia wananchi wasipate usumbufu juu ya maji machafu ambayo yatakuwa yanapatikana kwa namna moja au nyengine. Misingi hii imekuwa hewa, imetumia gharama kubwa lakini kazi zake kusema kweli sisi wengine tunaweza kusema kwamba hatuzielewi. Kwa mfano:

Mhe. Spika, katika eneo la kutokea Mpendae kuja maeneo haya ya Migombani mpaka ukashukia Kilimani, kuna misingi ambayo inachukua maji lakini maji yale uendaji wake unakuwa wa mitihani. Serikali imegharamika fedha nyingi sana kwa ajili ya kuweka mitaro ile ili iweze kuwasaidia wananchi waweze kuondokana na matatizo ambayo yanaweza kuwakabili.

Kama hiyo haitoshi Mhe. Spika, katika maeneo ya jimbo la Kikwajuni, kuna misingi imetokea katika maeneo ya Gongoni tukashuka mpaka kwenye Msikiti Mabati kule. Misingi hii ipo mingi lakini kati yake kusema kweli hatuielewi. Sasa hii inasababisha uharibifu wa mazingira na ule uchafu wa maji machafu kuweza kuingia katika nyumba na maeneo ambayo wananchi wanaishi na baadaye kusababisha maradhi ya aina tofauti na wananchi wale wakapata usumbufu wa afya zao.

Katika kulitekeleza hili ningeliomba sana Mhe. Waziri wa Afya pamoja na sekta husika za wizara nyenginezo ikiwemo Manispaa na maeneo mengine mengine, hebu wajitahidi kuona haya maeneo ambayo mitaro hii inapitisha maji ili yaweze kufikia pembezoni na mwisho wa bahari kule, njia hizi ziwe zinatengenezwa ili wananchi wetu waweze kupata hizo afya safi na salama na waweze kuondokana na matatizo ambayo yanawakabili.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa nataka kuja katika kifungu ambacho wenzangu wamekizungumzia sana. Kwa kweli kifungu cha Nam. 112 Mhe. Spika, kina walakin katika maisha yetu ya Kizanzibari hapa, hususan katika zile *culture* zetu. Hapa kama wenzangu waliotangulia kusema kwamba kifungu hichi kina matatizo. Kwa sababu kitakuwa kinatoa muelekeo na ruhusa ya kuweza kutumiwa vilevi ndani ya visiwa vyetu

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naona ooo Mheshimiwa uendelee.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kifungu hiki kwa kweli maelekezo yake hayatoi picha halisi ya asili ya kizanzibari pamoja na silka na mila zetu ndani ya nchi yetu. Ningeliomba na ningelipenda kuungana na wenzangu vifungu hivi tuviangalie tena kwa umakini zaidi na kuweza kuangalia namna gani ya kuweza kutumia lugha ambayo inaweza kusaidia ikawa nzuri zaidi kuliko lugha ambayo hapa imetumika kwa maslahi na muelekeo wa wananchi wa Zanzibar.

Baada ya maelekezo hayo sasa, mimi na wananchi wa jimbo langu la Kikwajuni naunga mkono hoja lakini vile vile ningependa kupata ufafanuzi wa kina kuhusiana na masuala ambayo yalikuwa yanataka ufafanuzi zaidi kama wenzangu walivyotangulia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia mswada huu ambao uko mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kutujaalia kutuleta hapa tukiwa na afya njema katika Baraza lako hili tukufu. Pia Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa SMZ aliyewasilisha mswada wake huu. Kwa kweli Mhe. Spika, nimefarajika sana mimi binafsi kwa kuona kwamba tumeingia katika Baraza lako tukufu kwa kujadili miswada hii na hasa huu mswada wa leo hapa.

Mhe. Spika, pia nimshukuru ndugu yangu Hussein Bhaa ambaye leo hapa ameapishwa rasmi na namuombea Mwenyezi Mungu amjaalie aweze kutekeleza majukumu ambayo aliyopewa na wananchi wa Bububu. Mhe. Spika, kiukweli kwamba sisi ni wanadamu na niseme kwamba wanadamu kama wanadamu basi hatujakamilika ni lazima tuwe na kanuni vile vile na kuwa na sheria ambazo zitatuongoza katika maisha yetu ya kila siku.

Nichukue fursa hii niwatake Wajumbe kwamba miswada hii tuisome vizuri na tuichangie ili tuweze kujiwekea zile sheria zetu ambazo zitatuongoza katika maisha yetu ya kila siku. Ni kweli kama wanadamu tutakuwa kuna mambo ambayo yatakuwa na mapungufu.

Mhe. Spika, mbele yetu au ndani ya Baraza hili kutakuwa kuna watu ambao walikuwa *nominated* na wengine ni *elected* lakini sote wajibu wetu ni mmoja ili tuwatendee haki wale ambao wametuchagua, sisi ni Wawakilishi wao kwa hivyo tunafanya kazi kwa niaba yao.

Mhe. Spika, niseme kwamba sheria hii iliyopo mbele yetu ni vizuri na tutakuwa ni wawajibikaji, msingi ule ule mkuu wa uwajibikaji katika kila kwenye kazi zetu basi tunatakiwa tuwe wawajibikaji. Lazima kuwe na uwajibikaji na hili ni jambo ambalo kila pembe yetu basi ni lazima tulitizame suala hili la uwajibikaji. Sisi kama wana familia na vile vile ni Wawakilishi wa watu kwa hivyo mambo haya ni lazima tuwajibike kwao.

Mhe. Spika, kweli uchafu mji wetu umekithiri kuna maeneo na hasa ukitizama pale kitovu cha mji wetu kwa kweli kama walivyokwisha kusema wenzangu kwamba kwa kweli haparidhishi, taka zinanuka mji wote hauna haiba nzuri kwa kweli pale niseme haparidhishi na mji ambao tunasema tunategemea utalii zaidi, kwa hivyo naomba serikali pamoja na wananchi tuwajibike kwa pamoja, hili suala nasema si la serikali peke yake, lakini na sisi kama wananchi basi tuchukue kila mmoja afanye uwajibikaji katika suala hili.

Mhe. Spika, usafi ni tabia kama nilivyosema hili ni jukumu la kila mmoja wetu na itakapotokea athari yoyote basi tujue kwamba tutaathirika sote. Kwa hivyo niseme Mhe. Spika, tuna tabia yetu wananchi pia au wanajamii kutupa taka ndani ya mitaro na baadae mitaro hii kukwama. Kwa hivyo niseme Mhe. Spika, ni lile suala la kuwa kila mmoja ajue umuhimu wa masuala haya ya usafi wa mji wetu. Na hili ni jambo kila mmoja kwa sababu nimeona kwa Wizara ya Afya anachukua nafasi kwa upande wake, vile vile kuna mazingira mengine labda yatamhusu Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa hivyo mambo haya yanakwenda kwa mashirikiano, bila ya mashirikiano nasema hatutofikia yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa sababu hii sheria wenzangu wameshasema na mapungufu wameshayaona na mimi nasema kwa niaba ya jimbo langu la Amani naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mchana huu ya kutaka kutoa maoni yangu mafupi juu ya mswada huu ulio mbele yetu. Pia nimshukuru Waziri kwa kuleta mswada huu mbele ya Baraza letu hili ili kujadiliwa.

Mheshimiwa, mimi nianze niseme kuna kauli ya viongozi huko nyuma kuwa *Zanzibar ni njema atakae aje*. Hapa nimjaalie bwana fulani kuwa ni mgeni kalisikia tangazo hili la kuwa Zanzibar ni njema atakae aje. Mji wetu wa Zanzibar, Zanzibar town ni pale Darajani na kaja mgeni mimi ndio mtembezaji wake namtembeza katika mji ninamwambia ni mwema atakae aje. Yale mazingira ya Darajani peke yake yanatosha kuoneshea kwa tangazo lile si sahihi kwa sababu harufu ya mwanzo atakayoipata mgeni ni harufu mbovu, mbaya ya uchafu, lakini tumemwita kama ni njema aje, je wema wetu ni la uchafu wa Darajani? Ambao ndio mji mkuu wa Zanzibar? Je, wema wetu ni zile taka zilizorundikana? Kwa hivyo Mhe. Spika, bado tuna matatizo juu ya uhifadhi wetu wa mazingira na kulinda afya za watu wetu.

Mimi nikienda pale mjini huenda pole pole na hujaribu kuangalia yale mazingira, wahudumu pale watu wa *municipal* wanafanya kazi mikono haina hifadhi yoyote, wanazoa taka zinanuka vile zinavyonuka. Je kuna kinga gani juu ya wafanyakazi wale ambao wametumikia jamii taka ambazo zimerundikana mbovu zinanuka wao wanazichukua kwa mikono wazi haina hifadhi yoyote, sijui hili ni la Wizara ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndio dhamana zake zile, lakini haya mambo yanaingiliana na hawa watu wa afya, kwa sababu kila mmoja anahitajika atoe taaluma juu ya kuhifadhi hizi afya zetu. Sasa hivi vihatarishi vya afya ya jamii ndio vipi, ni kitu gani ambacho tutakifanya hichi ni cha hatari kwa afya zetu.

Miongoni mwa hatarishi ni huu mrundikano wa takataka ambazo tunashindwa kuziondoa na kuzitupa mahala maalum, kwa sababu popote utapoziweka katika visiwa hivi bado ni maeneo ambayo yapo karibu na watu wanapoishi, waziondoe Darajani mjini wanakwenda kuzipeleka wapi Saateni. Je, kule hakuna watu. Kwa hivyo bado hatujakuwa na mpango maalum wa kuhakikisha kuwa tunaweka mji safi ili kulinda afya za watu wetu.

Mhe. Spika, unapoingia ndani ya soko, uchafu matumbo mabovu ya samaki maji mabovu, samaki wanakokotwa wanaburuzwa, sisi tunahuika kwa vimoja tu tumekuwa *immuned* miili yetu tayari imekuwa *immuned,* na hayo mazingira lakini sote tungelikuwa tunaumwa. Lakini miili yetu ishazoea haya mambo mabovu kwa hivyo nadhani ndio maana tukawa hatuathiriki, vyenginevyo sote tungelikuwa wagonjwa. Kwa sababu kila sehemu unayokwenda hairidhishi kwa mazingira yetu si nje si ndani.

Mhe. Spika, pweza wanauzwa au wamekaangwa muuzaji anapepea nzi sokoni ni hatari kweli kweli Mhe. Spika, ni hatari inatisha inatishia afya zetu. Majumba ya maendeleo yale ya Kengeja kama ningelikuwa nina uwezo mimi ningeliwahamisha jinsi yalivyo mabovu, machafu hayafai kukaa mwanaadamu, lakini bado tunahisi kwamba ni ya maendeleo. Kama ubovu ni maendeleo Zanzibar tumeendelea, kama uchafu ni maendeleo Zanzibar tumeendelea, lakini kama haya si maendeleo Zanzibar tuko nyuma tena sana. Kwa hivyo tuchague uchafu wa mazingira ni maendeleo? Kama ni maendeleo tujisifuni na tuwaambie wageni kuwa Zanzibar ni njema apendae aje.

Mhe. Spika, hapa vimetajwa vifungu kinachomtaka mtu ambaye yuko chini ya miaka 18 asiuze, asivute mambo ya ulevi, hii inamuhalalishia mtu mwengine kwake ni ruhusa akipenda alewe, alimradi tu muuzaji wa ulevi huo atoe onyo. Mimi Mhe. Spika, sikubaliani na hili tamko kuwa kuna ulevi halali, ulevi wote ni haramu hii si taasisi ya kidini lakini sisi ni watu wa dini. Kwa hivyo kupisha kifungu hiki kwa kusema ndio kwa kweli ni mtihani kwetu, ni mtihani tena mkubwa ikiwezekana vifungu hivi vyote ambavyo vinagusa ulevi ulevi viondolewe katika mswada huu kwa sababu havina muelekeo hapa.

Mhe. Spika, usafi wa mazingira, pamoja na usafi katika vyanzo vya maji nao pia unahitaji kuzingatiwa, kwa sababu mara nyengine pahala ambapo pana chanzo cha maji pengine pana mifugo inayokwenda ovyo, inakwenda haja zote mbili ovyo, hatimae vinaingia katika mkondo wa maji. Kwa hivyo ili kulinda afya za watu wetu, lazima kila sehemu inayohusiana na matumizi ya wanaadamu tuiangalie kwa udhati kabisa.

Zamani ilikuwa wagonjwa kama wa kifua kikuu ilikuwa wanatengewa sehemu maalum, kwa sababu sijui kwa sasa ikoje lakini zamani ilikuwa anapokohoa anatoa hewa wale wadudu wanasambaa mtu mwengine ambaye atavuta hewa ile anaambukizwa. Anapokohoa kohoo lake linapoanguka chini likakauka unapovuma upepo wadudu wanapopeperuka wanamuingia mtu mwengine. Makohoo yale yanaharibu mazingira kwa afya ya jamii. Kwa hivyo zamani hawa walikuwa wanadhibitiwa sasa sijui wagonjwa wa namna nadhani wanaachiwa tu hivi hivi je siku hizi hakuna yale maambukizi kupitia njia ya hewa? Kama ipo siku hizi inachukuliwa juhudi gani za watu wenye magonjwa ambayo yanaambukiza na kuachiwa tu wanakwenda bila ya kinga yoyote nyengine.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kweli hali si nzuri na sina hakika mswada huu unapokuwa sheria, sheria hii itakuwa na uzito gani kwa kuweza kufanya kazi ili hilo lengo lililokusudiwa lifikiwe. Kwa sababu hapa Mhe. Hamza *slogan* lake siku zote ni kuwa sheria zetu ni nzuri lakini zinakosa usimamizi kila anapozungumza anasema hivyo. Na kama kungelikuwa kuna usimamii mzuri wa afya, usimamizi mzuri wa *municipal* na halmashauri za wilaya ingelikuwa hakuna mrundikano wa taka na mji ungelikuwa safi na ule wito wa kitaifa wa kuwa Zanzibar ni njema apendae aje ungefikiwa.

Mhe. Spika, ningeomba nimalizie hapo kwa vile mimi bado siungi mkono mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na kumaliza muda wetu wa mchango naomba nikuarifuni rasmi kwamba pale juu katika eneo la wageni, yupo ndugu yetu Mhe. Alphonso Balozi wa Marekani nchini Tanzania. *May officially recognize his presence to see our session going on, Mr. Alphonso you are most welcome.*

Waheshimiwa kuna dakika kumi na tano zile za kumaliza majadiliano kwa mchana huu.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *subhanahu wataala* aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa leo hii kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa

letu. Lakini pili nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nami nafasi hii ya kutoa mchango wangu mfupi katika mswada huu ambao upo mezani wakati huu.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii ya Afya kwa kuliona hilo kuona kwamba umefika wakati wa kuwa na sheria juu ya hifadhi na usimamizi wa vihatarishi vya afya ya jamii Zanzibar. Sheria hii ni nzuri na ni matumaini makubwa kwa taifa lolote lile duniani linalohitaji maendeleo ya kweli, ni lazima kuweka utaratibu maalum ambao kufuatwa kwake ni kuijengea jamii afya bora, lakini pia kuijengea misingi imara ya uchumi madhubuti. Taifa ambalo watu wake mazingira yao yamezungukwa na hali mbaya ya mazingira machafu, nadhani hata shughuli zao za kimaendeleo zinakuwa finyu na mara nyingi watu hao au jamii hiyo hukumbwa na matatizo ya maradhi ambukizi au maradhi ya mripuko.

Mhe. Spika, kimtazamo mimi nilivyouangalia huu mswada vipo vipengele ambavyo vina matatizo ukizingatia mila na silka za kizanzibari, lakini ziko sehemu kwa kuwa mswada huu umeletwa na Wizara ya Afya ambao ndio wenye jamii ya kutunza afya ya jamii na kujua afya na hali za wananchi, basi ipo haja ya kuangalia vipengele vyengine kuona kwamba wao wana haki ya kuuleta mswada huu katika Baraza hili tukufu kwa ajili tu ya kulinda afya za jamii au afya za wazanzibari.
Hivyo basi ni wazi kwamba sote tunaelewa kwamba mazingira ya Zanzibar kwa sasa hayakuwekewa utaratibu maalum, mswada umeonesha hapa kwamba sheria ilikuwepo lakini ilifutwa. Na tangu 2006 hadi hii leo hali haikuwa nzuri na hakujulikana nani wa kusimamia hilo, pamoja na kuwepo sheria nyengine ambazo kiupande mwengine zilikuwa zinasimamia hilo lakini kama tabia yetu ilivyo, mara nyingi tunapitisha sheria lakini tatizo letu bado linaganda pale pale katika utekelezaji.

Mhe. Spika, wenzangu wengi wametangulia kuyasema mengi yale ambayo wanaona kwamba imekuwa ndio tatizo kuu. Nadhani kwa Wizara ya Afya wao wameona ili kuondoa hayo basi walete mswada huu kuona kwamba sasa hali ya masoko basi sheria yake ni hii kupitia Wizara ya Afya. Sasa usimamizi huu wa sheria ndio suala ambalo limekuwa ndio kikwazo kikubwa sana hapa kwetu Zanzibar.

Wakati tulipokuwa tukiupitia mswada huu tuliona kwamba sheria hii ya usafi na uhifadhi wa jamii ilikuwepo tangu nimesahau kidogo lakini wanasheria waliliona hilo kwamba ilikuwepo hii sheria, lakini baadae imepotea katika mazingira yaliyojulikana na hatimae sisi umefika wakati kuona kwamba kuirejesha sheria hii, kwa kuijengea afya za jamii wetu basi ipo haja ya kuleta sheria hii ili isimamiwe ipasavyo.

Mhe. Spika, ni dhahiri sote tunaona kwamba uchumi huu wa taifa letu tunasema kwamba tunatumia au pato la taifa linapanda kupitia utalii. Hivyo basi bila mazingira salama, bila jamii ambayo imesalimika sidhani kwamba hata hao wageni ambao wanahitaji kuja hapa na kuwekeza na kuweza kuongeza pato la wananchi wetu wanaweza wakaja bila ya usafi wa mazingira na afya nzuri kwa jamii wanayoikuta katika taifa lolote lile. Hili nimeliona kwamba ni kweli kabisa kuwa mji wetu utaratibu wake si mji tu kwa sababu sheria inapotungwa hawatungiwi watu wa mjini, bali hii sheria ni kwa ajili ya nchi nzima na kwa wananchi wote. Ni dhahiri kabisa kwamba kuna vifungu vya mazingira na afya nzuri kwa jamii wanayoikuta katika taifa lolote lile.

Hili nimeliona kwamba ni kweli kabisa kwamba mji wetu utaratibu wake si mji tu kwa sababu sheria inapotungwa hawatungiwi watu wa mjini, bali hii sheria ni kwa ajili ya nchi nzima na kwa wananchi wote. Ni dhahiri kabisa kwamba kuna vifungu vinahitaji marekebisho na kuna vifungu vinakubalika. Kwa sababu uwajibikaji tu ndio imekuwa ndio tatizo sugu kila mmoja kama atachukua jukumu la kutekeleza wajibu wake nadhani Wajumbe wote wasingesema kwamba wanapinga mswada huu, wale ambao wamepinga wangesema leo wanaukubali mswada huu.

Tatizo hili limekuwa kikwazo kikubwa kwa taifa letu, huu ni ukweli usiofichika. Lakini nadhani umefika wakati serikali iendane na hali ya dunia inavyokwenda. Wananchi wetu sasa hivi wapo katika sayansi na teknolojia, wanaona mambo mengi kupitia mitandao mbali mbali, wanajua kila kitu si wa kudanganywa tena. Hivyo basi kutunga sheria hizi na baadae zisitekelezeke nina wasiwasi hatimae wanaweza kukosa imani na Baraza hili. Tunazipitisha na hatimae utekelezaji wake unakuwa finyu. Mimi nadhani Manispaa ina majukumu yake inajua na upo utaratibu maalum, asubuhi hii ya leo tu nadhani sote tumekuwa mashahidi tumemsikia Waziri alivyokuwa akijibu hapa kuhusu taa za barabarani, jambo ambalo limeanzishwa na muasisi wetu marehemu Mzee Abeid Amani Karume tangu 1964 aliweza hilo.

Lakini tujiangalie sisi tuliorithi baada ya kufa kwake ambaye tumesema tutarithi yale yote mema aliyotuachia, hebu tuone kuna nini hasa hata zimeshindikana taa za barabarani tu. Nadhani kama tutaiga na tutakuwa na moyo huo na ushujaa na uzalendo wa taifa hili wa kuwatumia raia wa nchi hii, nina imani kwamba hili au mswada huu utakapopitishwa kama utatekelezwa basi nadhani ni neema ya wananchi wa nchi hii na ni sifa kwa viongozi watatekeleza haya kwa maslahi ya wanaowaongoza.

Ni mara nyingi imezoeleka kuona wenzangu wamepima vipimo mbali mbali lakini sisi tumeona kwamba taswira ya mji wa Zanzibar imekuwa ni tishio kubwa.Wageni wengi wanapotoka sehemu tofauti tofauti basi kioo chao huangalia ule mji. Tumeacha taa kwamba zimeshindikana lakini tuangalie na usafi wa mazingira ukoje na afya za wageni ambao wanaingia katika nchi hii nayo ikoje. Nasema kwamba mswada huu, sheria hii, kama inatekelezeka kama itatekelezwa imani hiyo ikajengwa nasema kwamba Wizara ya Afya kwa upande wake itakuwa imetekeleza majukumu yake ya kuwajengea afya bora na kuwahadharisha wananchi wake lakini pia lazima wasaidiwe kujengewa misingi imara ya kuweza kutekelezwa sheria hiyo. Wao ni sehemu moja ya kuona kwamba hili na lile lakini kuna sehemu nyengine ya utekelezaji wa sheria hii. Kwa hivyo sheria hii inahitaji nguvu za serikali kuona kwamba zitumike.

Kuna vipengele ni kweli kabisa lazima viende na mila, utamaduni na desturi zetu, tukikiuka hayo tutakuwa na sisi pia tumelichafulia taifa letu ile sifa yetu hasa na utamaduni wake tutalipotezea. Lakini ni dhahiri kwamba tutapoyatengeneza haya mengine tukayaweka vizuri, Wizara ya Afya wamewaweka watu vizuri kuona kwamba kuweka taka na kurundikana ni athari kwa afya yako. Kwa hivyo kuwe na hukumu maalum na utaratibu na mkondo ule upitiwe hivyo. Kwa ufahamu wangu mimi Mjumbe nilivyoliona hilo nimeliona katika hali hiyo na kuona kwamba wale ambao wanawaletea adha wenziwao kuona uchafuzi wa mazingira, kuona afya za jamii zinaharibika au kuathiriwa na kitu hilo ama kile chengine, zikiwemo sheria za kujenga kama viwanda katika maeneo ambayo wananchi wanaishi yanaweza yakaleta athari nilivyouangalia mimi niliuona kwa msingi huo.

Haya kujiwekea misingi imara ya kuona tunafanya udhibiti nakubaliana nayo, lakini cha kujiuliza na kusikitisha ni kusema kwamba humu mna mipango na *plan* ya mji, kuna maeneo wazi chungunzima ambayo yalikuwepo katika kipindi cha nyuma leo hayo yote nayo yameshajengwa, na waliojenga kwa vyovyote vile wamepewa vibali na nani suali la kujiuliza hilo, nani kawapa vibali? Mwananchi wa kawaida si rahisi kuweza kuingia popote na akaweza kulifanya hilo, nadhani kama tutakuwa tumejiangalia na kujichunga hasa na kuwa na imani na taifa hili tukaona zile sheria tunazojijengea tunaziwekea utaratibu wa kuzifuatilia, basi nadhani haya yasingekuwepo.

Kwa sababu moja katika kujenga afya ya jamii ni lazima uangalie *open space* kwa kupata afya zao na hewa safi na viwanja vya michezo, hivyo sasa vimejengwa vyote mjini Unguja. Sehemu za kuwekea mataka wenzangu wamesema hapa hazipo ni kweli hakuna sehemu za kutupia takataka tunahama hapa na pale, tumekosa *master plan* yenyewe kabisa ya utulivu, nani anahusika tunashindwa kuwajibika.

Umefika wakati tuwaonee huruma wazanzibari wenzetu tuwaonee huruma ndugu zetu, imefika sasa kuna kwamba iko haja ili taifa hili likwamuke na lifikie katika hali nzuri hata uchumi wake ukue kweli kweli na wananchi wafaidike na uchumi huo, basi taifa hilo lifuate utaratibu wa sheria. Na ninadhani tuliweka Wizara nzima Rais ameiweka hii ya sheria na utawala bora ili kuona kwamba mambo haya tunafanikiwa. Cha kusikitisha ni kuona wale ambao wanatuhumiwa na kuhusika hatimae hakuna hukumu inayotolewa.

Mwenzangu aliyetangulia kuchangia hapa alisema rushwa sasa katika taifa hili imekuwa ndio inayoongoza kwa ajili ya utendaji wa shughuli zote, hili ni tatizo tutawakabidhi wizara wenzetu kwa ajili ya utendaji, lakini tutakapowaambia tuleteeni sheria wakakaa na kujifungia wakapoteza fedha za serikali kwa ajili ya kujifungia na hatimae sheria hizi zisitekelezeke nasema ni kuwadhulumu wanyonge. Ni kutumia pesa za wavuja jasho kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa mimi nilipata taaluma wakati nikiwa ninaupitia mswada huu kuna sehemu niliziona niliouona umuhimu wake. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe baada ya majumuisho ya Mhe. Waziri ambapo atapewa uchambuzi wa kina yale ambayo wameyachangia lakini na mengine ambayo yamebaki humu tuyapitishe tuyakubali.

Lakini pia mwisho niseme kwamba na utekelezaji wa sheria hii au usimamizi ni suala la msingi, upitishwaji wa sheria tu hautoshi utungwaji wake bali utekelezaji wake hiyo ndio hatua muhimu.

Baada ya kuyasema hayo nasema ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni kwa mashirikiano yenu katika kuendesha shughuli za Baraza. Sasa wakati umefika tukapumzike, tuna shughuli pale Fumba baada ya kutoka hapa lakini tukumbuke jioni mnamo saa kumi na moja tuwepo hapa kuendelea na kazi zetu. Naakhirisha kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii nikiwa mchangiaji wa mwanzo kwa wakati huu kwenye mswada huu wa Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambapo mswada huu tumeupitia kwa siku tano. Hii ni kuonesha kwamba mswada ulikuwa mkubwa, mswada ulikuwa wa kitaalamu na tulilazimika kubakia siku nyingi ili kupata maelezo ya mswada huu kwa kina ili kuweza kuwasaidia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Lakini kabla sijachangia nikupongeze wewe Mhe. Spika, kwa niaba ya Baraza kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapata wadau kabla mswada kuja kwenye Baraza. Kamati yangu imefanya hivyo na tumewaita wadau wasiopungua Taasisi 12 ambapo mafanikio haya ya marekebisho tuliyoyapata ni kutokana na mchango wao kama wadau wa miswada miwili ya Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa niende moja kwa moja kwenye kifungu cha saba usafi na makaazi ambapo kamati yangu imeona busara kuongeza kifungu cha 7(3) kwa lengo la kuainisha adhabu ambayo makampuni na Taasisi binafsi watazipata.
Kifungu cha saba kinaonesha zaidi mkosaji ni mtu wa kawaida tu, lakini kampuni ilikuwa haijaonesha kama itafanya makosa haya adhabu gani watakayoipata. Kwa hivyo, kifungu cha 7(3) kamati yangu imeongeza ili kuweza kutoa makosa kwa Taasisi au kampuni ambazo zitasababisha makosa kwenye kifungu hiki.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho ningetaka nikizungumzie ni kifungu cha 15, kifungu hicho cha awali kilikuwa kinasomeka kwamba, mtu atakayekiuka masharti ya kifungu cha 12, 13 na 14 vya sheria hii atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi 500,000/- na kifungo kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa ujumla. Lakini kamati yangu pia iliona busara kwamba tuongeze kifungu cha 15(2) ili pia tuainishe makosa ambayo yatafanywa na taasisi na makampuni binafsi. Kifungu cha 15 kilikuwa kinamuonesha mtu wa kawaida tu, lakini hatukusema kampuni itakuwa na hatia gani. Kwa hivyo, kamati yangu iliona busara kwamba si mtu wa kawaida tu kwamba akifanya kosa lakini na makampuni na Taasisi za serikali zikifanya kosa pia ziwe zinawajibika kwenye sheria hii na zipigwe faini na kwa niaba ya mkuu wa taasisi hiyo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningesema kwa ufupi mswada huu niseme tu kwamba kifungu cha 5(3) Kamati yangu imeona busara kukifuta. Kwa sababu ilikuwa inaonesha dhahiri kwamba hakuna haki ya rufaa jambo ambalo haki ya rufa ni haki ya kila raia hivyo Kamati yangu iliona mswada huu unamzuia Mzanzibari au mwananchi wa kawaida kukata rufaa pale ambapo atahisi mambo hayako sawa. Kwa hivyo, Kamati yangu iliona busara kuwa kifungu hicho kifutwe na badala yake tuongeze maneno ya kuwepo na haki ya rufaa kwa mtu atayeona hakutendewa haki.

Mhe. Spika, jambo jengine ninalotaka nichangie kwenye mswada huu niipongeze Kamati yangu kwa jumla ni kifungu cha 58. Kamati yangu Mhe. Spika, pia iliongeza badala ya 58(1), (2), (3) Kamati yangu iliongeza 58(4) kama ifuatavyo. Sehemu hii ni kwa ajili ya kujumusiaha sehemu yoyote ya kuingilia Zanzibar iliyo rasmi na isiyo rasmi, yaani kifungu cha 58 kinaeleza taarifa ya maradhi ya kuambukiza hakikuonesha maradhi haya yataingia sehemu gani. Kwa hivyo, kifungu cha 58(4) kamati yangu ikaona busara kuainisha kwamba maradhi haya yakiingizwa kwenye bandari rasmi na iliyokuwa sio rasmi yote inahesabiwa ni makosa na kwa hivyo sheria ichukue mkondo wake. Kwa sababu mswada ulikuwa haujasema ni sehemu gani ambayo maradhi hayo yataingizwa.

Mhe. Spika, tumefikia maamuzi haya kwa sababu Zanzibar zipo bandari za vichochoroni ambazo sio rasmi lakini wajanja huingiza huko mambo ambayo si halali. Kwa hivyo, kama imesema wazi kuwa bandari rasmi ambazo serikali inazitambua na zile za vichochoroni ambazo si halali kiserikali lakini mtu akikamatwa basi lazima awajibike kwa mujibu wa sheria hii ambayo tunaipitisha.

Mhe. Spika, jambo jengine ni suala zima la kifungu cha 72(1). Kamati yangu imeamua kukifuta kifungu hiki na badala yake kifungu cha 72(2) itakuwa ni 72(1) na 72(3) itakuwa ni 72(2). Tuliamua kukifuta kwa sababu iliashiria ubaguzi kwenye haki ya msingi wa mwanadamu, kwa sababu 72(1) ya awali ilikuwa inasema kuwa, ni kinyume cha sheria kwa mmiliki, au dereva mwenye dhamana ya usafiri wa umma kwa kujua kuchukua au kwa madhumuni yoyote yale ya kumuweka katika chombo cha usafiri wa umma mtu mwenye maradhi ya kuambukiza.

Kamati yangu iliona kwamba tukiwazuia watu wenye usafiri wa umma kutomchukua mgonjwa kwa sababu ana maradhi ya kuambukiza huo ni ubaguzi, kwa hivyo tukasema sheria hii ingefanya ubaguzi wa wale wenye maradhi na hili sio jambo la msingi. Kwa sababu mtu mwenye maradhi ya kipindupindu mfano maana yake tunalazimika kumuacha nje bila ya kumchukua jambo ambalo sheria zetu hazikubaliani na ubaguzi wa aina yoyote na badala yake tukakifuta na kuvipanga kama nilivyovitaja hapo juu.

Jambo jengine ambalo ningeligusia haraka haraka ni yale makosa ambayo yamezungumzwa kwa wale wananchi wa kawaida. Nakubaliana kabisa na Mhe. Ismail Jussa kwamba sheria hii ina mapungufu ya kutokutoa adhabu kwa Taasisi za serikali au wale wasimamizi. Kamati yangu pia hilo imeliona na sisi tukakubaliana kwamba sio kwamba adhabu itolewe tu kwa wale wananchi mmoja mmoja, lakini hata serikali yenyewe kwa maana ya Taasisi husika iliyopewa dhamana ya kusimamia sheria hii ikifanya kosa lazima kuwe na adhabu ambayo itachukuliwa kwa Taasisi husika ambayo imepewa dhamana. Hilo mimi naungana mkono na Mhe. Jussa na Wajumbe wengine kwamba lazima taasisi husika iliyopewa dhamana iweze kuwajibika kwa makosa ambayo itafanya chini ya sheria hii.

Vile vile niungane mkono na Wajumbe wenzangu sehemu yote ya tisa ambayo inazungumzia matangazo ya vilevi ikiwemo sigara, pombe na mambo mengine. Nadhani nikiri kwamba Kamati hapa haikuzingatia kwa upeo wake lakini mimi binafsi baada ya kupata michango ya wajumbe wenzangu nimeona kuna hoja ya msingi kwamba si busara sheria ikaruhusu matangazo ya vilevi na kuruhusu biashara ya vilevi waziwazi, nadhani tungewaachia Taasisi nyengine lakini sheria isingetoa mwanya. Vileo hatujatoa mwanya huo watu wanafanya mambo wanayotaka je sheria ikisema kwamba sasa ni ruhusa kufanya biashara ya vilevi nadhani watu watazidi kufanya mambo ambayo si msingi ikwa taifa letu.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono kabisa wale Wajumbe wanaosema kwamba lazima tuwe makini sana kwenye kutoa ruhusa ya matangazo ya vilevi na vibali vya ulevi. Mhe. Spika, jambo hili litawapa wananchi wetu mwanya wa kufanya mambo ambayo si sahihi kwa taifa letu na lazima taifa litakua liko katika hali ya hatari.

Mhe. Spika, kwa msingi huo baada ya mchango wangu huo niseme tu kwamba niungane mkono na wenzangu kuwa kuna haja ya kuangalia sheria hii pale ambapo vifungu ambavyo vimetoa ruhusa kwa ajili ya matangazo ya ulevi na matangazo ya pombe ndahani Mhe. Waziri akubali tuviwache ili isiwe sababu Baraza hili kutoa ruhusa ya watu sasa kuwa kuuza pombe halali alimradi utimie miaka 18, maana yake ikiwa chini ya miaka 18 ndio huruhusiwi lakini kama mimi na wewe Mhe. Spika, tunaruhusiwa tufanye biashara nadhani sio jambo la msingi, si jambo la msingi kabisa na Mhe. Waziri nimuombe kwa niaba ya serikali kwamba walizingatie hili na kuna haja ya kufuta kifungu hiki ili tusitoe mwanya hata kidogo wa kuruhusu Wazanzibari wetu kufanya biashara ya sigara na vilevi kwa kisingizio kwamba ukiamua kufanya basi utoe matangazo tu ndio kinga yake kisheria. Nadhani Mhe. Spika, hili tuliache na itakuwa ni busara na heshima kubwa kwa Baraza letu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada huu.

Mhe. Suleimana Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi angalau ya kuweza kutoa mchango wangu katika mswada huu wa Waziri wa Afya ambao umeleta Mswada wa Sheria inayohusiana na Hifadhi na Usimamizi wa vihatarishi vya Afya ya Jamii pamoja na Mazingira na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mhe. Waziri kwa kazi nzuri pamoja na watendaji wake wote walioandaa mswada huu. Mswada huu kama tutausoma vizuri au kama tuliusoma vizuri tungeweza

kufahamu nini wizara inakusudia katika suala hili zima, lakini ukiusoma kwa haraka haraka itakuwa sisi hatutoweza kufaidika na naamini wananchi wanaotusikiliza hawatoweza kufaidika na sisi tunachotaka kukizungumza hapa ni kwamba tunataka wananchi wafahamu kile ambacho tunakizungumza.

Mswada huu mimi sijaona jipya ndani yake ni mambo ya kawaida ambayo kila nchi inatakiwa iwe na mambo haya mazuri. Sasa sisi tunaonekana katika nchi hii bado hatujafikia ile hatua ambayo tunatakiwa kama wale wenzetu katika nchi zilizoendelea. Mswada huu naupongeza kwa hali yoyote kwamba ni mswada mzuri, mswada umeeleza mambo mengi na mswada ambao ni wa kileo umetimia, unaokwenda na wakati niseme hivyo. Lakini vile vile nataka nitanabahishe kwamba mswada huu unazungumzia mambo mawili muhimu, wizara haikufanya vibaya kusema katika mswada huu ufanyiwe usimamizi wa yale mambo ambayo yanaweza kuhatarisha maisha ya afya ya jamii moja ni hilo usimamizi, lazima wapatikane watu wa kuweza kusimamia kuangalia ile afya ya jamii. Moja ni hilo.

Lakini vile vile wizara imeona kwamba mbali ya afya ya jamii lakini vile vile iko haja ya kuona hali ya mazingira ya hii jamii inayoishi. Kwa hivyo, mambo ni mawili tu, ni kuangalia afya ya jamii na kuangalia mazingira ya nchi yalivyo je yanakwenda vizuri au yanakwenda vibaya. Sasa kwa haya mimi sijaona kama kuna jipya ni mambo ya kawaida. Hivyo, mswada ni mzuri na mimi nauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, katika suala moja zima nililoliona mimi ni makaazi na hili linazungumzia katika usafi huu wa wakaazi halikuzungumzia mjini tu mpaka vijijini. Hilo ni jambo zuri kwamba wizara imeweza kufikiria kuwa hao wakaazi wote wako mjini na wengine wako vijijini kwa hivyo ni lazima tuangalie hali ya usafi wa jamii na hali ya usafi wa mazingira wanayoishi jamii yao.

Halafu wakafikiria vile vile kuweka viwango bora katika usafi, hivi sasa inaonesha kwamba viwango bora katika usafi wa afya ya jamii na mazingira yake hayako katika kiwango. Hilo sio baya ni jambo zuri, kwa hivyo; wizara vile vile imetueleza katika mswada huu kwamba katika suala ambalo linalishughulikia kuna mambo ndani ya afya ya jamii ambayo ni mambo muhimu kwamba humu katika afya zetu kuna mambo mengi ambayo sisi wanadamu tunishi na yale mazingira yetu tunafanya hili na hili. Kwa hivyo, katika mambo ambayo yameonekana ni kwamba zinaonekana kuwa ziko taka ngumu, vile vile kuna taka ambazo zinataka kushughulikiwa kiutibabu na kuna taka nyengine zinahitajiwa kuhifadhiwa ambazo kutokana na uchafu wake unatoa hewa chafu. Sasa hili ni suala muhimu kwamba taka ngumu zijulikane, taka za kitibabu ni zipi na namna ya kuzidhibiti taka zilizokuwa katika hali mbaya ambayo imeingia uchafu.

Mhe. Spika, inaonekana kwamba katika mswada huu ni mzuri sana, inaonesha kwamba hawataki wao wizara kuonesha kuwa hayo yote yanayotokezea yaweze kuenea ina maana wanataka wayadhibiti na hili ni suala zuri kuweza kudhibiti taka zote hizi. Taka ziko kila aina kuna taka za *metal*, kuna taka za *plastic*, kila aina ya taka zipo. Sasa kila moja taka hizo zinahitaji zifanyiwe udhibiti wake.
Lakini cha msingi vile vile wanaona kwamba lazima kupatikane taka hizi wananchi wajue kwamba kuna taka nyengine unaweza ukachimba ukazitia katika ardhi, kuna taka nyengine ni lazima uzichome na taka nyengine ni lazima uzisafirishe ukaziweke mahala pengine. Lakini vile vile wameweka indhari mimi niweze kusoma hii hatarishi ni kama indhari ndio maana ikaambiwa hapa kwamba usimamizi wa vihatarishi vya afya ni kama *caution* unapewa wewe mwananchi kwamba kuna hili na hili usifanye kuna hatari ambayo unaweza kupata athari katika afya yako.

Kwa hivyo, haya ni mambo muhimu lakini vile vile tunaona kwamba mbali ya taka ambazo zitakusanywa katika mji kwenye maeneo mbali mbali basi vile vile kuna taka ambazo zitaweza kuchukuliwa zisafirishwe zipelekwe mahala pengine kwa ajili ya kuhifadhiwa. Lakini ningelimuomba Mhe. Waziri wakati aina ya taka kama hizi zinapochukuliwa zifunikwe ili taka taka hizi zisiweze kuanguka anguka njiani.

Pia nataka nimuulize Mhe. Waziri, kwa kiasi gani amejipanga kwa sababu hili suala ni zito katika utekelezaji wake. Kwanza linahitaji kupatikana watendaji wa kutosha, pili zipatikane nyezo za kufanyia kazi na usafiri wa kuweza kusafirisha taka huku na huku. Je, Mhe. Waziri kwa suala kama hili umejipanga kiasi gani? Je, nyezo zipo za kutosha? Magari unayo na watendaji wapo wa kutosha? Kwa sababu katika suala la utawala kuna Mtendaji Mkuu ambaye ni Mkurugenzi ambaye Mkurugenzi atakuwa ni dhamana wa masuala yote, ambaye huyu utampa mamlaka ya kusimamia shughuli zote kiutendaji. Je, huyu umemuwezesha kiasi gani katika utendaji wake, kwa sababu kuweka tu au kupanga ni lazima umuwekee na mambo yake baada ya kupanga. Je, wizara imejipanga kiasi gani.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba katika mswada huu katika kuzungumzia taka zile hatari na taka zilizokuwa si za hatari, lakini hapa amezungumzia waziri kwamba atazungumza na taasisi zinatakiwa kila taasisi sijui kwa kiasi gani taasisi itaweza kutekeleza masuala haya, kwamba zisichanganyishwe taka zilizo hatarishi na taka ambazo zilizokuwa si hatarishi. Hapa namuuliza Mhe. Waziri ameshajipanga katika masuala haya katika kutoa elimu kwa Taasisi zote kwamba hizi taka zitofautishwe, waweze kuweka taka ambazo ni za hatari na hizi taka zilizokuwa si za hatari.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, haya ni mambo muhimu na ni mambo mazuri, lakini je tuje kwa wananchi ikiwa yeye amejitayarisha kwenye Taasisi kwamba aina zote za taka ziweze kubaguliwa kwa sababu hapa tukija katika taka za hospitali kuna mambo ya sumu, kuna mambo ya damu, kuna mambo ya uchafu chungunzima, je katika utaratibu wake masuala hayo yamewekwa vipi kwa wananchi..
Halafu nirudie katika suala hili hizi hospitali ziko *main hospital* za mjini na kuna hospitali ndogo ndogo ambazo zimeenea katika mashamba ambao wanatumia vifaa hatarishi kwa mfano, sindano, damu, plastiki, vidonda, vipi wanawekwa hawa katika utaratibu upi hawa ambao wanatoa huduma katika maeneo mbali mbali na mji wetu umejaa *pharmacy* za kutosha. Kwa hivyo, ina maana kama kuna *pharmacy* za kutosha ina maana mahospitali yapo watu watapewa huduma na zile taka taka zake zitakwenda vipi, utaratibu wake utakuwa vipi. Hapa niweze kumuuliza Mhe. Waziri kwenye hizi *private hospitals* ambazo zinatoa hizi taka taka za sumu utaratibu wake utakuwa uko namna gani. Kwa sababu na wao kwa upande wao lazima wajue.

Lakini la pili vile vile tujue je, wananchi wanapata elimu ya kiasi gani katika kuweza kutofautisha baina ya taka zilizokuwa za hatari na taka zilizokuwa si za hatari na taka za sumu. Je, wananchi wetu watapewa lini elimu hii ya kuweza kujua kwa sababu naamini mswada huu utakapopita na utakapokwenda kwa Rais ukirudi hapa baada ya muda itabidi mswada huu ufanye kazi. Sasa elimu ni kitu cha msingi na tunategemea kwamba elimu ingekuwa ni ya mwanzo.

Mhe. Spika, kuna suala la maji machafu ambalo limezungumzwa ndani ya mswada huu, maji machafu yakaro halafu kuna maji mengine ambayo yamo ndani ya karo tunaita utapishaji wa karo, tunaelewa sote tukisema utapishaji wa makaro. Hiki ni kitu uchafu ambapo uchafu huu hautakiwi kuenea katika mji. Je, Mhe. Waziri namuuliza amejipanga vipi katika utekelezaji wa utapishaji wa makaro ambako kuna uchafu uliokuwa mbaya sana na una sumu kali.

Kwa hivyo, hali hiyo hivi sasa inaweza kuwa kwa baadhi ya watu wanaelewa na wengine pengine hawaelewi, kuna maji ya karo, maji ya michirizi, maji yanayofufurika kwenye majumba, hali hii itachukua muda gani kuweza kusawazisha mambo haya Mhe. Waziri? *How long*, kwa sababu haya ni mambo ambayo tunayo katika miji yetu mji wa Zanzibar haujafikia *standard* katika usafi na namshukuru waziri kwa kuleta mswada huu ina maana labda amekwishajipanga vizuri na kama hajajipanga suala hili litakuwa gumu katika utekelezaji wake.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri katika hayo yote tunayozungumza maji machafu, maji ya michirizi, maji ya karo, karo zinazotaka kutapishwa katika mji wetu yapo na yameenea kila pahala na utakapopita lazima uchupishe mguu uchafu unaendelea kila wakati. Kwa hivyo, hapa tunachohitaji kwa jamii ili kuweka afya zao katika hali nzuri elimu ya kutosha inahitajika. Je, Mhe. Waziri katika elimu ya wananchi umejitayarisha kiasi gani? Hilo ndio suala muhimu ambalo linahitajiwa nahitaji kulielewa.
Mhe. Spika, kuna mambo mengine ambayo ni muhimu katika nchi zilizoendelea na sisi tunaiga Zanzibar, sio vibaya kuiga hata kidogo kwa sababu ni *part of development,* kila binadamu kila nchi inatakiwa iendelee na sasa hivi ukitaka usitake ni lazima uweze ku-*cope* na nchi zilizoendelea, huwezi ukabakia nyuma kwa karne hii ukasema mimi ni Zanzibar nchi ndogo, ina watu kidogo, haina maendeleo, haina uchumi, hiyo watu hawakuelewi unatakiwa na wewe uweze ku-*cope* na nchi ambazo na wenzako nini wanafanya na ndio maana tukapitisha mswada huu wengine wakasema kwamba mswada huu ni mgumu, sio mgumu hii ni *caution* yetu sisi hadhar na watu wanasema, "*tahadhar kabla l-athar'* athari yake ni yale maradhi tutakayopata katika uchafu.

Kwa hivyo tunata kuweka vyoo hebu tuiangalie Zanzibar kwa jumla jumla vyoo ambavyo ni *standard* tunajiwa na wageni wengi katika nchi hii tuangalie vyoo vyetu tulivyonavyo, wapi pana vyoo hapa *public*, vyoo vya wananchi na wageni wetu, kwa sababu mtu anaweza kutoka shamba akaja mjini lakini kama vyoo havikuenea kila mahala na vyoo vikawa standard je watu wale waka *defecate* wapi hapana *bush* hapa kama utakwenda *defecate* kwenye *bush* hapa ni *town*. Sasa kama ni mji huu lazima tuweke vyoo vya kisasa wenyewe wanaita vyoo rafiki, *ok* vyoo rafiki

tuwenavyo lakini tunasema ni muhimu kama mlivyozungumza katika mswada kwamba huu unatakiwa katika mahoteli yote, kwenye mikahawa, marikiti ambapo kwenye mkusanyiko wa watu, kwenye kambi za mikutano, kwenye skuli za *primary* na sekondari zote, kwa watu walemavu vile vile.

Sasa masuala haya kusema tu na kupanga sawa mmeshasema mmeshapanga lakini je utekelezaji wake wa haya, Mhe. Waziri hebu akifika hapa aje atueleze amejiandaa kiasi gani kwa suala hili. Kwa sababu hili suala sio baya ni zuri, lakini je *financial* uko vipi, tunaomba hilo suala kidogo akija atueleze. Mimi na-*appreciate* kwamba masuala haya una dhamira ya kuwa yawepo, lakini je umejiandaa kiasi gani?

Katika masuala haya tunasema ni lazima uwepo na usafi, usafi tuangalie kwa Zanzibar hivi sasa Mhe. Spika, bado haujawa mzuri katika mahoteli yetu na maeneo yetu ambayo watu wanajisaidia kwa vyakula vidogo vidogo, ingia hoteli kaangalie, unategemea katika hoteli au mkahawa pawe na maji na sabuni na mkahawa uwe nadhifu ambapo hapana nzi nenda kaangalie katika mikahawa yetu huwezi kuingia, *countless numbers of flies*, nzi wamejaa tele *diarrhea* iko tayari na bado tunaruhusu mpaka sasa watu wanaruhusiwa hakuna usimamizi wa kutosha katika mikahawa na mahoteli yetu. Hili ni suala muhimu tunaijua sote nini *diarrhea*, tumbo la kuharisha na hii inatokana na nzi na nzi wanapochukua kila pahala wanaweza kuathiri vyakula vyetu.

Je, Mhe. Waziri katika suala mikahawa imejaa katika kila kona ya Zanzibar, mahoteli yamejaa katika kona ya Zanzibar na kila pahala je, hii hali ya kudhibiti usafi wa mahoteli yetu katika kuweka sabuni na maji pamoja na kukimbiza nzi walio wengi katika mahoteli. Hilo Mhe. Waziri utapokuja nafikiri utaweza kunigaia maelezo kidogo. Kwa sababu hawa ni wadudu ambao wanaambukiza na hatupendi *infection* na hapa imezungumzwa maradhi ya kuambukiza, nzi wanaleta maradhi ya kuambukiza.

Mhe. Spika, katika mambo mengine ambayo yamezungumzwa katika mswada huu ambayo yanahitaji yazungumzwe na wananchi wafahamu ni masuala ambayo katika tabia ya watu wa Zanzibar nimejaribu kuangalia kila mahala, kila kona ya Zanzibar utakuta chungu ya mawe ambayo imekusanywa kwenye kando ya barabara. Tunataka kuweka mji safi haya mawe mawe yaliyokusanywa katika miji hii ambayo yasiotumika kwa miaka yamekaa pale nini hatari ya kuweka mawe mengi kwa muda mrefu. Hatari yake unasababisha mende, unaweka matandu, unaweka panya na aina yoyote ya vidudu.

Je, Mhe. Waziri katika suala hili ambapo mji wa Zanzibar umejaa mawe kila mahala na mawe yale hayajatumika hayo una yazungumziaje, kwamba chungu za mawe zilizopo na hatari yake huhifadhi hata nyoka anaweza kubakia kwenye mawe yale kama tunataka kuuweka mji wetu katika hali nzuri Mhe. Spika, tunaomba hili suala sijui utatwambia vipi katika masuala haya, ni suala la usimamizi jee tuone wasimamizi wako wanaweza wakakubalika katika masuala haya, kwa sababu huu ni mchakato baina ya wananchi na wizara yako, jee wananchi wapo tayari kwa masuala haya, wapo tayari kuweka usafi wa miji kwa sababu mji wa Zanzibar bado ni mchafu haujawa katika hali nzuri.

Mhe. Spika, tumeona hali ya madawa ya sumu ambayo ni kwa wingi na hii vile vile ni suala muhimu kwamba wananchi wajue nini hizi taka za sumu au taka hatarishi. Halafu katika suala jengine Mhe. Spika, kuna masuala ambayo kwenye mswada huu yamezungumzwa habari ya mitaro binafsi na mitaro ya umma.

Katika mitaro hii kwenye sheria zako umeweka kama maana yake *thirty meters away*, hebu ukija hapa utupe ufafanuzi Zanzibar kama ni Zanzibar, Mji Mkongwe umekuwa nyumba zimekaliana pahala pamoja, hizi thirty meters zitapatikana wapi.

Sasa Mhe. Spika, ninaomba atakapokuja Mhe. Waziri hii aje atueleze maelezo zaidi juu ya mitaro ya binafsi na mitaro ya umma namna ya watu wanavyoshirikiana. Hivi sasa kwa heshima yako Mhe. Spika, katika mji wa Zanzibar katika mitaro ambayo iliyokuwa wazi na mitaro hii imejaa maji, hapo Michenzani ukenda kuna mitaro hivi sasa imejaa maji tele na uchafu wote umo ndani ya hiyo mitaro, hakuna mtu ambaye msimamizi kuona na kupita na wanapita kila siku wanaona, ile ina hatarisha kwa sababu unapoweka maji yanapo tuama pahala ni kizalio cha mbu. Huku tunapiga vita vya mbu, kataa malaria lakini kuna maji yametwama na nzi wanazialiana pale na uchafu wote wa chupa, nguo na karatasi na kila kitu kinatiwa mule ndani ya maji.

Michiri ya maji ipo wazi na hayana mifuniko yamebakia hivi hivi yametwama vile vile, Mhe. Waziri hii ni kazi ndogo huna wasimamizi mpaka hivi sasa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ana kazi kubwa sana uiangalie Zanzibar kwa

macho mawili, upite uiangalie Zanzibar hivi leo ilivyo na hivyo unavyotaka Zanzibar iwe. Hali hii bado ipo michirizi imejaa na maji yame tuama na mbu wanaendelea kutaga katika maji yale.

Mhe. Spika, hapa imezungumzwa habari ya udhibiti wa bidhaa za tumbaku, ulevi. Tumeambiwa kwamba wavutaji wa sigara, tunajua sote hapa kwamba kuvuta sigara ni hatari au sio lakini bado still watu wanaendelea kuvuta. Lakini mimi ninataka kumuuliza swali moja tu Mhe. Spika, Mhe. Waziri. Hivyo sasa tujiulize ni nani mmoja, ni nani mkosa, mvutaji wa sigara au serikali yenyewe ndio mkosa. Kwa sababu ikiwa sigara hukuzileta watazipata wapi wao kuzivuta lakini serikali inaachia sigara zinaingia ndani ya nchi, ninasema kama vile unavyotaka kui-*eradicate* malaria na hapa sijui niseme kui-*eradicate* smoking au vipi, lakini unataka kuondosha au kupunguza kabisa.

Lakini ninajua serikali inatafuta juu ya income kwenye serikali. Wafanyabiashara wakileta sigara serikali inapata *income* ndani yake, mapato yanapatikana lakini sasa tuangalie jee *whichi is better*, kupata mapato au kuhatarisha afya za wananchi katika kuvuta sigara tuone. Hapa hii ni changamoto kwa wizara, ama azipige marufuku sigara Zanzibar zisije, kwa sababu inazungumzwa sigara ni tumbaku na tumbaku ipo ya aina nyingi; kuna tumbaku ya kuvuta kama sigara na kuna tumbaku zile za kuchoma kama ni majani, halafu watu wanavuta, aina nyingi tu za tumbaku lakini zote zinahatarisha. Tumeona watu wanavyopata athari kwenye mapafu yao, mapafu yalivyoharibika kwa uvutaji wa sigara.

Tumeona hapa jinsi machavu yalivyovimba yote yameharibika namna hii, nyama zote zimeharibika ndani. Tumeona ile *system* yote ya uvutaji hewa ni mbaya. Tumeona mambo mengi tu. Sasa kwa hivyo Mhe. Waziri akija hapa angalau aje atueleze jee, utazipiga marufuku sigara zisije Zanzibar, lakini vile vile ukizileta watu watazivuta na huku unazunumza kwamba ni hatarishi. Hii hatarishi ni *caution*, jee sasa una-caution kwenye uvutaji wa sigara lakini serikali yako inaleta sigara, basi ondosha sigara watu wasivute. Akitaka kwenda Dar Es Salaam akinunua lakini hapa isiuzwe.

Lakini jee ukiingia katika haki za bindamu, *Is it right* kwa watu wa nchi usiwaondoshee, ulevi upo hapa Zanzibar au haupo hapa Zanzibar, upo unauzwa. Upo ule wa kugema kwenye minazi na upo ule unaouzwa kwenye maduka. Kun bia, brand, whisky upo hapa ulevi na Zanzibar unaletwa hapa ulevi na serikali inapata *income* na tukileta sigara serikali inapata income, lakini tuangalie which is which, tulete sigara watu waathirike, usiwakataze tu kwa sababu ukiwakataza na ukizileta itakuwa haisaidii kitu. Hapo ninakuachia kwamba hiyo ni changamoto ya Waziri I don't know what are going to do.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ninalotaka nilizungumze juu ya *vaccination and inoculation*. Haya ni masuala muhimu na ni masuala international si ya Zanzibar peke yake. Kila nchi ni lazima idhibiti watu wake, mtu yeyote anayeingia Zanzibar masuala haya yawepo. Haya wala sio masuala mageni hata sisi tunapotaka kuondoka kwenda nchi za nje ni lazima twende tukachanje tupige na sindano tukitaka kusafiri na uwe na kadi maalum.

Ninakumbuka zamani kulikuwa na kadi za rangi ya manjano. Mtu huwezi kusafiri kabla ya hujapigwa sindano pamoja na kuchanja. Sasa hizi chanjo zimeondoka Zanzibar watu wanapita mlango wa nyuma wanachukua na wakati hajafanya chochote. Hiyo ni *negligence* ya wizara *itself*, kweli ninasema. Kwa nini iwe hivyo. Kama kuna utaratibu mzuri ungeliweekwa utaratibu mzuri kwamba kila mtu anapotaka safari lazima apite katika afisi ile akapate chanjo na sindano ndio aweze kusafiri, na yule atakayeingia Zanzibar hali iwe hivyo hivyo, wanaokuja kwa meli na wanaokuja kwa ndege na kwa njia yoyote ni lazima wachunguzwe afya zao na ni lazima suala la *vaccination* and *inoculation* ni lazima lirudiwe kama kweli tunaitaka Zanzibar tuweke katika afya nzuri za watu.

Sisi hatutaki kutoa watu waliokuwa wabovu tukawapeleka nje na sisi tunataka tuoneshe kwamba watu tunaowatoa hapa tukawapeleka nje huko wamepitia na wao wanaotoka kule nje wakaingia Zanzibar na wao vile vile wapate hifadhi hiyo, ikiwa watu wanaokwenda na ndege na kurudi ndege, abiria wote wanaosafiri kwa bahari. Hiki ni kitu muhimu na cha lazima Mhe. Waziri jee na hapo umeshajipanga.

Haya mambo ya chanjo na sindano umeshajipanga kwa sababu haya ni mambo ya gharama. Ni lazima wizara yako, hapa mimi ninasema fedha uwe nayo kwa sababu huu mradi ni mzito sana, utahitaji fedha nyingi sana za kuendesha mradi huu, usiangalie kwa macho ya woga. Mradi wako utakuwa mkubwa na utahitaji fedha nyingi sana kuuendesha mradi kwa sababu kila pahala panataka fedha, zinatakiwa nyenzo na hawa utakaowatuma lazima uwalipe, fedha hiyo inatakiwa vile vile.

Mhe. Spika, hapa kulikuwa kuna jambo ambalo utalifanyia utafiti kwenye nyumba za watu, *I don't know how are you going to do*, sijui hili utalifanya vipi, yaani mimi ninaishi katika nyumba yangu na kila mmoja hapa anaishi katika nyumba yake lakini kila mmoja ana tabia yake ya kuishi. Kuna wengine wanapenda kuishi katika hali nzuri ya usafi na mazingira safi, kukafagiwa ndani na kama kuna wadudu wakatolewa, kama kuna panya akauliwa.

Lakini kuna watu ndani ya nyumba katika nyumba hizi hizi tunazoishi; mimi ndani ya nyumba yangu watu wanatembea wanatoka chumba hiki wanakwenda katika chumba hiki, inakuwa kila siku wewe unatafuta panya, kwa sababu ni *share negligence* katika hali ya usafi hawashughuliki, panya wanatoka *from one room to another room* kwenye nyumba hizi za Michenzani, ndio hali ilivyo.

Sasa jee ninakuuliza Mhe. Waziri hii utaifanya vipi, nyumba baada ya nyumba au utakuja kuifanya vipi ya kuona kwamba panya hayakutawala katika nyumba, mende, matandu na mazingira ya nje yapo safi ni kazi kubwa na ngumu. Unayo *management* ya kutosha. Kwa hivyo hiyo ni kazi ambayo Mhe. Waziri changamoto ninakupa ni kubwa sana hiyo na unahitaji ujikaze kweli kweli uje utupe maelezo.

Sasa Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo limezungumzwa katika mswada huu ni suala la usumbufu katika majengo ambayo watu wanaishi hayo. Tunaulizana hapa huu usumbufu. Mimi ninataka niseme katika majengo niseme huku ng'ambu kunakwenda vizuri kidogo lakini tuje katika Mji Mkongwe, hali ya mji mkongwe ni nyumba zilizokaliana pahala pamoja, na inawezekana pengine kiafya mtu hapati pumzi, hakuna *ventilation* ya kutosha katika nyumba, panya, mende yamo humo na umeeleza katika mswada wako kwamba utakuja usafishe uondoe yote, *is that possible* Mhe. Waziri ni kweli unaweza ukafanya hivyo. Mji Mkongwe kwanza hauna taratibu hizo, mji mkongwe una taratibu zake ambao huko unakozungumza kwenye haya mambo yote yapo vile vile, vipi utafanya Mhe. Waziri hapa. Utauondosha ule mji wote halafu ujenge nyumba nyengine au utakarabati ule mji na kuondosha ule uchafu, hapo kidogo umetupa kitandawili hapo.

Maana yake umesema hapa mkuu au Mkurugenzi au mtu yeyote anayo mamlaka ya kusema kuuondosha ule mji wote pale ukajengwa vyengine, unakusudia ng'ambu au mpaka huko mji mkongwe. Ninaona kule mji mkongwe kuna utaratibu wake.

Mhe. Spika, hivi sasa katika mji wetu, ninalotaka kumwambia Mhe. Waziri hivyo kweli wizara yako kama ni wizara hivyo kweli kitu kama hiki unaweza ukakifanya wewe peke yako. Mimi lazima hapa mawazo yangu ni lazima papatikane *joint effort*, huwezi kufanya peke yako hilo suala. Hili suala kwanza linamuhusu kila mtu sio Wizara ya Afya peke yake, mimi limenihusu na sote hapa limetuhusu kama ni individual, sote hapa tunawajibika, jee sisi tuliomo humu tunawajibika katika masuala haya kiafya, katika nyumba zetu tunazoishi tunawajibika kufanya haya kwa sababu masuala haya kama hii ni wizara ni lazima sekta nyengine iweze kukusaidia katika masuala haya lakini sio Wizara ya Afya peke yake, haiwezekani na mimi ninasema kwa uhakika *unless* unashirikiana na sekta nyengine kama tunavyofanya MKUZA I na MKUZA II.

Mhe. Spika, MKUZA I unauona unavyofanywa kwa kushirikiana na sekta mbali mbali. Kwa hivyo Wizara ya Afya ili kuhifadhi afya ya jamii na mazingira yaliyokuwa safi ni lazima ushirikiane na sekta nyengine ili uweze kupiga hatua kwenye mambo haya.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza na mimi kutoa maoni yangu kwenye masuala haya. Mhe. Spika, ahsante sana ninakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo kuhusu hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu umekuja wakati ndio kwa sababu mpaka hivi tunavyozungumza Wazanzibari tumekosa ile hulka au tabia ya kuchukia uchafu, jambo ambalo ni tatizo kubwa kwa afya yetu.

Sasa ninapenda nichukue fursa hii Mhe. Spika, kumpongeza Mhe. Waziri na wataalamu wake kwa kuweza kutuletea mswada huu. Kwa kweli mswada huu ni mkombozi wa Wazanzibari.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya mswada huu kama ukiangalia ni kuweka sheria inayosimamia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii, wakati huo huo kunyanyua kiwango cha afya cha watu ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kama kuna tatizo linalotusibu Wazanzibari ni kushindwa kabisa kuweza kuangalia afya ya mazingira sisi wananchi pamoja na serikali kwa ujumla. Mhe. Spika, ninashangaa sana katika mswada tumezungumzia taka ngumu na taka maji lakini hatukuzungumzia uharibifu wa mazingira ya hewa ambalo nalo ni tatizo kubwa sana. Tumegusa habari ya sigara tu lakini hvi tunavyozungumza kuna baadhi ya nyumba, zimetajwa nyumba za watu binafsi lakini kuna viwanda ni hatarishi kwa afya za watu.

Tumepiga kelele hapa siku nyingi sana lakini serikali imezima masikio Mhe. Spika. Kwa mfano kama kuna sehemu hatarishi ya afya ya mazingira basi ni katika jimbo langu la Wawi kwenye eneo la Kiwanda cha Makonyo.

Kiwanda kile pale Mhe. Spika, kimejengwa kisiasa, hakikujengwa kiuchumi kwa sababu kipo kati kati ya mji. Sisi tulipiga kelele sana kipindi kile kwamba kiwanda kile kijengwe Makaani yaani nje ya mji. Lakini kwa sababu pale kulikuwa na watu wazima waasisi wa nchi hii wenzangu wakaamua kukiweka pale.

Sasa hili ni tatizo Mhe. Spika, na ninashukuru kwamba mswada huu sasa utatoa nafasi kwa sisi Wazanzibari wa nchi hii kuweza kuwashitaki wale wote ambao watashindwa kukiondosha kiwanda kile pale na hatimaye kukiweka pahala ambapo hakitoleta madhara.

Ndio nikasema ni ukombozi kwa sababu Wizara ya Biashara na Viwanda sasa tutakuwa na mamlaka ya kukishitaki ikiwa hawakukihamisha kile kiwanda. Ninaipongeza sana Wizara ya Afya kwa kutuletea huu mswada. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo tunalokumbana nalo kama utakuta kwenye kifungu cha 11 kwenye mswada huu utaona kwamba wajibu wa kusababisha madhara kwa jamii. Kifungu hicho cha 11 kinasema kama mtu au taasisi inayofanya kazi ya uondoaji, usafirishaji na utupaji wa taka kutoka katika jamii au makaazi itahakikisha kwamba njia anayotumia haisababishi madhara yoyote kwa jamii au kwa chanzo cha uenezaji wa maradhi.

Mhe. Spika, kama ukija pale Chake Chake utasjaabu sana Halmashauri, Baraza la Mji la Wilaya ya Chake Chake jinsi linavyochukua taka na kuzipeleka katika maeneo ya kuzitupia taka hizi ni tatizo. Halmashauri au Baraza la Mji wa Chake Chake Mhe. Spika, inatumia kigari cha *canter* kidogo, wanaweka maumbi, nikisema maumbi yaani ni mlundikano mkubwa wa taka, zile taka ngumu zimechanganyika na taka za maji maji wakati mwengine, wanaziondosha pale mjini Chake Chake na kuzipeleka Makaani pwani, huku zikipita katika vijiji zikiwa zinachuruzika katika barabara na mitaa ya miji yetu na kutoa harufu kali sana. (Makofi).
Sasa Mhe. Spika, ndio nikamsifu sana Waziri na watalamu wake kuleta huu mswada, wametukumboa watu wa Chake Chake kwa sababu siku zote pale sisi ikipita gari ya Baraza la Mji basi lazima tutuumwa na vichwa au tutashikwa na matumbo ya kuharisha. Kwa huu mswada ninaamini ni mkombozi kwetu, ahsanteni sana Mhe. Waziri na wataalamu wako.

Mhe. Spika, tatizo jengine tunalolipata ninashukuru mswada huu umeeka maeneo maalum ya kutupia taka na jinsi ya kuyalinda yale maeneo ili yasileta madhara. Mhe. Spika, kama kuna watu waliokuwa na shida, dhiki na madhila basi ni sisi watu wa Vitongoji. Tumeletewa jaa katika Makaani kule ambako kuna makaazi ya wlipata ninashukuru mswada huu umeeka maeneo maalum ya kutupia taka na jinsi ya kuyalinda yale maeneo ili yasileta madhara. Mhe. Spika, kama kuna watu waliokuwa na shida, dhiki na madhila basi ni sisi watu wa Vitongoji. Tumeletewa jaa katika Makaani kule ambako kuna makaazi ya watu, wanakwenda kutupa taka zote za Chake Chake zinaletwa Vitongoji katika eneo la Makaani.

Mhe. Spika, tena zikishatupa pale ndio zimetupwa, manzi yaliopo kule Vitongoji ni wengi sana jambo ambalo wengi wetu hivi sasa tunaumwa na ugonjwa wa macho ya tongo yale, matumbo ya kuharisha kwa sababu manzi yametuzidi. Inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba Baraza la Mji wakishakumwaga zile taka hata hawashirikiani na watu wa afya kwenda kuzifanyia fumigation, jambo ambalo uchafu umezidi katika maeneo yetu.

Sasa mimi ninaamini kwa kuja mswada huu, sisi watu wa Vitongoji tutapata nguvu ya kuweza kulishitaki Baraza la Mji kwa kutaka kutusambazia maradhi. Ndio nikasema awali kwamba mswada huu ni ukombozi.

Halikadhalika Mhe. Spika, jinsi taka ngumu zinavyotupwa Vitongoji kule wanavyoziteketeza wanaziteketeza vibaya sana, kwa sababu huchoma moto siku na siku zinapochomwa moto taka zile kuanzia Vitongoji Kibokoni, Kisiwani, Umangani, Vumba, Vunjabebe mpaka Uwandani hakukatiki kwa harufu mbaya na watu wanaumwa na kichwa kwa harufu ile kali sana.

Sasa Mhe. Spika, kuja kwa mswada huu ninaamini jeuri tunayofanyiwa na Baraza la Mji wa Chake Chake itaondoka na itaku. Inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba Baraza la Mji wakishakumwaga zile taka hata hawashirikiani na watu wa afya kwenda kuzifanyia fumigation, jambo ambalo uchafu umezidi katika maeneo yetu.

Sasa mimi ninaamini kwa kuja mswada huu, sisi watu wa Vitongoji tutapata nguvu ya kuweza kulishitaki Baraza la Mji kwa kutaka kutusambazia maradhi. Ndio nikasema awali kwamba mswada huu ni ukombozi.
Halikadhalika Mhe. Spika, jinsi taka ngumu zinavyotupwa Vitongoji kule wanavyoziteketeza wanaziteketeza vibaya sana, kwa sababu huchoma moto siku na siku zinapochomwa moto taka zile kuanzia Vitongoji Kibokoni, Kisiwani, Umangani, Vumba, Vunjabebe mpaka Uwandani hakukatiki kwa harufu mbaya na watu wanaumwa na kichwa kwa harufu ile kali sana.

Sasa Mhe. Spika, kuja kwa mswada huu ninaamini jeuri tunayofanyiwa na Baraza la Mji wa Chake Chake itaondoka na itakuwa ni ukombozi kwetu sisi watu wa Vitongoji. Kwa hivyo Mhe. Spika, sina sababu ya kutouunga mkono mswada huu.

Mhe. Spika, tuje katika ibara ya sehemu ya nne ya mswada. Sehemu hiyo ya mswada inazungumzia vile vile habari ya majaa ya kutupia taka. Sasa mimi nilikuwa ninashauri Mhe. Spika, kwamba katika kuangalia maeneo ya kutupia taka hizi ni lazima tuone kwamba tunazitupa nje kabisa ya maeneo ya wakaazi, kwa sababu wao watu wa Baraza la Mji wanazitupa katika maeneo ya makaazi na nyengine wanazitupa baharini.

La kusikitisha zaidi ni kwamba taka wanazozichukua Baraza la Mji na kuziingiza katika maeneo ya bahari kule, nyengine zinakuwa ni taka taka za matibabu, yaani kutoka hospitali. Sasa inasikitisha sana kwamba taka taka za hospitali zinatupwa kule zinaingia baharini viumbe vile vya baharini wanakula na tunategemeana na sisi kwa kula ambapo viumbe vitaathirika na sisi tutaathirika. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana katika hili iwe makini sana itakapopita sheria kutiwa saini na Mhe. Rais katika kusimamia hili, kwa sababu hasa Pemba usimamizi yaani sio nzuri wa mambo kama haya.

Mhe. Spika, uvutaji wa sigara katika ibara ya 109. Mhe. Spika, mimi ninadhani sisi ni kisiwa kwa maumbile lakini kwa ulimwengu si kisiwa. Huu ni utandawazi yaani sisi ni sehemu ya dunia.
Mhe. Spika, hivi tunavyozungumza suala la sigara ni tatizo kwetu, watu wanavuta sigara ovyo ovyo. Mimi nilikuwa ninafikiria kwamba samahani nimemtaja hapa Maalim Salim, hizi sigara kungekuwa kama hii sheria ninadhani itasaidia sana.

Mimi sitaki iwe *total prohibited*, *smoking* sitaki iwe total hivyo lakini kuwe na maeneo maalum ya kuvutia sigara. Kwa mfano hapa hili eneo la Chukwani litengewe sehemu karibu na bahari kule, waende wakavute tu sigara lakini wakifika huku wasituvutie tena sigara Mhe. Spika. (*Makofi*).

Halikadhalika Mhe. Spika, katika usimamizi wa sheria hii pindi tutakapoitisha, mimi ninaamini tutaipitisha hii wasimamizi wa sheria hii waende mpaka Gerezani. Mambo ya biashara ya tumbaku lakini imetajwa aina moja ya tumbaku, hawakutaja bangi.

Mhe. Spika, kama kuna matumizi ya tumbaku pahala kunakotumiwa tumbaku mno basi ni jela, tena wanatumia hizi tumbaku hii aina ya pili niliyoitaja ya bangi. Sasa naomba sana katika hili Mhe. Spika, ninawashawishi na Waheshimiwa wenzangu hii sheria tuipitishe ili wale ambao mara nyengine tunaingizwa kule gerezani, basi tunusurike na kupuliziwa bangi kule.

Mhe. Spika, ninadhani sasa nizungumzie hili suala la vilevi. Mhe. Spika, hakuna jambo ambalo lisilokuwa na mapungufu, pamoja na kuiunga mkono sana mswada huu lakini kidogo una mapungufu. Mswada huu umehalalisha mtu kuanzia miaka 19, aliyezidi miaka 18 alewe na auze ulevi.

Mhe. Spika, sheria za nchi lazima ziende sambamba na mila na silka ya Wazanzibari. Hatuwezi kuburuzwa buruzwa tu hivi hivi kienyeji kwa sababu tuna ndugu zetu wa damu wanakuja hapa wanachezea tembo hapo na tusiburuzwe buruzwe. Mhe. Spika, tusikubali na wala tusimuonee haya mtu. Kwa nini sisi tuone haya wakati sisi ni waasisi wa nchi hii tulikuwa hatuoni haya. Kama Muungano umeletwa na waasisi wa nchi hii, kama ni Mapinduzi yameletwa na waasisi wa nchi hii, munaogopa nini serikali kukataza ulevi hapa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Mzee Karume katika miaka sitini na tisa na sabini na sabini na moja, ilikuwa wachilia mbali wa kugema tu, ukikamatwa unagema tu basi utapigwa bakora 24 na kuingia jela miezi 6; 24 ukiingia jela na ukitoka unapigwa tena bakora 24. Ilikuwa total prohibited mambo haya ya ulevi. Sisi tunaona haya nini Mhe. Spika, na kwa nini tuone haya.

Sasa mimi ninadhani nimuombe Mhe. Waziri kifungu hiki bora tukiondoshe. Tutakuwa tumefanya madhambi makubwa sana kama sisi Wawakilishi tutahalalisha tembo humu. Kwa heshima na taadhima namuomba Mhe. Waziri wa Afya na wataalamu wake leo usiku waende wakakae wakakifute kwamba suala la pombe Zanzibar *is total prohibited*.

Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya kufanyiwa marekebisho hayo ninaunga mkono asilimia mia kwa mia huu mswada. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma tunakushukuru na hasa pale ulipochangia kwamba wale wavutaji sigara basi wakavutie upande wa baharini, lakini samaki itakuwa hatuwafanyii haki. Nafikiri Mhe. Hamza Hassan anataka kuchangia karibu.

Inaonekana Mhe. Hamza hayuko tayari basi Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Lakini vile vile nimshukuru pia Mhe. Hamza kwa kunipa nafasi ili nimtangulie.

Mhe. Spika, mswada huu uliowasilishwa leo, kwanza kabisa nilikwenda kwenye madhumuni ya kuwasilishwa kwa mswada huu. Madhumuni makubwa ya mswada huu kama yalivyoelezwa kwamba ni kuweka sheria itakayosimamia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii na wakati huo huo kunyanyua kiwango cha afya ya watu ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu ni mazuri sana, ni mazuri kwa kuwa sasa hivi jamii yetu ndani ya Zanzibar imevamiwa na maradhi mbali mbali, maradhi yatokanayo na vihatarishi vinavyotokana na aina mbali mbali za uchafuzi wa mazingira pamoja na afya.

Mhe. Spika, nafahamu kuwa madhumuni ya mswada huu ni kuweka sheria ambayo itasimamiwa na wizara, ndivyo nilivyofahamu, kwa sababu kuna mamlaka nyingi zenye jukumu hili. Tukiangalia kuna mamlaka nyingi nchi ambazo kila moja ina sehemu yake katika suala hili, lakini tulifika pahala tukaona kwamba kunakuwa hakuna chombo kinachoweza kusimamia kwa ujumla wake suala zima linalohusiana na suala la afya pamoja na mazingira. Kwa hivyo, ni kitu kizuri kuziunganisha taasisi hizi utendaji wake chini ya mwamvuli wa wizara inayohusika na masuala ya afya. Nadhani ndio madhumuni makubwa ya sheria hii.

Mhe. Spika, ni lazima sasa tufike pahala tuwe na sheria ya aina hii, kwa sababu uchumi na chumi nyingi katika dunia huathirika kwa kutumika katika masuala mazima ya kutibu. Bajeti na sehemu kubwa ya fedha za serikali huingia kutumikia suala zima la kutibu maradhi ambayo yanatokana na sababu ambazo si za msingi. Kuna maradhi ambayo tunaweza tukayadhibiti, lakini iwapo tutachukua tahadhari ya kuzuia maambukizi pamoja na suala zima la kutunza mazingira.

Pia ilielezwa kwamba nchi hizi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwamba zitumie zaidi ya asilimia 10 za bajeti yake kwa agizo lile la Abuja, zitumie zaidi ya asilimia 10 ya bajeti yake katika sekta ya afya. Mimi naamini katika asilimia hiyo 10 ambayo ni sehemu ya bajeti ya serikali, laitani kama tungekuwa na sheria madhubuti, basi huenda tukafika pahala sasa tukaanza kupunguza, kwa sababu tutakuwa hatuhitaji tena fedha za ziada kuingia katika bajeti ya afya.

Kwa hivyo, kwa ujumla Mhe. Spika, suala la afya ya jamii tunayoizungumzia hapa ni suala mtambuka, kwa sababu inahusiana na taasisi nyingi za serikali. Tunakumbuka kwamba katika Wizara ya Afya tunayo Idara ya Kinga. Idara ya Kinga sehemu moja kubwa ya kazi yake ni suala zima la kupambana na aina mbali mbali za maradhi. Lakini nakumbuka vile vile tunazo serikali za mitaa, kwa maana ya manispaa, Mabaraza ya Miji na halmashauri. Sehemu kubwa ya utendaji wa kazi za serikali zetu hizi za mitaa ni juu ya kudhibiti afya ya jamii.

Vile vile Mhe. Spika, tuna Idara ya Mazingira, kwa sababu uchafuzi wa mazingira hupelekea kwa sehemu kubwa kuathiri afya za wanajamii. Kwa hivyo, Idara ya Mazingira nayo ni sehemu kubwa ya kushirikisha katika suala hili la afya ya jamii.

Mhe. Spika, tunayo Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na kazi nyengine, lakini kudhibiti ubora wa bidhaa zetu, hasa za utumiaji kama vile vyakula na vitu vyengine.

Mhe. Spika, tunacho kitengo hiki cha dawa za kulevya. Tumeshuhudia kwamba dawa za kulevya nazo kwa sehemu kubwa zinaathiri afya ya jamii. Mhe. Spika, tuna Idara ya Mipango Miji kama ilivyoelezwa ndani ya sheria hii. Idara ya Mipango Miji nayo ni mdau mkubwa katika suala zima la afya ya jamii.

Mhe. Spika, kwa kuwa sehemu kubwa ya kinachotumiwa na wanaadamu ni maji, na sehemu kubwa kuna ile *water bond diseases*, maji tunayokunywa hupelekea kuathiri afya ya jamii. Kwa hivyo, Mamlaka ya Maji ZAWA nayo ni mdau mkubwa sana katika suala la afya ya jamii. Lakini siku hizi kuna NGOs, tunajua kwamba kuna NGO's ambazo zinajikita kwa sehemu kubwa sana kusaidia mambo ya usafi pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo, suala hili la afya ya jamii pamoja na mazingira ni suala la mtambuka na kwa vyovyote vile sheria hii inapaswa iwe na mahusiano au mashirikiano ya moja kwa moja na taasisi hizo ambazo nimezitaja. Sijui ni kwa kiasi gani, lakini kadiri nilivyoipitia sheria hii imegusa tu baadhi ya taasisi, lakini taasisi nyingi humu hazikuguswa moja kwa moja kwenye sheria hii. Sasa sijui mahusiano yake yatakuja vipi, ikiwa tulijua kwamba kuna taasisi ambazo zina umuhimu katika suala hili, lakini sheria zimekaa kimya kuzitambua taasisi hizo.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atueleze, iwapo atakubaliana na mimi kwamba taasisi hizi ni muhimu katika suala zima la afya ya jamii, namuomba aeleze sheria hii ni kwa kiasi gani imezigusa taasisi hizo ambazo nimezitaja.

Mhe. Spika, nimeona katika sheria hii kwamba Mhe. Waziri katajwa katika sehemu nyingi. Katajwa katika kifungu cha 21, 23,24,26,29 na vyenginevyo. Kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba uwepo wa Mhe. Waziri katika vifungu hivi nilivyovitaja, Mhe. Waziri asihusike katika vifungu hivi. Asihusike kwa sababu kazi zilizotajwa katika vifungu hivi kwa kweli zinaweza kufanywa na Afisa ama Mkurugenzi anayehusika katika kadhia hii. Leo haitokuwa vizuri Mhe. Waziri, kwa sababu kwa namna Mhe. Waziri alivyotajwa katika sheria hii, basi atakapoitekeleza tu sheria hii, mimi nadhani katika kipindi chake chote cha uwaziri kwa kweli hataitumikia sheria hii, kwa sababu humu katajwa ana majukumu mengi mno. Sasa mule ambapo yeye atapaswa kuandika katika gazeti la serikali na kusimamia mambo ya msingi kama waziri katika mambo ya sera na mambo mengine ya kisera ni vizuri awepo, lakini katika zile sehemu ambazo pengine ni za kuwaongoza wale wazoaji taka, haiwezekani leo waziri aende moja kwa moja katika kazi kama hizo, ambazo afisa mwengine yeyote anaweza akazifanya. Kwanza ni kumdhalilisha Waziri kwa kweli kuhusika na mimi naamini kwamba kuna watendaji wengi ambao wanaweza kutekeleza majukumu hayo.

Kipengele chengine katika sheria hii Mhe. Waziri kwa kweli kapewa mamlaka ya kuandaa kanuni mbali mbali kama ilivyonakiliwa katika vipengele kadhaa. Ni vizuri na sisi tunaunga mkono kwamba Waziri apewe mamlaka hayo ya kutunga kanuni. Lakini Mhe. Spika, tumekuwa tukilalamika sana kwamba Baraza hili linatoa mamlaka kwa Mhe. Waziri, lakini miaka inapita, utungaji wa kanuni hizo kwa kweli unakuwa ni tatizo. Lakini hata pale kanuni zinapotungwa, kanuni nyengine zinakuwa na nguvu zaidi ya hiyo sheria wenyewe.

Mhe. Spika, tuchukue uzoefu wa wenzetu. Wenzetu katika mabunge mbali mbali sasa hivi wanakuwa na Kamati maalum inayohusiana na kusimamia kanuni, kwa sababu kanuni hizi leo tu natoa mamlaka lakini haiwezekani kanuni kuwa na nguvu zaidi ya sheria. Kwa hivyo, narudia tena ombi Mhe. Spika, kwako kwamba pamoja na kumpa Mhe. Waziri mamlaka ya kutunga kanuni, lakini kama nilivyopendekeza katika vikao vya nyuma na leo napendekeza kwamba Kamati yako ya Katiba na Sheria ipewe jukumu la kuzipitia kanuni hizi, kama ikiwa

hakukuwa na ule ulazima wa kuunda Kamati maalum ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi. Kamati yako ya Katiba na Sheria basi ipewe jukumu hili la kusimamia kanuni mbali mbali zinazotungwa katika wizara zetu.

Mhe. Spika, jengine nililiona katika kifungu cha 68, kuna kitu kinaitwa ugonjwa wa kuambukiza. Na katika tafsiri iliyoelezwa katika mswada huu kwamba ugonjwa wa kuambukiza umetafsiriwa kwamba maradhi yanayosababishwa na vimelea kama vile bacteria, virus, kupe au kuvu, maradhi yanayoweza kusambazwa moja kwa moja au vyenginevyo.

Kwa hivyo, mtu anayepata ugonjwa wa kuambukiza ambaye kama tafsiri inavyosomeka, kazuiwa mtu huyo kumkodisha nyumba, mtu huyo asikodishwe nyumba, mtu huyo katika kifungu kile cha 70(B) katakiwa atakapotembea njiani, atakapokwenda kwenye mahoteli na sehemu nyengine, basi mtu huyo aepukwe kwa mujibu wa sheria ilivyoandikwa hivyo. Sasa kama hivyo ndivyo Mhe. Spika, mimi nadhani turudi katika lile suala la dunia, kwamba haiwezekani kwa sababu tunapozungumza hivi suala la ugonjwa wa kuambukiza na tafsiri yake, maana yake hata wale wenzetu wanaopata ugonjwa wa ukimwi wanaingia katika *category* hii.

Kwa hivyo, kama hivyo ndivyo Mhe. Spika, nadhani sio sahihi kusema kwamba nyumba zao au hairuhusiwi kumkodisha mtu wa aina hii, tukifanya hivi maana yake itakuwa tumeingia katika suala la unyanyapaa kitu ambacho kinapigwa vita na dunia nzima sasa. Sisi Zanzibar tutakuwa ni wa kwanza kuleta sheria kama hii. Kwa hivyo, kama hivyo ndivyo, naomba sheria hii tuiangalie vizuri, ili tusionekane kwamba leo tunatunga sheria zenye kunyanyapaa, wakati sisi ndio wa kwanza kusema kwamba suala la unyanyapaa halifai, kwa hivyo tusilitungie sheria suala hili.

Mhe. Spika, jengine ni suala la udhibiti wa bidhaa za tumbaku. Kwanza niipongeze serikali kwa kuliona suala hili. Nililiuliza katika suala la msingi mwaka jana nadhani, na Mhe. Waziri akaahidi kwamba atalichukulia hatua, kwa hivyo nipongeze kwamba kaliona.

Lakini na mimi niungane na Mhe. Saleh Nassor kwamba adhabu iliyotolewa hapa haitoshelezi kabisa, kuandika tu bidhaa za tumbaku yaani kuandika onyo, kwa kweli haisaidii kitu au ni marufuku kuvuta. Maana yake imeandikwa katika kifungu cha 109 kwamba ni marufuku kuvuta au kushikilia sigara iliyochomwa katika eneo lisilo la wazi au sehemu ya umma. Mhe. Spika, mimi hili nalipinga, nalipinga tena nitalipinga kwa nguvu zangu zote. Wavutaji wa sigara wasiruhusiwe kuvuta sigara au kushikilia sigara sehemu zenye hata watu wawili wasiruhusiwe kabisa, ile ni starehe na mtu mwenyewe anajua wakati gani wa kufanya starehe, suala la starehe anajua wakati wa kufanya starehe.

Mhe. Spika, sasa hivi Mwakilishi wako yeyote akishikwa na kileo anajua, anajua kileo tayari. Kwa hivyo, kukimbia akenda kukaa nyuma kule nadhani hilo halisumbui, kulikoni kutusubiri watu watatu hapo nje na yeye ukamuona kajiweka katikati anavuta sigara hilo haliwezekani. Kwa hivyo, mimi nadhani na wala suala hili sio tatizo. Suala la uvutaji wa sigara kwenye mkusanyiko hata wa watu wawili iwe ni *strictly prohibited.* Kwa hili Mhe. Waziri naomba uliangalie sana, kwa sababu mvutaji wa sigara mbali ya kuathiri, wataalamu wanatuambia kwamba ni sehemu ndogo sana anayojiathiri yeye kama wale waliomzunguka. Wale waliomzunguka wanaathirika zaidi kulikoni hata yeye mwenyewe. Wenzetu hawa kwa kweli wakishashikwa na kileo hawaoni wala hawasikii, popote wao huvuta tu, kwenye maboti huvuta na kila sehemu. Sasa suala hili linaleta kero na athari mbaya sana kwa jamii.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba kipengele hiki ukirekebishe ili iwe kuvuta sigara kwenye mkusanyiko hata wa watu wawili tu, yaani yeye na mwenziwe iwe ni *prohibited* hatulitaki suala hili. Kama ataandikiwa onyo au hatoandikiwa onyo ni hiyari yake mwenyewe.

Mhe. Spika, nije kwenye baraza la ushauri wa afya ya jamii na mazingira. Katika kifungu cha 128 kwenye sheria imetaja Baraza la ushauri wa afya na imetaja wajumbe, lakini wajumbe waliotajwa katika baraza hili nirudie katika ile lugha yangu niliyozungumza kwamba haikujumuisha watu wanaotoka katika zile sekta ambazo ni muhimu katika masuala ya afya, ni baadhi yao tu. Ingekuwa ni vizuri zaidi wajumbe hawa wakatoka moja kwa moja kwenye taasisi hizi, tena hapa naomba nishauri kitu kimoja.

Tumekuwa na uzoefu mara nyingi vyombo hivi vinapoundwa huchukuliwa maafisa kwa nyadhifa zao, kwamba maafisa wataingia kwa nyadhifa zao, huchukuliwa watu wa kawaida tu. Sasa unapomchukua mtu wa kawaida katika taasisi yangu wakati mimi ni bosi pale nipo, sheria zetu nyingi Mhe. Spika, hazitekelezeki kutokana na tatizo hili. Ni vyema katika chombo hiki au katika vyombo kama hivi tukawaweka watu ambao wana mamlaka ya kutekeleza yale

yaliyoamuliwa katika kikao, imethibitika kwamba watu kama hawa wakiteuliwa kuingia katika mamlaka hizi, wakati wanaporudi sasa kutekeleza katika taasisi zao kuna wakubwa zaidi.

Mathalan katika taasisi fulani kuna Mkurugenzi ukampeleka tu afisa wa kawaida, mara nyingi Mkurugenzi hafuati maagizo yaliyotolewa na huyu afisa wake wa chini. Kwa hivyo, Mhe. Spika, napendekeza kwamba katika watu ambao wameteuliwa, basi napendekeza Idara ya Afya Mkurugenzi wa Afya aingie kwa nafasi yake. Vile vile serikali ya mitaa na kwa sababu sehemu kubwa ya afya ya jamii iko kwenye serikali za mitaa, kumchukua afisa mmoja tu kwenye manispaa, tukumbuke kwamba tuna na halmashauri na halmashauri nazo zina kazi kubwa. Lakini vile vile na Mabaraza ya Miji yaliyoko Pemba nayo yana kazi kubwa, sasa ikiwa hayakupata mwakilishi ni tatizo. Pia ni ukweli kwamba hatuwezi kuwachukua wawakilishi katika halmashauri na mabaraza yote tukayawaingiza.

Kwa hivyo, katika nafasi hii mimi napendekeza kwamba Mkurugenzi anayehusiana na Serikali za Mitaa katika Ofisi ya Rais aingie kwa nafasi yake. Mkurugenzi atakapoingia pale atakuwa na uwezo sasa wa kuziamrisha mamlaka zote zilizoko chini yake. Kwa hivyo, hilo ni pendekezo. Lakini vile vile tuangalie, kadiri kama nafasi itakuwepo basi tuangalie na taasisi nyengine zilizokuwa zinahusu moja kwa moja katika suala hili kama nilivyoeleza mwanzo kwamba suala hili ni suala mtambuka ambalo linagusa taasisi nyingi sana tulizonazo.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba niseme kwamba mimi siamini kuwa sheria hii, tumuombe Mwenyezi Mungu tuitekeleze, lakini tatizo hasa tulilonalo sio sheria. Laitani kama sheria tulizonazo hivi sasa tunazifanyia kazi na tunazisimamia basi kungekuwa na haja ndogo sana ya kuwepo kwa sheria hii. Lakini tunazo sheria, na taasisi zote hizi nilizozitaja zina sheria, na zote kila moja kwa nafasi yake kwa kweli ina nafasi ya kuisimamia afya ya jamii. Lakini leo tujiulize ni taasisi gani iliyoitekeleza sheria kama ilivyo katika taasisi yake, hakuna. Kwa hivyo, hata kuwepo kwa sheria hii, mimi kwa tafsiri yangu ni kuwatafutia watu kijio tu, ni kutafuta nafasi wakaja watu wakaajiriwa au wengine wakawachagua, lakini hakuna kitu ikiwa hatutoweza kuzisimamia. Suala hili natoa wito kwa serikali kwamba tujenge utamaduni wa kuzisimamia na kuzitekeleza sheria zetu, vyenginevyo kila siku Baraza hili la Wawakilishi na kwa sababu ndio kazi yetu, sisi hatuchoki.

Mhe. Spika, kadiri utakavyoletwa mswada, madam ni kazi yetu sisi tutapitisha tu, lakini tutapitisha vitu vilivyokuwa havitekelezwi, mwisho wake tutakuja kupitisha sheria ambayo tumeshaipitisha hapa, mimi nahofia hiyo, kwamba kuna siku tutakuja kupitisha sheria ambayo tayari tumeshaipitisha, hatujui na kwa sababu sheria haina utekelezaji na ili sheria ujuwe kama ipo ni lazima sheria ile itekelezwe ndio utajua kama sheria ipo.

Kwa hivyo, mwisho kabisa naiomba serikali ilifanyie kazi suala zima la kuzisimamia sheria tunazozipitisha katika Baraza letu hili. Kama hata sio kusimamia basi ifike pahala iseme tu, iende kwenye vyombo vya habari, jamani eeh, tukumbushe tu kwamba tuna sheria nambari fulani ya mwaka fulani, na tuna sheria fulani ya mwaka fulani. Hivyo tu inatosha kutukumbusha kwamba sheria hii ipo. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba sisi mtakapotuletea sheria, madam ni kazi yetu tutapitisha sheria, lakini ni kazi ya serikali kuhakikisha kwamba sheria zote tunazozipitisha zinafanyiwa kazi. Vyenginevyo vyovyote Mhe. Spika, tutakuwa tunafuja pesa bure za umma, pesa ambazo zina kazi nyingi sana za kuwasaidia wananchi wetu wanyonge walioko majimboni kwetu. Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikatoa mchango japo mdogo katika mswada huu uliosheheni maelekezo mengi, utekelezaji mwingi nadhani tukiwa makini Mhe. Spika, mswada huu utatusaidia sana katika kuziimarisha afya zetu. Vile vile kuipunguzia mzigo serikali wa kununua dawa kila siku kwa ajili ya kututibu.

Mhe. Spika, nataka nianze kwa yale aliyomalizia Mjumbe mwenzangu aliyepita. Mhe. Spika, mswada huu kama tukiusoma vizuri, kwa kweli hakuna sababu ya malalamiko ya kwamba labda kuna maeneo yetu pengine machafu, labda kuna mtu kafanya mambo ya makuruhu kwenye gari, kuna watu wamefanya biashara kiholela ambazo pengine zimepigwa marufuku. Kwa hivyo, kimsingi mswada huu umejaa muongozo wa sheria mbali mbali.

Mhe. Spika, sitaki kurejea ile kauli yangu ya kwamba tunatunga sheria nyingi nzuri, kwa sababu jambo ukishalisema kwa hivyo, ina maana inabakia utekelezaji. Lakini nataka niseme watu wetu wengi hapa Zanzibar nataka niseme sheria zetu nyingi hawazijui, wengi kabisa na ukifuatilia utakuta sheria hizi za nchi ambazo tunazitunga sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi basi hawazijui.

Kwa hivyo, nadhani sasa wakati umefika. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kila siku zinavyokwenda tunajaribu kuangalia Baraza letu lina mapungufu gani, tufanye nini tujifunze kwa wenzetu ili Baraza letu liweze kufanyakazi nzuri itakayoleta tija kwa jamii. Mhe. Spika, wenzetu Zambia ambapo na wewe mwenyewe Mhe. Spika, ni shahidi, uliongoza timu yako ya Kamati ya Wenyeviti tukaenda kujifunza kwa wenzetu ni namna gani wanavyopitisha miswada yao ya sheria.

Mhe. Spika, tumegundua kwamba kila tunavyotembea kwa wenzetu kwamba iko haja ya kwenda kujifunza zaidi. Wenzetu wanapiga hatua, sisi tunasema maneno, lakini wenzetu kwa kweli Mhe. Spika, wanapiga hatua na kwa nini tukasema wanapiga hatua. Ni kufuata tu sheria zao walizotunga, wakazisimamia na wananchi wakazitekeleza basi hakuna suala jengine.

Mhe. Spika, nini tulichojifunza Zambia, wenzetu sasa hivi miswada kama hii wameanzisha utaratibu wa *Public Hearing*. Leo kwa bahati nzuri asubuhi kipindi cha TVZ aliitwa Katibu wetu wa Baraza, akaambiwa bwana hatutaki kuwasikia Waheshimiwa Wawakilishi wanatohoa maneno ya Kiingereza ndani ya Baraza la Wawakilishi. Sasa tunaposema *Public Hearing* tumelitohoa neno la watu, lakini nakusudia kwamba miswada yoyote ya serikali na kwa bahati nzuri sasa hivi tumeanzisha utaratibu mzuri, miswada ya kikao kinachokuja inaanza kutangazwa mapema kama *first reading*.

Kwa hivyo, ina maana wakati ule mswada ukishatoka unatakiwa ukabandikwe kwenye maeneo mbali mbali na Baraza litoe matangazo mbali mbali kwamba mswada wa sheria fulani utakuja katika kikao fulani. Kwa hivyo, wananchi wapite wakauangalie wausome na waulize maswali na Kamati zako ziwe huru kwenda kwa wananchi ili wakawasomee miswada ile, wawatafsirie miswada ile na kama wananchi wana maswali basi waulize. Nadhani hii itaweza kuwasaidia wananchi wetu angalau kujua hizi sheria tunazotunga hapa Barazani.

Mhe. Spika, leo ukiuangalia mswada huu muna sheria nyingi humu zimo katika taasisi mbali mbali. Lakini je, tujiulize ni kwa kiasi gani tumeweza kuzitekeleza sheria ambazo leo tuna *review*, tunampa jukumu Mhe. Waziri wa Afya kusimamia sheria hizi zote, kwa sababu pengine katika utekelezaji wa shughuli zao wanaona kuna ugumu, na ugumu wenyewe unatokana kwamba labda anahisi labda pengine sheria hii ina matatizo.

Mimi nadhani sasa hivi wakati umefika na mimi nataka nitoe wito hasa kwa wafanyakazi wa serikali, kwa sababu kila mtu amekabidhiwa jukumu lake katika wizara yake. Sheria hizi tunazozitunga kama hazitekelezwi basi matokeo yake siku zote tutakuja hapa tunailaumu serikali. Kwa bahati nzuri humu haingii Mkurugenzi, wala haingii Katibu Mkuu, humu wanaoingia ni Mawaziri. Kwa hivyo sisi itakuwa siku zote hapa ni kuwasulubu mawaziri kwa makosa ya watendaji wao huku chini.

Kwa hivyo, mimi nitamuomba sana kiongozi wetu wa shughuli za serikali, kama kuwastahamilia watu umeshawastahamilia sana, kama kuwavumilia umeshawavumilia sana. Sasa hivi tumemuona Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anachukua mfano kama alioufanya Mhe. Rais Kikwete. Mhe. Rais Kikwete alipoingia madarakani alikuwa na semina za watendaji, kuanzia Wakuuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi na wengineo. Aliwaweka Ngurudoto kule nakumbuka katika kipindi cha mwanzo kabisa, akawapiga msasa na kwa nini akafanya vile, kwa sababu kwa bahati nzuri Mhe. Rais wetu alikuwa Mwakilishi na Mhe. Rais Kikwete alikuwa Mbunge. Kwa hivyo, yeye alikuwa ni mmoja katika anayejua udhaifu au ubora wa utendaji wa wafanyakazi wetu.

Sasa mimi nadhani viongozi wanapokuwa wanazungumza lugha kila siku hizo hizo, ina maana, sitaki kusema, lakini ina maana wanakuwa hawaridhiki. Maana yake leo mtu keshasema suala hilo hilo, kesho analisema tena suala hilo hilo na keshokutwa analisema suala hilo hilo. Mimi nafikiri wakati wa maneno umekwisha, hebu twendeni kwa vitendo.

Mhe. Spika, jengine ulitupeleka China. Tunaishukuru serikali yetu imetupeleka China na tumekwenda kujifunza. Hebu tujiulize tangu kurudi China ni nini ambacho tumeanza kuki-*practice*. Ni juzi tu katika sherehe ya maadhimisho ya miaka sijui mingapi ya China kwenye sherehe zao za uhuru, Balozi wa China kazungumza na hata leo gazeti la Zanzibar Leo nimesoma, wanasema mafanikio makubwa waliyoyapata China na hata sisi kule tuliwauliza, hebu tuambieni kuna changamoto gani mlizokabiliana nazo na mmeweza kuzikabili na kuweza kuzichukulia hatua mkazivuka mpaka leo China imekuwa ni nchi ya kupigiwa mfano.

Wakatuambia ni mambo mawili tu wala hakuna jengine. Ni kujituma zaidi, sio kujituma. Ni kujituma zaidi na uwajibikaji. Wenzetu China unapokabidhiwa majukumu yakikushinda basi wewe tena huulizi swali, unawajibika tu.

Kwa mfano, tumewaona mabingwa China na wataalamu wakubwa pamoja na wazalishaji wakubwa wametengeneza bidhaa imeua wanadamu basi na yeye shingo hana, na watu watapiga kelele kwamba hakuna Haki za Binadamu. Lakini mtu hayupo kwa sababu yeye ameua na yeye amekwenda.

Sasa sisi hatutaki tunyonge au tuue mtu aa! Kwa hivyo, tunataka mtu anapopewa sheria ambayo inasema kila kitu, lakini unakuta mambo yanarudi yale yale. Mhe. Spika, nafikiri tukianza kuchukua hatua kwa mtu mmoja, wawili, watatu basi wa nne na wa tano na sita hawatorejea makosa yale.

Mhe. Spika, naomba hizi sheria nzuri tunazozitunga basi hebu tuwasaidie wenzetu kuweza kuzisimamia vizuri na mimi naamini tutaweza kufanikiwa, vyenginevyo kila siku tutakuwa tunakwenda kujifunza lakini tunarudi hapa na mambo yanakuwa ni yale yale.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niingie kwenye mswada wenyewe. Mhe. Spika, sheria yenyewe inasema kusimamia afya ya jamii, mazingira na mambo mengine mbali mbali. Sasa katika sheria hii kuna mambo tofauti ambayo yameelezwa kama vile kulinda jamii na vihatarishi vya jamii, pia yamezungumzwa mambo mbali mbali kuhusu suala la uvutaji ovyo wa sigara, pengine utupaji taka ovyo.

Lakini mimi nataka nizungumze jengine ambalo nimejifunza katika masuala ya usafi. Mhe. Spika, mimi nilibahatika kwenda Rwanda *special* kwa ajili ya kujifunza mambo ya usafi.

Mhe. Spika, wenzetu utaratibu wao wanavyofanya kule Baraza la Manispaa kila siku ya Alkhamis kuna basi maalum wanapanda Maafisa wa Baraza la Manispaa, ambapo katika Baraza la Manispaa kuna Afisa wa Afya na ninapozungumza Baraza la Manispaa nachukulia mpaka na Halmashauri kwamba kuna Maafisa wa Afya, Maafisa wa Mazingira, Usafi wa Taka, Mipango Miji na mambo mbali mbali.

Baraza la Manispaa au Halmashauri wanatoa maelekezo katika wale watu ambao wako chini yao. Kwa mfano, wafanyabiashara, watu wa masokoni, wenye maduka, wenye vituo vya petroli na kutoa *conditions* zao na wenzetu kule hawatumii nguvu nyingi kwa kutumia nyenzo nyingi za serikali, kwa sababu wao kazi yao ni kutoa maelekezo tu.

Kwa mfano, umejenga Kituo cha Petroli Maafisa wa Mipango Miji wanakuja pale na kukupa maelekezo na kukwambia umeshatengeneza *Petrol Station* tunataka hapa uweke *garden*, wanakuja na wataalamu wao na kukusaidia utaalamu wa kuweka ile bustani pia wanakupa masharti yao kama mfano hapa imefunguliwa *Petrol Station* tukitoka *Airport* pale.

Sasa kama pale kabla hajaanza kazi wanakwenda na kuanza kumpa masharti, kwamba tunataka kwa kuwa *Petrol Station* yako iko karibu na barabara basi tunataka uweke vibaraza, bustani pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, ina maana wale baada ya kutoa maelekezo kiasi ya wiki moja kuna wale maafisa niliosema kama wanane wanapanda kwenye basi na kwenda kukagua yale maeneo waliyotoa maelekezo je yametekelezwa vipi.

Mhe. Spika, wenzetu kule hawana mjomba na wala hakuna muhali kule, yaani yale masharti waliyokupa umeyatekeleza sawa na ikiwa hujayatekeleza kufuli wanakuzuia tu na wakeshakukuzuia utafanya nini. Kwa hiyo, Mhe. Spika utakuta kwa sababu gani ni usimamizi, sheria tayari zipo na unapokwenda kuomba kibali pengine cha kujenga *Petrol Station* au Soko kila kitu kipo, sasa unaposhindwa kutekeleza yale basi wanakuchukulia hatua.

Jengine mfano kuna gereji ambazo ziko maeneo ya mjini ambazo zinafanya *pollution*, utakuta vyombo kama vile vespa, magari wanapiga *kick* na kutoa moshi na kupelekea kuharibu mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa wenzetu Rwanda hulikuti gereji mjini, lakini leo gereji ziko katikati ya miji na watu wanajaribu magari kuna wagonjwa, moshi mwingi, *oil* chafu na vitu mbali mbali. Sasa leo kuna watu wanatengeneza gari barabarani, gari zinalazwa barabarani na sheria zipo. Lakini je, nani anayechukua hatua. Kwa hivyo, mimi nadhani haya yote yanakuja na suala zima la uwajibikaji.

Mhe. Spika, nataka nichukue hii sehemu ya tatu ya mswada inayosema usafi wa makaazi. Mhe. Spika, ukienda Baraza la Manispaa au katika Halmashauri zetu, kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambapo katika kusimamia ni pamoja na kusimamia Ofisi ya Rais inayoshughulikia mambo ya Tawala za Mikoa, kwa hiyo halmashauri hizi ziko chini yetu.

Mhe. Spika, ukienda kule wanazo sheria nzuri sana, yaani sheria zetu za Baraza la Manispaa hivi sasa nyumba yako mwenyewe ikija ikikutikana na Afisa wa Manispaa imezungukwa na uchafu hujasafisha, basi kwa mujibu wa Sheria za Manispaa unachukuliwa hatua na kufunguliwa mashtaka na kupigwa faini shilingi 200,000/= na miezi sita.

Sasa kweli kama hizi sheria ingekuwa maafisa wetu wanazisimamia, hivi leo kuna nyumba ambayo ungekwenda na kukuta imezungukwa na uchafu, hakuna, lakini na hapa katika mswada huu unasema usafi wa maakazi wakati huku sheria tayari zipo na hapa leo tunatengeneza sheria nyengine.

Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri wa Afya na kusimamia suala la usafi ni mambo ambayo ni mtambuka kama walivyosema wenzangu, kwamba kunahitajika mashirikiano makubwa. Wizara ya Afya watatoa elimu kwa ajili ya masuala ya afya, Baraza la Manispaa na Halmashauri wao watatekeleza, kwa sababu wao ndio wenye nyenzo za kufanyia hizo kazi. Mhe. Spika, mimi naomba sheria hizi ziweze kufuatwa.

Jambo jengine katika suala zima la uhatarishi wa usalama wa afya za majirani katika mitaa, na wenzangu wamezungumza panya na mambo mengine, mimi nataka nizungumze kitu ambacho utakiona ni kidogo lakini ni kikubwa. Kwa mfano, leo nyumba zetu katika maeneo ya mjini bado mpaka leo watu wanashindwa kuchimba karo kwa ajili ya maji machafu, mtu anafanya uchafu wake ndani na maji anayatoa nje na watu asubuhi wanapita wanakimbilia kazini kiatu kimeingia pale nguo yote imechafuka. *(Makofi)*

Lakini ukienda Baraza la Manispaa wanayo Sheria ya Udhibiti wa Maji Machafu kama haya, sasa je wale maafisa wa Manispaa au Halmashauri wako wapi, wanafanya ufuatiliaji katika haya maeneo. Mhe. Spika, mimi nadhani haya ndio miongoni mwa mambo ambayo yanaambukiza na tunaishukuru sana serikali yetu kupitia Wizara ya Afya tumepiga sana vita malaria.
Mhe. Spika, hivi sasa Zanzibar katika nchi ambazo zinapigiwa sifa duniani kwa kutokomeza malaria Wizara ya Afya. Sasa je, tukiendelea kuacha ile mitaro ovyo na maji yale yanakwenda kutuama sehemu.

Mhe. Spika, jirani yangu hivi karibuni alipita punda, unajua maeneo yetu huko Kwamtipura, amepita punda nyuma na kuingia kwenye karo, yaani punda miguu ya nyuma yote iko kwenye karo, miguu ya mbele na shingo ndio iko juu, tunashukuru wasamaria wema vijana pale wakaenda kumkamata masikio punda yule na wala hakulia hata kidogo. Kwa kweli katika kiungo kinachouma kwa binadamu au mnyama yoyote ni sikio basi *Wallahi* punda amevutwa masikio na amenyamaza kimya, nikasema ama kweli kufa.

Sasa hii imetokana na nini, ni karo mtu amechimba hajalifunika na punda amepita ameingia. Lakini nashukuru na ananisikia hivi sasa tena nampongeza baada ya punda yule kutolewa juzi tumepita karo lile amelitengeneza vizuri hivi sasa na punda wakipita hawaingii na leo ameingia punda. *(Makofi)*

Je, angeingia mtoto pale na watoto wetu tunawajua kwamba wanacheza na kufukuzana, wanacheza foliti kama angeingia mtoto ina maana ndio angekuwa ameshakufa, kwa sababu masikio ya punda marefu ndio ameweza kukamatwa na kuvutwa masikio, ya mtoto yangepatikana? Kwa hivyo, haya ni mambo ambayo Mhe. Spika ni mambo ya kuchekesha kidogo, lakini yana mantiki. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, hii nakusudia wananchi wetu na kwa bahati nzuri hivi sasa wananchi wetu ukiacha ile niliyoishauri *Public Hearing*, hii Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kutoa matangazo ya Baraza la Wawakilishi *live*, basi hii peke yake ni *Public Hearing* na hapa tunapitisha sheria kwa hiyo tunawaomba wananchi wetu kwamba kutupa taka ovyo katika maeneo yetu ni kosa, kuacha michirizi ya maji machafu ni kosa na ndio sheria hii tunaitunga.

Vile vile tumeshamwambia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hivi sasa asimfumbie mtu macho. Kwa hivyo, leo kama wananchi wataendelea kuchafua ina maana wanamhatarishia kazi yake yule aliyepewa majukumu kule. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, mimi ninaomba kwamba hawa watendaji ni wenzetu, ndugu zetu na tuwaonee huruma na wa kuwaonea huruma ni sisi wananchi.

Mhe. Spika, sisi kama itatokea miripuko ya maradhi basi watakaoathirika ni sisi, ina maana tukifanya uchafu tutakaoathirika ni sisi. Kwa hiyo, mimi nawaomba wananchi wajitahidi suala hili waweze kujisaidia.
Pia nilikuwa na ombi Mhe. Spika, kwa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tunaomba sana kwamba serikali imeanzisha utaratibu mzuri wa *Public Private Partnership* tukiweza kuitekeleza hii kwa vitendo, basi Mhe. Spika suala la kupiga kelele mji mchafu litakuwa halipo.

Kwa kuwa sheria zipo Baraza la Manispaa na Halmashauri katika Kanuni pamoja na Sheria zao ndogo walizozitunga wametoa ruhusa ya kuweza kukusanya ada pale Afisa wa Afya au Taka anapokuja kufanya usafi. Hivi sasa Mhe. Spika, mji wetu umeongezeka na serikali uwezo wa kusema kila siku iendelee kuajiri watu kwa ajili ya usafi uwezo huo hauna.

Mhe. Spika, tunaomba na hivi sasa tunashukuru kupitia Polisi Jamii wananchi wetu wengi wamejiunga katika vikundi vya usafi kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, Mhe. Spika naomba hizi kazi wapewe wananchi wetu, yaani wapewe maeneo *block* zile, na waambiwe eneo lenu ni kutoka hapa mpaka kule waweze kufanya kazi, kwa sababu naamini wananchi wakiruhusiwa kukusanya ada wao wenyewe nyumba kwa nyumba, basi nadhani hii kazi ya kupiga kelele Manispaa au Halmashauri itakuwa imeondoka. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kazi yetu Wawakilishi na Madiwani wetu kujilaumu kwa nini wananchi wetu ile kazi ya kukusanya taka na kuweza angalau kukusanya ada imewashinda na itakuwa sasa badala ya kuwanyooshea vidole Mabaraza ya Manispaa au Halmashauri, itabidi sasa sisi wenyewe tujinyooshee vidole. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi naomba wananchi wangu wa Saateni, Shehia ya Shaurimoyo, na mimi ninavyo vikundi vitatu katika jimbo langu. Ninacho Kikundi cha Usafi na Mazingira ya Mkele, nashukuru Baraza la Manispaa wamekuja na kutusaidia mabero na *gloves* tunawashukuru sana.

Kikundi cha Shaurimoyo pia tunashukuru mumetuletea *gloves* pamoja na mabero, isipokuwa hamkutuletea tu kwa utashi wenu baada ya kuona jitihada yetu tunavyofanya kazi ya usafi wa mazingira na Kwamtipura tunacho Kikundi chengine cha Usafi, tunashukuru kwa misaada midogo midogo tunayoipata.

Kikundi cha Shaurimoyo baada ya kuona wananchi wetu wanafanya kazi kwa ujasiri, watu wanachafua na wao wanakwenda wanasafisha na taka wanaziweka mahala pazuri, na Manispaa tunashukuru hivyo hivyo magari tabu, tunashukuru tunasikia magari kuna *tender* imeshatolewa nadhani kama hayajafika basi karibu yatafika, na tunaamini kwamba magari yatakuwepo ya kutosha na taka zitakuwa hazikai kwa muda mrefu.

Sasa tuliliomba lile Soko la Saateni pale Mhe. Spika, katika masoko ambayo nataka nikwambie ambayo yanayoongoza kwa usafi hivi sasa hapa mjini basi ni Soko la Saateni, kwa sababu gani. Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura Shehia ya Shaurimoyo wameona kwamba watu wametoka huko wamekuja kuletewa soko, na halafu lile soko limekuwa chafu na kwa kuwa wananchi wa Kwamtipura ni watu wasafi, basi wameona bora waamue wakalisafishe wao.

Mhe. Spika, ukienda pale utadhani Rwanda, na kwa bahati nzuri tumekwenda na Mkurugenzi wa Manispaa tunamshukuru sana ametupa changamoto nzuri, najua ananisikia huko na ile ahadi aliyoitoa kwa wale wananchi wa Shehia ya Shaurimoyo katika usafi wa soko lile, basi tunamuomba aikamilishe kwa vitendo na tayari ameshaanza kuitekeleza.

Vile vile na mimi namuahidi kama soko lilivyo safi na wananchi wangu wale wako tayari na wataendelea kusafisha soko lile, lakini bado tunaomba yale maandishi ya makubaliano, kwa sababu kuna baadhi ya mambo lazima tuandikiane mikataba na Baraza la Manispaa, ili wale wawe wanafanya kazi kisheria zaidi kuliko hivi sasa kiutashi zaidi, kwa sababu lile ni eneo la watu la wafanyabiashara.

Sasa wakati wafanyabiashara wanapofanya kazi huwezi kwenda na ukamwambia ondoa meza yako hivi sasa nataka kusafisha, au mbona leo hapa tumekupa masharti uweke hivi na wewe umeweka vyengine.

Mhe. Spika, tunaomba ili kuitekeleza vizuri hii sheria ndio maana tumesema kwamba tunataka tufanye ile *PPP*, serikali ifanye taratibu zake ambapo tayari imeshatunga sheria, basi na wananchi wapewe kazi ya kuendeleza hii kazi iliyofanywa na wananchi. Nadhani Mhe. Waziri ananisikia na ninaamini na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa bila ya shaka na yeye ananisikia.

Jambo jengine kuna eneo ambalo kila siku Waheshimiwa Wajumbe wanapiga kelele, na kwa bahati mbaya na mimi nilipita pale na iliingia harufu kwenye gari yangu na kidogo sikufurahi vizuri kuhusu Soko la Darajani.

Kwa kweli mimi nadhani pale tuweke mkakati maalum hivi sasa, maana yake pale unajua taka za Darajani zote za kunuka kama vile mbatata, matumbo ya samaki, madengu, badia unajua mambo ya Mji Mkongwe kule unajua vile vitu rojo zote zinazotupwa pale zikiingia pale na watu wa Mji Mkongwe hawali mihogo kama kwetu Kwamtipura, lakini watu wa Mji Mkongwe rojorojo tu wanachanganya, kwa hiyo mbatata inakuwa harufu tupu na pale ndio kioo chetu cha mji.

Mhe. Spika, naomba hebu tungejaribu kuweka *conditions*, unajua nchi za wenzetu tunapotembea huko hivi sasa Zanzibar tumepiga marufuku mifuko ya *plastic*, lakini wenzetu kule kwa kuwa wao wananchi wao wanajua sheria za nchi pia wanajua hichi tukikifanya hivi kitaleta athari ya mazingira na hivi na vile. Kwa hivyo, utaona wanatia taka ndani ya nyumba utakuta taka kuna mifuko ya aina tatu kuna taka nyepesi, ngumu na nyengine zinazooza.

Kutokana na hali hiyo, utakuta mtu anakwenda kutupa taka amebeba mifuko yake mitatu anakwenda kuweka kwenye kituo pale, hivyo Manispaa wakija sio anachukua fyagio kusafisha isipokuwa yeye anakuja kuchukua ile mifuko yake na kuitia kwenye gari na kuondoka.

Sasa naomba itolewe elimu maalum kwa wale wanaouza samaki pale marikiti, maana yake zile harufu zote matumbo ya samaki yakichanganyika na mbatata ndani ya masaa mawili basi lazima harufu itatoka, basi wapewe elimu maalum na waekewe chombo pale cha *plastic* ambapo yale matumbo yao ya samaki yote wayatie kwenye sehemu maalum, kila baada ya muda fulani yawe yanakuja kuchukuliwa na kuondolewa.

Mhe. Spika, vyenginevyo kila siku tutakuwa tunazungumza lugha hiyo hiyo na pale kweli panakuwa na harufu mbaya sana, na sijui wale wafanyabiashara watu wa *taxi* pale na wengine sijui wanakaa vipi, maana yake mtu unapita dakika moja tu unakuja harufu. Kwa hivyo, mimi nadhani wangeandaa utaratibu maalum kwa ajili ya kuweka usafi.

Vile vile kuna maeneo haya katika masuala mazima ya kuweka afya ya jamii na mambo ya maambukizi kuhusu lile suala la maeneo ya kuzikia, na katika kuzika kuna tafsiri ya kufukia au kuchoma. Kwa kweli ni vizuri kuweka masharti maalum unajua wakati mwengine yanapotokea maradhi ya mripuko huwezi tu mtu kwamba una maiti wako unalia sana unamuonea uchungu na kuzika tu, kwa sababu unaweza kuzika na baada ya siku tatu na wewe ukazikwa, kwa sababu kuna maradhi haya ya maambukizi.

Kwa hivyo, sheria itatusaidia kwamba watu na kwa sababu tuna utamaduni, unajua kawaida mtu anapofariki anatakiwa lazima apelekwe hospitali apimwe, ili ijulikane amekufa kwa maradhi kama amefariki nyumbani. Lakini tunajua utamaduni wetu wewe Matemwe huko unafikiri mtu atatoka ndani maweni huko ambebe ampeleke Kivunge kule, sasa wakati mwengine huwa wanazika huko huko. Mhe. Spika, vizuri sheria hii kwa kuwa imeeleza hivi kwa ajili ya kupata utaratibu mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sheria hii imesema kwamba kuna ruhusa ya maeneo ya kuzikia, kwa sababu hivi sasa kuna tatizo. Kwa mfano, unaweza kutoka Jumapili unakwenda kondeni na kukuta kaburi na watu wanajizikia tu, unakuja kaburi mtu shamba si lake na yeye amezika tu. Sasa sheria hii imeeleza vizuri kuna maeneo ambayo yatakuwa yanawekwa kwa ajili ya kuzikia, na pia kuna na marufuku ya kuacha kuzikia.

Kwa kweli hivi sasa kuna eneo moja ambalo tayari tumeshalizungumza sana Mwanakwerekwe basi tena kuzikiwa, kwa sababu eneo lile hivi sasa watu wanarejea humo kwa humo. Mhe. Spika, pale kuna maeneo ya *VIP* unaweza kwenda ukaambiwa pamejaa lakini kuna maeneo ya *VIP* ukitoa dau kubwa, lakini *VIP* yenyewe na sitaki nizungumze siri za watu, inawezekana mtu amesogezwa pembeni unawekwa na wewe na kidogo inakuwa si utaratibu mzuri.

Kwa hiyo, ndio maana wenzetu hivi sasa wamejenga utamaduni makaburi wanaanza kujengea na zamani Zanzibar watu walikuwa hawana utamaduni wa kujengea makaburi, labda wale wenzetu waliotoka nchi mbali mbali, lakini kwa jamii yetu ya Kiswahili ukishaweka tuta pale pamoja na mbono, basi mtu anajua alama ni mbono, na hivi sasa mbono unakatwa na watu wanamsogeza pembeni kidogo na watu wanakuwekea.

Sasa mimi nadhani Mwanakwerekwe imefika pahala pameshajaa. Kwa maana hiyo, mimi nafikiri kwa kuwa sheria hii tunaitunga, basi ni vyema Mhe. Waziri aangalie eneo jengine kwa mfano kuna eneo lile tulilozikia wale maiti wetu waliopata na maafa, na wale wanakuwa hawapati dua sana mpaka atoke mtu huko msamaria mwema, mashekhe wanakwenda kuomba dua, sasa maeneo yale yangefunguliwa *public*, ili watu wakaendelea kwenda kuzikwa na wale wenzetu wanaendelea kupata dua nyengine. Mhe. Spika, vyenginevyo kuendelea kurudia maeneo hayo kwa hayo inakuwa kidogo si vizuri sana.

Jambo jengine katika masuala ya usafi na uhifadhi wa mazingira pamoja na afya ya jamii. Mhe. Spika, ujenzi wetu bado una matatizo, ambao haukuwa *planned* katika maeneo yetu ya kawaida na watu wanajenga ovyo, hawaweki maeneo ya kupita gari na wakati mwengine utakuta vyoo vinaelekezana na choo, na kidogo inakuwa si uzuri.

Sasa nafikiri katika haya maeneo yetu mapya Mhe. Spika nadhani kwa sababu tumeanza kuona, kuna baadhi ya maeneo kwa mfano kama Tunguu ukienda kule kuna watu wengine wamejenga katikati ya njia, na nyumba ile inajengwa ukiangalia ile *master plan* kwa sababu maeneo ya kule Tunguu angalau ile ramani imewekwa kitaalamu, lakini kuna baadhi ya nyumba zimejengwa katikati ya barabara. Kwa hivyo, leo mtu anakwenda kwenye kiwanja chake anakwenda kujenga ile sehemu ya mbele pale ndio kuna nyumba ya mtu na matokeo yake ile njia inakuwa haipo.
Kutokana na hali hiyo, kuna baadhi ya migogoro inaweza kujitokeza, kwa sababu mtu amepewa kiwanja cha *plan* kimepimwa kila kitu njia pande zote, lakini matokeo yake mtu amejenga chini ya njia.

Mhe. Spika, hivi sasa kwa wenzetu kwa mfano kama China na nchi nyengine kuna hii miji mipya ambayo inayojengwa hivi sasa, na kwa bahati nzuri kuna baadhi ya makampuni tumesikia yanaanza kuja hapa Zanzibar na makampuni hayo wao wanasema wanao uwezo wa kutafuta fedha, isipokuwa wao wapewe maeneo kwa ajili ya kujenga miji mipya kama mradi ambao uko pale Dar-es-Salaam, Kigamboni.

Kwa hivyo, maeneo kama yale hivi sasa Mhe. Spika na ndio miji ya wenzetu inavyojengwa na wenzetu Bara tayari wameshaanza, na sisi Wizara yetu ya Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati nafikiri Mhe. Waziri yupo pale nadhani na yeye yumo katika utaratibu wa kwenda huko.

Kwa kweli imefika pahala hivi sasa nyumba zetu tunajenga *style* ya vibanda, maana yake ni nyumba za kawaida, na wenzetu hivi sasa Mama Anna Tibaijuka pale anafunga mikataba na watu wa Kinondoni anawapelekea mji ambao tayari umeshakuwa *well planned* pale na unawekwa juu ya meza pale anawaambia Kinondoni nyumba zetu 1000 hizi na mji wenu utakuwa huu hapa, kwa mfano tutajenga *blocks* 100, pengine *blocks* 30 za watu wa Kinondoni ambao wapo hivi sasa, na nyumba zile zote zinavunjwa na kujengwa mji mpya wa kisasa na halafu baadaye wanapewa nyumba zao.

Mhe. Spika, mimi nafikiri kuna haja ya kuelekea huko hasa ukiangalia Zanzibar nchi yetu ni visiwa, lakini visiwa vyenyewe ni vizuri na wala bado havijajengwa kitaalamu.

Sasa tumesikia kuna makampuni yanaanza kuja katika utaratibu ule wa *PPP* namuomba sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ajaribu kukaa na watu hawa. Mhe. Spika, baadhi yapo wakati tulipokwenda Zambia tulikutana nao, na ulituona pale na tulifanya mazungumzo na tulikuwa mimi, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk lakini hivi sasa hayupo hapa.

Kwa hivyo, tunajaribu kutafuta wawekezaji ambao watakuja kuisaidia Zanzibar kuibadilisha wanasema wako tayari fedha zipo, na sisi tuwape maeneo wapi waweze kujenga majengo yale, ili baada ya muda fulani aidha wananchi au serikali iweze kulipa kidogo kidogo wenzetu ndivyo wanavyofanya.

Mhe. Spika, kwa kutegemea mshahara mtu ajenge nyumba, asomeshe watoto, atibu kwa kweli itachukua muda mrefu. Lakini kwa kushirikiana na kampuni kama hizi nadhani wananchi wetu wanaweza kupata nyumba za bei nafuu katika muda ambao watakaokubaliana na hao wawekezaji.

Vile vile maeneo kama yale utakuta yanajengwa kitaalamu kama vile vituo vya afya, *drainage system* kila kitu kinawekwa, na kuliko ilivyo hivi sasa wakati mwengine miji yetu bado iko kikawaida zaidi pamoja na kuangalia mipangilio ya miji.

Mhe. Spika, suala hili sio Dar-es-Salaam au labda kule Zambia wenzetu, lakini hata Rwanda pale kuna mji waliwapa wenzetu wa Malaysia. Kwa mfano, mimi nilikwenda kipindi kile wakati tulipokwenda kuangalia masuala ya usafi tukawakuta watu nyumba zao zimebomolewa mtaa mzima na kujengwa nyumba za muda zenye vyumba viwili na wamepewa, na tuliambiwa makaazi yao yatakuja kuwa pale pale lakini baada ya ule mji mpya kujengwa.

Kwa hivyo, tunahisi wenzetu wanaanza kuendelea katika hali kama hiyo. Sasa mimi nadhani masuala kama hayo, kwa sababu ukijenga mji mzuri bila ya shaka na masuala ya afya yanakuwa yanaimarika.

Jambo jengine ni kuhusu usumbufu. Mhe. Spika, katika suala zima la usumbufu, mimi ninaye rafiki yangu mmoja anaye mjomba wake ambaye alikwenda ulaya baharia. Amekaa miaka mingi tena jamaa mwenyewe ni mzanzibari alikuwa akikaa pale kwa Biziredi, lakini baada ya kurudi wakati meli yao ilipofika Mombasa pale akapata bibi wa pwani Mombasa akamuoa, kwa hiyo baada ya kurudi kwao akamalizia pale Mombasa.

Mhe. Spika, kipindi hicho ambacho nilikuwa nikienda Mombasa sana, lakini mimi sikuwahi kuoa, basi Mhe. Spika tulimkuta alikuwa na kesi, kwa mimi ambaye kipindi hicho sijaanza kuingia katika vyombo vya sheria nikaona ah! Mbona huyu wanamuonea na kesi yenyewe ilikuwa vipi, amekuja na *music system* anapiga mziki. Mhe. Spika katika majumba yale ya Mji Mkongwe kule Mombasa madongo yanaporomoka, yaani anafungua *full* mziki utafikiri labda yuko Ugiriki, ndio unajua *chain* tatu. *(Makofi)*

Mhe. Spika siku ya pili yake jirani yake amekwenda polisi na kupeleka malalamiko kwamba jana kucha sikulala ananipigia mziki, basi siku ya pili waraka wa polisi na amekwenda pale polisi na Mhe. Spika ameshtakiwa na kulipwa fedha za Kenya shilingi 15,000.

Sasa shilingi 15,000 fedha za Kenya katika miaka ya 1990 zilikuwa ni fedha nyingi sana, na kumbe wenzetu kule ile ni sheria yao, wanasema unapomuudhi mwenzako yaani ukifanya jambo katika nyumba yako likambughudhi mwenzako, basi anapokwenda kukushtaki unachukuliwa hatua za kisheria.

Kwa kweli wenzetu hivi sasa wanao utaalamu kwamba hizi kumbi za ma-*disco* zinakuwa zinajengewa mfano kama humu ndani ya Baraza la Wawakilishi humu Mhe. Spika utapiga mziki hapa mpaka asubuhi na hapo barabarani hasikii mtu.

Mhe. Spika, mimi nadhani katika sheria hii kwenye yale mambo ya kuondoa usumbufu pamoja na mambo mengine tuwawekee *conditions* hizi. Kwa mfano, Dodoma tu pale kwa wale waendaji wa Dodoma kuna ukumbi unaitwa 84, nikisema hivyo vijana wanacheka kwa sababu wanakujua 84, yaani watu wamekwenda kwenye uchaguzi ameshinda anamalizia 84 pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna ukumbi mdogo tu na huu ukumbi wetu tunaofanyia mkutano pale sehemu ya juu ni mkubwa, basi unapigwa mziki Mhe. Spika kwanza humuoni mtu, maana yake taa inawaka na kuzima hujawahi kumuangalia vizuri taa tayari imeshazima, basi mule vijana wanajirusha lakini nje hasikii mtu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nadhani tuanze na utaratibu huo kwa sababu kuna watu wanalalamika, wengine wanaumwa na miziki inakuwa mikubwa, pia kuna baadhi ya viongozi wa nchi wanakimbia majengo kwa sababu ya miziki, pengine hapo ulipohamia ukija mziki mwengine utahamia wapi. Mhe. Spika, nafikiri ni vyema hivi sasa tuweke utaratibu na sheria hii kama tutaifuata basi nadhani mambo mengi yataweza kutuepuka. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli suala la usumbufu sio sigara tu makuruhu kwenye daladala na mambo mengine, lakini mpaka na haya mambo mengine ambayo yanayosababisha athari kwa jamii. Mhe. Spika, naona unaniangalia basi naomba nimalizie dakika zangu tano zilizobakia, ili nisiweze kukiuka hizi taratibu zetu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, kwa kweli ni dakika tatu tena hiyo kwa upendeleo. *(Kicheko)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Tatu? Haya. Mhe. Spika, hapa kuna kitengo kimezungumzwa, suala la Kitengo cha Afya Bandarini. Mimi nadhani katika sheria hii labda kitiliwe nguvu kwa kuwekewa vitendea kazi. Hili Mheshimiwa ni jambo muhimu sana kwa nchi za visiwa. Nchi zetu za visiwa hizi tuna usafiri wa siku zote, kwa hiyo wanapoingia abiria pale Bandarini ni lazima suala la afya ni kitu muhimu.

Mhe. Spika, sasa hivi kuna maradhi ya miripuko mfano, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali. Jirani zetu Uganda hivi karibuni yaliingia maradhi ya *ebola*, tukajakusikia mpaka Tanzania Bara wakaanza kuweka *alert*. Lakini tunashukuru kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu maradhi yale hayakuwahi kufika hapa.

Kwa hiyo maeneo kama yale ya Bandarini kuweka vizuizi ni muhimu. Lakini sasa je, tutaweza ku-*control* vipi. Kwa sababu unaweza kuweka kizuizi cha kuangalia masuala ya afya ikiwa kuna taratibu za ukaguzi. Sijui bandari zetu kama kuna ukaguzi, ukiacha wale Wazungu. Maana sisi pale mtu unayemjua kwamba ni mgeni ni mzungu tu, lakini kwa mtu mwengine yeyote mwenye sura kama mimi anapita tu. Sasa sijui atakaguliwa vipi na hivi vitengo vya afya bandarini vinaweza vikafanya vipi hasa kwa abiria. Hili ni suala najaribu kulizungumza wenyewe Wizara ya Afya wajaribu hili kulifanyia utaratibu mzuri.

Jengine katika maeneo ya Bandarini kwa vyakula ambavyo zinavyoingia nchini. Mhe. Spika, hichi kitengo kilichokusudiwa humu nadhani sio kama kile cha kumlinda mlaji moja kwa moja, nadhani kitengo cha Afya Bandarini kuna bidhaa ambazo zinaingia zinakuwa zimeshakwisha wakati wake wa matumizi. Kuna maradhi mengi sasa hivi yanajitokeza ma-*pressure*, masukari, pengine labda kwa vitu ambavyo vinavyoingia kiholela katika maeneo yetu ya bandari.

Mhe. Spika, nadhani baada ya hayo machache nataka nimalizie la mwisho kabisa ili niweze kukaa kitako nizungumzie suala la taka. Sasa hivi kwa bahati nzuri kuna vikundi vinanunua taka. Mimi nadhani tushajihishe hivi vikundi vinavyonunua hizi taka kwa ajili ya kutengeneza mbolea na kukushanya chupa za plastiki na chupa za vigae, taka ni mali Mheshimiwa. Lakini bado kama hatujaweka mpango mzuri, nafikiri kwa sheria hii kama tulivyosema kama wataweza Halmashauri na Baraza la Manispaa kuwapa watu wa *private* mimi nadhani wale wanaweza wakatafuta masoko ili taka sasa ikawa mali baada ya kwamba taka inaleta uchafu ije iwe unanyang'anyiwa.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini naamini Mhe. Waziri Soko la Saateni ile Mikataba yetu na wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura Shehia ya Saateni na mimi nitaweza kupatiwa ufumbuzi. Lakini pamoja na hayo naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsanteni.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa wa kuchangia Mswada wetu huu unaozungumzia masuala mazima ya afya ya jamii pamoja na mazingira.

Mhe. Spika, kwa kweli huu Mswada ni muhimu sana, tunapozungumza jamii tunakusudia sote viongozi na wananchi tunaowaongoza. Hili suala ni nyeti sana, suala la afya yetu na ndio maisha yetu. Hili suala nimefurahi sana waheshimiwa wengi wamechangia kwa hamasa nzuri sana na kwa kututaka hasa wizara zetu mbili Wizara ya Afya na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais inayoshughulika na dhamana ya Tawala za Mikoa, kuhusiana na mambo ya uzoaji wa taka, usindikaji wake sisi ndio dhamana.

Ushauri mwingi umetolewa na Mhe. Spika, niseme tumeupokea. Kubwa na ninalotaka kusema mengi haya mambo yaliyokuwemo kwenye hii sheria ndio mambo yetu ya kawaida ya kazi. Lakini ni lazima nikiri kwamba ufanisi wetu haupo mia juu ya mia, tuna mapungufu. Mapungufu hayo mengi yanatokana na ufinyu wa zana za kufanyia kazi, hilo ndio tatizo kubwa sana. Kwa kweli Waheshimiwa mtakubaliana na miye vijana wanajitahidi sana juu ya ufinyu huo wa bajeti na zana za kufanyia kazi.

Nitatoa mfano hapo mnapo zungumza Darajani na siku zote huwa natoa mfano huo. Pale Darajani siku moja tu sisemi mbili, pale kama pasizolewe taka ndio hayo waheshimiwa wanayo yazungumza kila mmoja atapita kabana pua na itakuwa hapapitiki kabisa kabisa. Lakini tumejipanga na *Alhamdulillahi* niseme kwa kushirikiana na vikundi mbali mbali na wanahamasa, wanajamii ambao na wao wanakerwa na uchafu, wanataka mji wetu safi, tunaendelea kushirikiana na kupanga.

Alhamdulillahi pia mradi wa ZUSP nafikiri tumeshasema mara nyingi sana juu ya mipango yake na zana ambazo tunazitarajia. Matumaini yetu ni makubwa sana watakuja kutusaidia. Lakini hili alilomalizia Mhe. Hamza la *outsource* hiyo ni kweli na sisi tumeshasema mara nyingi milango yetu ipo wazi. Hata Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nakumbuka katika moja ya hotuba zake za ufunguzi alizungumza kwamba milango ya serikali ipo wazi, mwenye kampuni yoyote ambaye anataka kuja kuwekeza kwenye usafi wa miji yetu kama kwengine milango ipo wazi.

Tunashukuru zimejitokeza kama Kampuni mbili moja inataka kununua hizi chupa za plastiki zote wananunua hasa na kampuni nyengine wanataka kununua taka halafu watengeneze umeme. Bahati nzuri tunazungumza nao na *Alhamdulillah* nafasi hiyo sifikiri kama tutaiwacha, tutaitumia vizuri tuone tutafika wapi.
Mhe. Spika, nilikuwa naomba kusisitiza sana madhumuni ya Mswada huu. Madhumuni ya Mswada huu kama alivyoeleza mwenyewe Mhe. Waziri ni kutunga sheria zitakazosimamia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii. Hili ni suala la msingi kabisa katika sababu kubwa Mhe. Waziri ameleta Mswada huu. Ukipitia vifungu hivi vyote ambavyo waheshimiwa wamevichambua vizuri sana kwa kweli vifungu vyote ni vizuri. Kila kifungu kwa kweli kama tukivisimamia vizuri kila kifungu tukatekeleza ipasavyo, imani yangu kwamba mji wetu utakuwa safi. Na hivi vinanavyoitwa vitaharishi vya afya ya jamii tutavishinda.

Nitatoa mfano mdogo tu, Mhe. Hamza Hassan Juma, kule kwake kuna mto unaitwa Mtopepo. Mto ule umeanza juu kule, ule mto umeteremka mpaka unakwenda kwa Mheshimiwa wa jimbo la Mwembe Makumbi. Yale maji watu wanayatumia kwa namna mbali mbali, wengine wanafulia, wengine wanakogea, wengine wanafanya mambo makubwa tena humo humo na mikeka inaoshwa humo humo. Ndio maana *Cholera* kule haiondoki. *Cholera* ndio hayo miongoni mwa maradhi yanayoambukiza, vimelea vya *cholera* siku zote haviondoki, siku zote vinachukuliwa tu humo hivyo ndio vihatarishi.

Mhe. Spika, ukenda kule utacheka kuna nyumba kule ambazo hazina vyoo, mambo yote yanamiminwa humo humo mtoni. Kwa hiyo aliyekuwa juu ndio anafanya mambo yake vizuri, lakini aliyekuwa chini huku tena mambo yote anakoga yeye. Hio ndio hatari moja, ni lazima nyumba zetu ziwe na vyoo na tuvitumie hili ni suala la msingi kabisa. Haya mambo huko zamani au huko nyuma mabwana afya wetu walikuwa wakifanya kazi vizuri sana. Juzi tulitembelea bustanini hapo Migombani, tukakuta nyumba zaidi ya 20 utashangaa hazina vyoo, mambo yote yanaingia kwenye msingi yanaingia kwenye msingi mkubwa. Ni hatari sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, haya mambo kwa kweli yote yameelezwa kwenye sheria kwa vizuri kabisa. Mimi nimpongeze sana Waziri. Waheshimiwa wamezungumzia nakumbuka Mhe. Omar Ali Shehe, ule uundaji wa Baraza la Ushauri, nafikiri hii ni rai moja nzuri sana. Uzuri wa rai hii kwamba itawahusisha wale wadau wote kwenye Wizara ya Afya, Mabaraza ya Miji na Manispaa kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe sio Manispaa tu na Mabaraza ya Miji. Na mimi naomba hili tuliongeze katika marekebisho, nafikiri ni suala la msingi sana.

Suala jengine ambalo ni kubwa sana ni suala la Mwanasheria kuwemo humu, imeelezwa hapa kwamba atakuwemo Mwanasheria. Umuhimu wa Mwanasheria tatizo sio usimamiaji au ufatiliaji tatizo ni watu wengi kukiuka zile taratibu ziliopo na mtu anajua hasa hivi ninavyofanya mimi sivyo. Haya mengine mtu suala la usafi huhitaji mpaka wewe uhimizwe, usimamiwe, lakini inafika mahala inabidi tufanye sasa, tutumie askari, ili tuweke usafi. Kwa kweli haiingii akilini suala la usafi kuwa mtu ahimizwe. Wewe mwenyewe unaona kwamba hapa ninapokaa mazingira yake hayaridhishi. Kweli mazingira hayaridhishi unahitaji mpaka aje askari wa Maspaa, au askari gani akuhimize.

Mhe. Spika, hili nataka kusisitiza kwamba hili suala ni letu sote na sote tukereke. Ile tabia yetu tubadilike tuone kwamba hali ya usafi ni jukumu letu sote, kila mmoja ule moyo wake kama ni nyumbani kwako, mahali kwako unapofanyia kazi ukerwe na ule uchafu. Sote tukiwa katika hali hiyo kwa pamoja naamini tutafanikiwa. Lakini ukisema hiyo ni kazi yao Baraza la Manispaa, kazi yao Baraza la Mji tukuachie wewe utupe tu taka ovyo, nafikiri hivyo sivyo. Sasa hili mimi ningewaomba sana Waheshimiwa hasa sisi twenye majimbo ya Mijini humu tushirikiane.

Nashukuru kuna vikundi hivi vinatusaidia sana vile tulivyovianzisha, wanafanya kazi nzuri sana, Mji Mkongwe, vijana wa Malindi, Kwamtipura, Mkele na kwengineko kama Mombasa, wanafanya vijana wale wenyewe wemejikusanya, wamejiajiri wanazoa taka ni shilingi elfu tatu tatu tu kwa kila mwezi huna haja wewe kwenda kuzitupa, wanakuja kuchukua wao. Lakini kwengine inakera kidogo wanazitupa mahala ambapo sipo. Lakini hilo ni suala letu wenyewe la usimamizi tu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kusisitiza tu kwamba hili suala tumeshaliweka wazi, makampuni au vikundi vijitokeze na tutawapa mashirikiano na tutawasaidia na tutawalinda.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na naomba nisisitize suala la kupulizwa dawa katika kifungu 94 ukurasa wa 267. Tumefanikiwa sana katika mradi wa Malaria kwa njia mbali mbali, kwanza za kumdhibiti mbu na sisi wenyewe kulalia katika vyandarua vilivyotiwa dawa. Lakini haipendezi kuona baadhi yetu ikifika siku ya kutiwa dawa nyumba zetu tunafunga milango kwa kufuli ili wasije wale watiaji dawa, tunawapa lugha ambazo si nzuri. Dawa ile imetusaidia sana hasa katika mitaa ya Kilimani, Mazizini na kwengineko sehemu ya mabondeni bondeni ilikuwa malaria haiondoki lakini leo *Alhamdulillah* hali ni nzuri sana kwa dawa ile. Tena basi mbali ya wadudu wa malaria lakini hata vijidudu wengine, inasaidia sana.

Nimefurahi sana kuona Mhe. Waziri kwenye sheria yake hii hili suala nalo kaligusia. Pia nimefurahishwa kwenye ukurasa 266 Mhe. Waziri alipozungumza suala la cheti kutolewa kwa ukamilishaji chanjo. Kuna wengine hapigwi chanjo lakini kile cheti chake anakwenda kipigwe stempu tu ili apate kusafiri, pengine anaona zitampa tabu pengine zitampa homa. Kwa kweli si jambo zuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hii Sheria kama walivyosema Waheshimiwa wengine ukiisoma kwa makini na kwa undani kabisa na tukasimamia vizuri kwa pamoja sote, nashukuru Masheha, Madiwani, ningeomba na sisi waheshimiwa Wawakilishi kwenye majimbo tuwe nao viongozi hawa wenzetu wa chini, tufanye nao kazi pamoja kwa masuala ya usafi. Imani yangu kwamba tukifanya kazi kwa pamoja kwenye suala hili kwa kweli tutafanikiwa. Mifano mingi sana Waheshimiwa wamesema kama Rwanda na kwengineko wao wamekuja wao kwa umoja wao na ukweli wao na uwadilifu wao na sisi uwadilifu mimi nasema tunao, tunao kwenye mengine kwa nini tushindewe kwenye usafi.

Zamani mimi nasema hivyo kwa sababu sasa hivi kumebadilika sana. Mimi nilikaa Michenzani juu kule ghorafa ya sita mtu yupo anachukua pakacha anarusha. Siku moja nilikaa varanda nimepumzika kidogo mtu kesha kula wali wake basi ule uliobaki baki akaurusha tu, ukanijia wote kwenye tumbo. Basi na mimi nikatoka na tumbo langu vile vile nikampandia huko huko juu, nikamwambia Mzee ndio namna gani hebu tizama ulivyonirovya hivi. Asakasema aaah! Samahani, samahani, samahani sana. Samahani ndio lakini ndio umeshaniharibu, salama ndio ulikuwa wali tu. Sasa hayo ndio mambo ambayo kuwa tulikuwa tunafanya. Lakini sasa hivi *Alhamdulillah* sasa hivi watu niseme wamebadilika, kuna mipango mizuri tu imefanywa pale sasa, bustani zile zitaimarishwa zitawekwa sawa na taka watu tuzichukue.

Mheshimiwa naomba kusisitiza sana la watu kubadilika. Tubadilike, tukibadilika sote tukawa pamoja kwenye suala la usafi tutafanikiwa kabisa. Kumezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa pale Marikiti kwamba kuna taka zinatupwa za samaki, nyama mbovu na mambo mengine ya uchafu. Sisemi kama si kweli lakini nafikiri pengine mnapopita hizo taka ndio zipo kwenye njia ya kuondolewa. Mswada pia umezibagua hizi aina ya taka, kuna taka za gesi, taka maji, taka ngumu. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwenye Mswada wake kaziwekea utaratibu hizi aina za taka. Hizo taka zote tunazo.

Nakumbuka zamani Lumumba pale palikuwa na *incinerator* taka zile kama za Hospitali au matumbo kama hayo hazitupwi zile, zinakwenda pale zinachomwa. Sasa taka zile za afya nazo hazitupwi wana *incinerator* zao majiko yao ndani ya Hospitali, usiku wanazichoma zile. Kwa sababu huwezi taka za ndani za *operation* kuzitoa wakati wa mchana ni hatari. Sasa zile wanazichoma wenyewe pale pale hazendi kutupwa kwenye majaa makubwa.

Kwa hiyo ili suala la aina tofauti ya taka Mhe. Spika, ambazo waheshimiwa wamezungumza, mimi nakubali kweli inaweza ikawa ni bahati mbaya kwa watu wetu. Lakini hilo linalotendeka hasa huwa zinatengwa na hapo Darajani ndio kwenye njia za kupelekwa huko, kama hayo matumbo, taka gesi, taka maji na taka ngumu.

Mimi nashukuru kwamba hii sheria yote haya imeyaona na imeyafafanua vizuri sana na tutajitahidi sote kushirikiana, Mabaraza ya Miji, Baraza la Manispaa na Wizara pamoja ili tuone kwamba haya masuala ya usafi na usimamizi wa sheria. Waheshimiwa wengi wamezungumza sana suala la usimamizi wa sheria. Sisi tunao askari wetu wa Mabaraza ya Miji na Manispaa wanafika wanapigwa Mhe. Spika, ataogopa. Kweli yeye ni msimamizi lakini anapigwa, maana pale atamfurusha mtu, yule mtu anamwambia ngoja utaniona wewe. Anamfuata nyumbani

kwake usiku, anakwenda anamuita fulani anaitikia, anamwambia toka anatoka pale wanampiga mawe, wanamg'oa meno au wengine wana mapanga. Sasa hayo yanakuwa ni matatizo.

Vyombo vya Dola navyo tunaweza kutumia nguvu lakini kwa kweli tutumie nguvu kwa mambo kama haya ya usafi. Sasa tutajitahidi sana suala la elimu. Tuwaelimishe watu wetu, wafahamu na wao wafahamu kwamba hili suala ni letu sote, tushirikiane. Suala la elimu nalo Mhe. Waziri kalisisitiza sana na nafikiri tukishirikiana kwa pamoja sote tutafanikiwa.

Naomba nimalizie Mhe. Spika, kwa kusema kwamba ndani ya Mabaraza yetu ya Miji au Baraza la Manispaa tuna Kamati mbali mbali. Nitatoa mfano katika Baraza la Manispaa tuna:

- Kamati ya Fedha na Uchumi,
- Kamati ya Sheria na Utawala,
- Kamati ya Kazi, Ujenzi na Mazingira,
- Kamati ya Huduma za Jamii na Mipango Miji.

Haya mambo ukiyatizama yote haya Sheria hii kwa njia moja au nyengine imeyagusa. Ndio nasema hii sheria kwa kweli imechukua mambo mengi sana na haya yanatugusa sote. Sasa ni vizuri kwamba tutakuwa na sheria ambayo itasimamia. Zamani ndio ilikuwa ndio ile ya *Public Health Decree Cape of 73* kama alivyoitaja mwenyewe kwenye sheria yake.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuwaomba sana waheshimiwa kwamba tujitahidini sote tuwaelimishe watu wetu au wananchi wetu tusaidiane. Suala la usafi ni la pamoja ni suala letu sote. Tukikerwa na uchafu na uharibifu wa mazingira ni imani yangu kwamba tutafika tunapotaka na tutaleta haiba nzuri kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni kwa michango mbali mbali ambayo imetolewa. Tumekubaliana na Mhe. Waziri kwamba majumuisho yafanyike kesho baada ya kipindi cha Maswali ambapo Mhe. Naibu Waziri atatangulia kumsaidia Mhe. Waziri halafu baadaye Mhe. Waziri wa Afya amalizie majumuisho.

Kwa hiyo tukubaliane kusitisha shughuli hii hadi kesho ili kuja kumaliza kazi hii. Kutokana na hayo basi Waheshimiwa wajumbe naakhirisha Kikao hichi hadi kesho tarehe 11/10/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:20 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 11/10/2012 saa 3:00 za asubuhi)